JACKPOT BABA LAO!
TZS. 355,121,030
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 9

**AVUNJIKA** kiuno akiangua nazi usiku wa manane

Pata Bitcoin Africa ya bure kila lisaa.
Wekeza kuanzia $25.
Jiunge: kamatacrypto.com
Lipia Lipa No. 5727186.
vodacom | m-pesa



117060802


# Nipashe

Jumatatu Septemba 26, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581080

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# Magari ya serikali yalivyo hatari ajali



Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Wilboard Mtafungwa.

**TAKWIMU** vifo vya watendaji zashtua jeshi... *Endelea ukurasa 22*



Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa NMB, Filbert Mponzi (katikati), Meneja Mwandamizi wa Uhusiano wa Serikali wa benki hiyo, Amanda Feruzi (kulia) na Meneja Mwandamizi wa Uhusiano wa Biashara ya Nje ya Nchi, Lucy Kimei, wakifurahia tuzo ya Benki Bora ya Wateja Binafsi na Biashara Tanzania kwa Mwaka 2022 iliyotunukiwa benki hiyo, jijini London mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## CRDB yatimiza ahadi ya Rais Samia

UKURASA 8

UKURASA WA 2



### BOT YACHUKUA HATUA KUKABILI MFUMUKO BEI

GAVANA wa Benki Kuu (BoT), Prof. Florens Luoga amesema Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) imeiridhia benki hiyo kuendelea...

UKURASA WA 4

### NMB YASHINDA TENA TUZO YA BENKI BORA YA WATEJA BINAFSI

KWA mwaka wa pili mfululizo Benki ya NMB imeshinda tuzo ya benki kiongozi wa kuwahudumia wateja binafsi nchini...

UKURASA WA 7

### MTOTO ANAJISIWA CHOO CHA SHULE

MWANAFUNZI wa kike mwenye umri wa miaka sita (jina lake limehifadhiwa) anayesoma darasa la awali amedaiwa kunajisiwa na mtu ambaye hajajulikana, akiwa chooni katika Shule ya Msingi Bugimbagu, Kata ya Mwawaza, Manispaa...

## Wasiojulikana wamzuia Mbatia kuteta waandishi wa habari

UKURASA 2

**MICHEZO** MANDONGA MTU KAZI NA 'NDONGA' YA JICHO MTWARA UK.15

**KABWELA** UK. 7



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma jana kuhusu taarifa ya mkutano wa Mapitio ya Sera na Mitaala unaotarajiwa kufanyika kuanzia leo hadi Septemba 28. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wasiojulikana wazuia mkutano wa Mbatia

**Na Elizabeth Zaya**

KATIKA hali isiyo ya kawaida, jana James Mbatia, aliyetangazwa juzi kuvuliwa nafasi ya uenyekiti wa Chama cha NCCR-Mageuzi, alizuiwa na watu wasiojulikana kufanya mkutano na waandishi wa habari katika moja ya hoteli zilizoko Mikocheni mkoani Dar es Salaam.

Mwanasiasa huyo pia alilalamikia kile alichokiita kuingiliwa kwa uhuru wa mahakama na kutaka wadau kuingilia jambo hilo alilosema linadidimiza ukuaji wa vyama vya siasa nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari nje ya hoteli hiyo baada ya uongozi wa hoteli hiyo kumzuia kufanya mkutano aliokuwa amepanga, Mbatia alisema alikuwa ameshakamilisha taratibu zote za mkutano huo ikiwamo malipo kwa hoteli lakini baada ya kufika huko aliambiwa asingeruhusiwa kufanya kama walivyokuwa wamekubaliana awali.

"Tuliomba tufanye mkutano katika hoteli hii, lakini kwa bahati mbaya tumeambiwa kwamba haturuhusiwi tena kufanyia hapa.

"Na kabla sijafika hapa nikiwa na wakili wetu, tulipigiwa simu kwamba tusifanye mkutano huu, tuusitishe. "Na kweli tulivyofika tukazuiliwa, makubaliano yalikuwa yamefanyika na tulikuwa tumeshalipia. Kama wengine walizungumza jana (juzi) na wakafanya uamuzi wao, wananizuiaje mimi raia wa Tanzania kuzungumza?

"Inatusikitisha sana kwamba nchi yetu inaweza kufika hapa baada ya mfumo wa vyama vingi vya siasa. Vyama vingi vya siasa ni uhuru, na nchi yetu ina katiba ambayo inaelekeza umuhimu wa jamii kufanya majukumu yao bila kuvunja sheria," alilalamika Mbatia pasi na kumtaja aliyemzuia.

Mbatia pia alieleza kushangazwa na uamuzi uliofanyika dhidi yake juzi wakati wa mkutano mkuu wa dharura wa chama hicho jijini Dodoma uliowafukuza baadhi ya wanachama wake kwa kuwa shauri hilo lilikuwa limefikishwa mahakamani kwa ajili ya kutolea uamuzi.

Mbatia alikiomba Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS), Kituo cha Msaada wa Kisheria na viongozi wa dini na serikali kujadili na kuingilia kati suala hilo.

"Tusiruhusu taratibu zilizoko mahakamani zikaingiliwa, uhuru wake uko wapi? Niwaombe TLS, LHRC, TAWLA, taasisi za dini na zote za utetezi wa haki za binadamu pamoja na serikali kwa ujumla, kuona namna ya kulijadili hili jambo.

"Jana watu wamefanya mkutano na walikuwa wanalindwa, hivi ni nani asiyejua mchango wangu kwa taifa ndani ya mfumo wa vyama vingi vya siasa? Kosa langu ni nini? Yaani kutoa mawazo yangu. Kama wale wameshafanya uamuzi, kwanini wananinyima hata haki ya kuongea?" Alihoji.

Mbatia alisema ameshauriana na wanasheria wake kuwa na utulivu wa fikra na wachukue uamuzi sahihi.

Juzi mkutano mkuu wa dharura wa chama hicho jijini Dodoma uliwavua uanachama Mbatia na wanachama wengine.

Pia uliamua kuwafikisha wanaotuhumiwa kufanya ubadhirifu wa mali za chama mbele ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

# Majina 640 ufadhili Samia kuwekwa wazi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI kesho inatarajia kuweka wazi majina 640 ya wanafunzi waliofaulu vizuri masomo ya sayansi ambao wana sifa ya kupata ufadhili kupitia 'Samia Scholarship'.

Miongoni mwa vigezo vya kupata ufadhili huo ni kudahiliwa kwenye vyuo vikuu vya ndani ya nchi kusomea masomo ya sayansi, uhandisi na elimu tiba ambapo Sh. bilioni tatu zimetengwa kwa ajili yao.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda aliyasema hayo jana jijini hapo alipozungumza na waandishi wa habari.

"Septemba 27, (kesho) tunafungua rasmi tangazo la wanafunzi waliomaliza kidato cha sita na kufanya mitihani kupitia Baraza la Mitihani Taifa (NECTA) na kufaulu vizuri sana kwenye masomo ya sayansi ambao wanastahili kupewa Samia Scholarship, baada ya hapo majina yao yatatangazwa.

"Kwa wanafunzi ambao wamefanya vizuri sana katika masomo ya sayansi ambao wanastahili kupewa Samia Scholarship, tunayo majina 640, tutangaza na watajua endapo wataomba udahili katika masomo ya sayansi, basi watakuwa wanufaika wa ufadhili huu," alisema.

Waziri huyo alisema kwa mwanafunzi ambaye atadahiliwa kwenye masomo ambayo si ya sayansi, hawatanufaika na ufadhili huo hata kama jina lipo kwenye orodha ya walio na sifa ya kupata.

"Au umefaulu vizuri hapa umeamua kwenda kusoma nje, kuna mtu anakusomesha, basi jina litaandikwa hapa ulistahili kupata lakini hujadahiliwa katika chuo kikuu hapa Tanzania katika masomo ya sayansi, uhandisi na elimu tiba," alisema.

Kuhusu bajeti, waziri huyo alisema wameangalia wastani wa kumsomesha mwanafunzi chuo kikuu mwaka wa kwanza wakapata fedha hiyo (Sh. bilioni tatu) itatosha kwa wanafunzi 640.

"Tutakapoingia mwaka wa pili, inaweza kuwa Sh. bilioni sita na zitaendelea kuongezeka kulingana na uhitaji, hapa tutazindua tangazo lakini uzinduzi wa hii scholarship yenyewe tumemwomba Rais akutane na hao watakaokuwa wamekamilisha vigezo vyote," alisema.

Prof. Mkenda pia alisema wamezindua tuzo za waandishi bunifu zijulikanazo Tuzo za Mwalimu Nyerere.

"Tunaendelea kuwakaribisha waandishi bunifu wa riwaya na mashairi wawasilishe rasimu ya maandiko yao kwa kamati inayosimamiwa na Prof. Mlama, mwisho wa kupokea mawasilisho yao ni Novemba 30, 2022," alisema.

# BOT yachukua hatua kukabili mfumuko bei

**Na Maulid Mmbaga**

GAVANA wa Benki Kuu (BoT), Prof. Florens Luoga, amesema Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) imeiridhia benki hiyo kuendelea kupunguza taratibu kasi ya kuongezeka ukwasi kwenye uchumi kwa mwezi Septemba na Oktoba mwaka huu ili kupunguza kasi ya mfumuko wa bei.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa umma juzi, MPC ilifanya kikao Septemba 23, mwaka huu, ili kutathmini utekelezaji wa sera ya fedha na mwenendo wa uchumi kwa mwezi Julai na Agosti, ikibaini kilichosababisha kupanda kwa mfumuko wa bei ni ongezeko la bei za bidhaa katika soko la dunia.

Katika taarifa yake hiyo, gavana huyo alisema kwa kuzingatia tathmini ya mwenendo wa uchumi wa nchi na shida za kuongezeka kwa mfumuko wa bei za bidhaa nchini na duniani, uamuzi huo pia utalenga kukabiliana na athari za kuendelea kuongezeka kwa mfumuko wa bei na kulinda kasi ya ukuaji wa uchumi.

"Mfumuko wa bei nchini umeendelea, kwa upande wa Tanzania Bara umeongezeka na kufika asilimia 4.6 mwezi Agosti mwaka huu kutoka 3.6 mwezi Machi, kiwango ambacho kipo ndani ya lengo la wastani wa asilimia 5.4 kwa mwaka 2022/23. Kwa upande wa Zanzibar, umeongezeka kufikia asilimia 5.4 kutoka 3.5, kiasi ambacho ni juu kidogo ya lengo la asilimia tano.

Aliongeza kuwa katika robo ya kwanza ya mwaka huu, uchumi wa Tanzania Bara ulikua kwa asilimia 5.4, kulinganishwa na makadirio ya 4.7, ukuaji huo ukichangiwa na shughuli za kilimo, ujenzi, viwanda na uchimbaji wa madini.

Pia alisema kwa upande wa Zanzibar, uchumi umekua kwa asilimia 5.1, kulinganishwa na makadirio ya 5.4 kwa mwaka huu, ambao unatokana na kuimarika kwa shughuli za utalii, huku akieleza kuwa kutokana na mwenendo huo wa uchumi, kuna uwezekano mkubwa wa kufikia makadirio ya ukuaji wa uchumi wa nchi kwa mwaka huu.


## KUFUNGA KAMPUNI

WAMILIKI WA **FIDDY COMPANY LTD** ILIYOPO DAR-ES SALAAM KUNDUCHI YENYE USAJILI WA **NO.141790617.**

1. **HAFIDHI AMEIR**
2. **HADIJA AMEIR**
3. **ABDULMALIK AMEIR**
4. **YUSUPH AMEIR.**

WANAPENDA KUUTANGAZIA UMMA KUWA WAMEFUNGA KAMPUNI YAO KWA SABABU YA KUSHINDWA KUJIENDESHA /KUKOSA MTAJI. AZIMIO LA KUFUNGA KAMPUNI LILIFANYIKA TAREHE **09/08/2022.**



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MBEYA**

**SHAURI LA RUFAA YA ARDHI NA. 43/2022**

**(Asilia kutoka Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Mbeya)**

**AMKENI SACCOS..................................MRUFANI**

**DHIDI YA**

**1.PROSPER AUGUSTINO NGOLLO...........MRUFANIWA**
**2.ALOYCE MHAPA.................................MRUFANIWA**

**KWA: ALOYCE MHAPA**
**POPOTE ULIPO**

**KUITWA SHAURINI**

Unaamriwa na Mahakama hii,kuhudhuria hapa mahakamani siku ya tarehe 29/09/2022,siku ya Alhamisi saa 3:00 asubuhi bila kukosa.
ELEWA KWAMBA,ukikosa kufika siku hiyo,shauri litasikilizwa bila wewe kuwepo na uamuzi kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na muhuri wa Mahakama leo hii tarehe 05/09/2022.

THE HIGH COURT OF TANZANIA

**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MBEYA**



## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**EVA KONAWILLIAM KIWANGO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 914 AXP – NISSAN PATROL** yenye Chassis namba **WYY61800900.** Engine namba **RD28497994.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi.
Taarifa ya Polisi: **DAR/URA/RB/375468/202**

TANGAZO

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PRESIDENT'S OFFICE - REGIONAL ADMINISRTATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**MLELE DISTRICT COUNCIL**

# MLELE DISTRICT COUNCEL FINANCIAL STATEMENT FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2022

## STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT 30 JUNE 2021

| | Notes | 2021 TZS '000 | 2020 TZS '000 |
|---|---|---|---|
| **ASSETS** | | | |
| **Current assets** | | | |
| Cash and cash equivalents | 23 | 1,172,659 | 1,276,590 |
| Receivables and prepayments | 24 | 575,092 | 465,665 |
| Inventories | 25 | 82,450 | 101,399 |
| | | 1,830,201 | 1,843,654 |
| **Non-current assets** | | | |
| Other financial assets | 26 | 7,064 | 7,064 |
| Property, plant and equipment | 29 | 13,294,191 | 10,506,588 |
| | | 13,301,255 | 10,513,652 |
| **TOTAL ASSETS** | | 15,131,455 | 12,357,306 |
| **LIABILITIES** | | | |
| **Current liabilities** | | | |
| Deferred income | 11 | 166,879 | 23,560 |
| Payables | 34 | 311,768 | 498,483 |
| Employee benefits | 37 | 834,462 | 967,908 |
| Provisions | 38 | - | - |
| | | 1,313,109 | 1,489,951 |
| **Non-current liabilities** | | | |
| Deferred income | 40 | 819,295 | 995,125 |
| | | 819,295 | 995,125 |
| **TOTAL LIABILITIES** | | 2,132,404 | 2,485,076 |
| **NET ASSETS** | | 12,999,050 | 9,872,230 |
| **NET ASSETS** | | | |
| Accumulated surplus/(deficit) | | 12,984,922 | 9,858,102 |
| MCR | | 14,128 | 14,128 |
| **TOTAL NET ASSETS** | | 12,999,050 | 9,872,230 |

The Financial Statements for the year ended 30 June 2021 were authorized for issue by Councillors on 05/03/2022 and were signed on behalf of the Council by

Soud M. Mbogo
Council Chairman
05.03.2022
MWENYEKITI
HALMASHAURI YA WILAYA

Teresia A. Irafay
District Executive Director
05.03.2022
EXECUTIVE DIRECTOR
MLELE DISTRICT COUNCIL

## STATEMENT OF FINANCIAL PERFOMANCE FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2021

| | Notes | 2021 TZS '000 | 2020 TZS '000 |
|---|---|---|---|
| **Revenue** | | | |
| Local taxes | 9 | 940,566 | 905,717 |
| Fees, fines, penalties and licenses | 10 | 315,257 | 117,749 |
| Amortisation of recurrent grants | 11 | 5,993,276 | 5,711,740 |
| Revenue from exchange transactions | 13 | 29,091 | |
| Amortisation of capital grant | 40 | 3,077,991 | 2,312,416 |
| Other own source revenue | 16 | 157,641 | 82,113 |
| | | 10,513,822 | 9,129,735 |
| **Expenses** | | | |
| Wages, salaries and employee benefits | 17 | 5,691,784 | 5,273,444 |
| Supplies and consumables used | 18 | 987,751 | 1,120,355 |
| Maintenance expenses | 19 | 71,359 | 141,016 |
| Grants and other transfer payments | 20 | 168,233 | 109,197 |
| Depreciation of property, plant and equipment | 29 | 372,086 | 307,392 |
| Provision for bad debts (Defaulters) | 24 | 95,789 | 378,407 |
| | | 7,387,002 | 7,329,811 |
| **Surplus/(deficit) during the year** | | 3,126,820 | 1,799,924 |

The Financial Statements for the year ended 30 June 2021 were authorized for issue by Councillors on 05/03/2022 and were signed on behalf of the Council by

Soud M. Mbogo
Council Chairman
05.03.2022
MWENYEKITI
HALMASHAURI YA WILAYA

Teresia A. Irafay
District Executive Director
05.03.2022
EXECUTIVE DIRECTOR
MLELE DISTRICT COUNCIL

## STATEMENT OF CHANGE IN NET ASSETS FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2021

| | Accumulated surplus/deficit TZS '000 | MCR TZS '000 | Total TZS '000 |
|---|---|---|---|
| At 1 July 2018 | 9,934,657 | 7,064 | 9,941,721 |
| Prior year Adjustment | 7,064 | (7,064) | |
| Surplus/(deficit) for the year | 824,375 | - | 824,375 |
| Minimum Contribution Reserve (LGLB) Restated | (14,128) | 14,128 | - |
| At 30 June 2019 | 10,751,968 | 14,128 | 10,766,096 |
| At 1 July 2019 | 10,751,968 | 14,128 | 10,766,096 |
| Surplus/(deficit) for the year | 1,799,924 | - | 1,799,924 |
| Net Asset transfer to Ruwasa | (2,693,790) | | |
| At 30 June 2020 | 9,858,102 | 14,128 | 9,872,230 |
| At 1 July 2020 | 9,858,102 | 14,128 | 9,872,230 |
| Surplus/(deficit) for the year | 3,126,820 | - | 3,126,820 |
| At 30 June 2021 | 12,984,922 | 14,128 | 12,999,050 |

The Financial Statements for the year ended 30 June 2021 were authorized for issue by Councillors on 05/03/2022 and were signed on behalf of the Council by

Soud M. Mbogo
Council Chairman
05.03.2022
MWENYEKITI
HALMASHAURI YA WILAYA

Teresia A. Irafay
District Executive Director
05.03.2022
EXECUTIVE DIRECTOR
MLELE DISTRICT COUNCIL

## CASH FLOW STATEMENT FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2021

| | Note | 2021 TZS '000 | 2020 TZS '000 |
|---|---|---|---|
| **Cash flows from operating activities** | | | |
| ***Operating Receipts*** | | | |
| Local taxes | 9 | 844,777 | 556,350 |
| Fees, fines, penalties and licenses | 10 | 275,377 | 117,749 |
| Recurrent Grants Received | 11 | 6,150,871 | 5,729,357 |
| Capital Grants Received | 55 | 2,809,814 | 1,581,011 |
| Transfer from other Government entities (Transfer receipts) | 12 | - | - |
| Revenue from exchange transactions | 13 | 21,471 | - |
| Finance income | 14 | - | - |
| Other own source revenue | 16 | 157,641 | 82,113 |
| Change in Deposit Account | 41 | (27,207) | 33,298 |
| ***Operating Payments*** | | | |
| Wages, salaries and employee benefits | 17 | (5,822,845) | (4,983,770) |
| Amount transferred to exchequer- | 11 | (14,276) | (66,586) |
| Supplies and consumables used | 18 | (1,048,493) | (1,104,181) |
| Maintenance expenses | 19 | (106,944) | (171,062) |
| Grants and other transfer payments | 20 | (168,233) | (109,197) |
| **Net cash from operating activities** | | 3,071,953 | 1,665,082 |
| **Cash flows from investing activities** | | | |
| Purchase of property, plant and equipment | 55 | (2,953,489) | (2,255,666) |
| Purchase of property, plant and equipment (prepayment) | 55 | (165,356) | |
| Receipt from WYD groups | 38B | 47,961 | - |
| Grants and other transfer to Women | 38A | (105,000) | (115,950) |
| **Net cash from investing activities** | | (3,175,884) | (2,371,616) |
| **Cash flows from financing activities** | | - | - |
| Proceeds from borrowings | | - | - |
| Repayment of borrowings | | - | - |
| Grants transferred to deposit account | 0 | - | - |
| **Net cash used in financing activities** | | - | - |
| **Net increase in cash and cash equivalents** | | (103,931) | (706,534) |
| Cash and Cash Equivalents at Beginning of the Year | | 1,276,590 | 1,983,124 |
| **Cash and cash equivalents at end of the Year** | 24 | 1,172,659 | 1,276,590 |

The Financial Statements for the year ended 30 June 2021 were authorized for issue by Councillors on 05/03/2022 and were signed on behalf of the Council by

Soud M. Mbogo
Council Chairman
05.03.2022
MWENYEKITI
HALMASHAURI YA WILAYA

Teresia A. Irafay
District Executive Director
05.03.2022
EXECUTIVE DIRECTOR
MLELE DISTRICT COUNCIL

20

## 1.0 INDEPENDENT REPORT OF THE CONTROLLED AND AUDITER GENERAL

Hon. Chairperson of the Council,
Mlele District Council,
P.O. Box 686,
MPANDA.

### 1.1 REPORT ON THE AUDIT OF FINANCIAL STATEMENTS

**Qualified Opinion**

I have audited the Financial Statements of Mlele District Council, which comprise the Statement of Financial Position as at 30 June 2021 and the Statement of Financial Performance, Statement of Changes in Net Assets and Cash Flow Statement and the Statement of Comparison of Budget and Actual Amounts for the year then ended, as well as the Notes to the Financial Statements including A Summary of Significant Accounting Policies.

In my opinion, except for the effects of the matter described in the basis for qualified opinion section of my report, the accompanying Financial Statements present fairly in all material respects, the Financial Position of Mlele District Council as at 30 June 2021, and its Financial Performance and its Cash Flows for the year then ended in accordance with International Public Sector Accounting Standards (IPSAS) Accrual basis of accounting and the manner required by the Local Government Finances Act, Cap. 290 [R.E 2019].

**Basis for Qualified Opinion**

Under Note 24, Mlele District Council has reported collected revenue through POS not banked amounting to TZS 474,196,000; TZS 95,789,000 in 2020/21 and TZS 378,407,000 in 2019/20 which were all impaired due to uncertainties in recoverability.

I however noted that, of the impaired amount of TZS 474,196,000; no any legal actions have been taken in respect of TZS 132,157,577 against staff and revenue collecting agents including reporting the matter to investigative organs to warranty the disclosure of contingent asset in line with IPSAS 19.

I conducted my audit in accordance with International Standards of Supreme Audit Institutions (ISSAIs). My responsibilities under those standards are further described in the Auditor's Responsibilities for the audit of the Financial Statements section of my report. I am independent of Mlele District Council in accordance with the International Ethics Standards Board for Accountants' Code of Ethics for Professional Accountants (IESBA Code) together with the National Board of Accountants and Auditors (NBAA) Code of Ethics, and I have fulfilled my other ethical responsibilities in accordance with these requirements.

I believe that the audit evidence I have obtained is sufficient and appropriate to provide a basis for my opinion.

### .2 REPORT ON COMPLIANCE WITH LEGISLATIONS

**Compliance with the Public Procurement Act, 2011 (as amended by the Public Procurement (Amendment) Act, 2016)**

**Subject matter: Compliance audit on procurement of works, goods and services**

I performed a compliance audit on procurement of works, goods and services for Mlele District Council for the financial year 2020/21 as per the Public Procurement Laws in Tanzania.

**Conclusion**

Based on the audit work performed, I state that, except for the matters described below, procurement of goods, works and services of Mlele District Council is generally in compliance with the requirements of the Public Procurement Laws in Tanzania.

**(a) Annual Procurement Plan (APP) was not confirmed to have been approved by the budget approving authority and published in tender portal**

Regulation 69(7) of the Public Procurement Regulations, 2013 requires a procuring entity to draw up procurement plans for those requirements for which sufficient funds have been included in the approved budget, in the current financial year or if payment is due in the subsequent financial year, such payment has to be budgeted for. Further, Regulation 18(3) of the same Regulations states that, "A procuring entity shall publish the summary in the Journal and a full general procurement notice in the Tenders' Portal at least one month prior to any publication or notification of a tender or a request for proposals to prospective tenderers".

However, the annual procurement plan prepared by Mlele District Council for the year 2020/21 was not published in the general procurement notice through PPRA Tender Portal. Also, there was no evidence on whether the Annual Procurement Plan was approved by the budget approving authority as required by the aforementioned Regulations.

**(b) Non-use of Tanzania National e-Procurement system (TANePs) by the Council for procurements**

Regulation 342 of the Public Procurement Regulations, 2013 requires e-PPs to be implemented by all procuring entities in full or partially in parallel with the conventional manual procedures. Also, a Public Notice issued by PPRA on 20 August 2019 announced full application of TANePS with effect from the financial year 2019/20.

Mlele District Council did not use the system for all procurements made during the financial year 2020/21 contrary to the above-mentioned Regulation.

**(c) Performance bond not renewed to cover the extended time period TZS 439,016,506**

Regulation 29(6) of the Public Procurement Regulations, 2013 as amended by Regulation 12 of the Public Procurement (Amendment) Regulations, 2016 requires the performance security to be kept by the procuring entity until the final completion of the contract and shall be released after issuance of the certificate of acceptance of the final report or certificate of completion of works or services if there is no claim filed against the tenderer, contract guarantor or the surety company.

Performance bond for contract No. LGA.154/2018/2019/W/SS/01 amounting to TZS 2,195,082,530 between Mlele District Council and SUMA JKT for the construction of Mlele District Council Administration Block was not renewed following an extension of the completion time from 11 March 2021 to 06 September 2021 contrary to the aforementioned Regulation. Absence of performance security (bond) exposes the Council to the risk of losing its resources for on-going project in case contractor fail to execute the contract in full.

Charles E. Kichere
**Controller and Auditor General,**
**Dodoma, United Republic of Tanzania.**
**21 March 2022**

217060002

HABARI KITAIFA

# NMB yashinda tena tuzo ya Benki Bora Wateja Binafsi

**Na Mwandishi Wetu**

KWA mwaka wa pili mfululizo Benki ya NMB imeshinda tuzo ya benki kiongozi wa kuwahudumia wateja binafsi nchini kutokana na ubora wa huduma zake kukidhi mahitaji ya huduma za kifedha za umma wa walio wengi.

NMB ilitunukiwa tuzo ya Benki Bora ya Wateja Binafsi Tanzania kwa mwaka 2022 kwenye hafla ya tuzo za Global Banking and Finance (GBAF) zilizofanyika London, Uingereza.

Tuzo hizo zilianzishwa mwaka 2011 na Jarida la Global Banking & Finance Review lenye wasomaji zaidi ya milioni tatu ulimwenguni kote na ambalo shughuli yake kubwa ni kuangazia matukio na maendeleo ya kifedha duniani.

Akizungumza kwenye hafla ya kutoa zawadi kwa washindi wa tuzo za mwaka huu, Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa NMB, Filbert Mponzi, alisema ushindi wa benki hiyo ni kutambuliwa kwa dhamira yake thabiti ya kuwawezesha wateja na kulihudumia kikamilifu taifa kwa ujumla.

"Kwetu sisi NMB, mteja na huduma jumuishi za fedha ndiyo msingi wa shughuli zetu zote. Tunatoa huduma nafuu za kifedha kwa wateja zaidi ya milioni tano Tanzania nzima," Mponzi alibainisha kwenye hotuba yake ya kupokea tuzo hiyo.

"Tunawahudumia wateja binafsi wa aina mbalimbali wakiwamo wakulima wadogo, watumishi wa umma, wafanyakazi wa sekta binafsi na wajasiriamali wa kada zote kuanzia ile ya chini kabisa hadi wale wa kati. Kwenye hilo hatuna mpinzani. Tupo kwa asilimia 100 katika wilaya zote nchini," Mponzi alisema.

Aliwaambia waliohudhuria hafla hiyo kuwa NMB inaongoza kwa kuwa na mtandao mpana wa usambazaji huduma wenye matawi 227 ambayo asilimia 70 yapo maeneo ya vijijini na zaidi ya NMB Wakala 15,000 pamoja na zaidi ya mashine za kutolea pesa 750.

Mponzi pia alisema NMB imekuwa kinara wa maendeleo ya kidijitali nchini huku akibainisha maeneo kadhaa ambayo benki hiyo imeyaanzisha ikiwamo kuwa benki ya kwanza Tanzania kuwa na mawakala wanaotumia simu za mkononi.

Vilevile, alisema NMB imekuwa benki ya kwanza Tanzania kuwakopesha wateja wake kidijitali na benki ya kwanza kuwawezesha wajasiriamali kuwa na uwezo wa kukubali malipo ya kidijitali kwa njia ya msimbo wa QR.



Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi (katikati), Meneja Mwandamizi wa Mahusiano ya Serikali wa benki hiyo, Amanda Feruzi (kulia) na Meneja Mwandamizi wa Mahusiano ya Biashara ya Nje ya Nchi, Lucy Kimei (kushoto), wakifurahia tuzo ya Benki Bora ya Wateja Binafsi na Biashara Tanzania kwa mwaka 2022 kutoka jarida la Global Banking and Finance baada ya hafla ya ugawaji tuzo iliyofanyika London, Uingereza hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

"Dira na mkakati wetu wa sasa hivi na siku zijazo ni kuendelea kutumia maendeleo ya teknolojia za kidijitali kutuwezesha kulisukuma gurudumu la huduma jumuishi za kifedha kwa kutoa huduma zinazohimilika, rahisi na zinazofikiwa na wengi kwa wepesi," alibainisha.

Mponzi alisema mafanikio makubwa iliyonayo NMB yasingewezekana bila mchango na msaada wa serikali na Benki Kuu ya Tanzania (BoT), akisisitiza wameisaidia benki hiyo kustawi na kushamili kwa kuweka mazingira wezeshi na rafiki ya biashara na shughuli za kibenki.

Pia alibainisha kuwa mipango na ushirikiano wa benki hiyo na wadau wake wote umeiwezesha kuwa na matokeo chanya kwenye jamii na kupelekea kuaminika sokoni. Hali hii imepelekea kukua kwa amana za wateja kwa asilimia 24 hadi Sh. trilioni 6.5 mwaka 2021.

Kwa mujibu wa Mponzi, tuzo hiyo ni uthibitisho wa umakini, ari na dhamira ya wafanyakazi zaidi ya 3,500 wa NMB kuhakikisha benki hiyo siyo tu ni Benki Bora ya Wateja Tanzania, bali pia ni benki bora kuliko zote nchini.


NMB Close to you

## Appointment of **Mr. Ramadhani Mwikalo** as the **New Board Director of NMB Bank Plc.**



The Board of Directors of NMB Bank Plc (the Board) is pleased to announce Mr. Ramadhani Mwikalo as a new independent Director of the Board. Following the competitive selection process for onboarding an independent Director, Mr. Mwikalo was appointed as an independent Board member by the shareholders of NMB Bank Plc on 3rd June 2022 during its 22nd Annual General Meeting. After that, he obtained the Bank of Tanzania's approval to join the Board.

Mr. Mwikalo, a longstanding ICT savant, works as an Independent Consultant. He has over 40 years of hands-on working experience in the Technology Sector. His areas of expertise include Digital Strategy Formulation, Enhancements, and Integration of transformational digital banking platforms and process engineering and automation to enhance the overall customer experience.

He is recognized both nationally and internationally. Nationally, Mr. Mwikalo contributed to developing various core Government service delivery digital systems. In the international cycles, he worked in the United States (Silicon Valley) and has registered three ICT patents in Biometrics identification and Blockchain technologies with United States Patents and Trademarks Office (USTPO).

Mr. Mwikalo holds a Master's Degree in Engineering from the University of Ottawa, Ontario, Canada, and is a registered Professional Engineer in Ontario, Canada. He is also registered with ICT Commission in Tanzania as ICT Professional.

Mr. Mwikalo brings into NMB a wealth of experience and professional wisdom in areas of Technology and digitalization as the Bank has embarked on (and continues to) its customer-centric digital transformation journey. Accordingly, we kindly welcome Mr. Mwikalo to the Board and wish him abundant success in the service. At the same time, the Board and Management of NMB Bank Plc take this opportunity to congratulate Mr. Ramadhani Mwikalo on his appointment.

**Dr. Edwin P. Mhede**
**Board Chairman**

www.nmbbank.co.tz

217062602

# MATANGAZO

NMB Close to you

## Appointment of **Mr. Clement Esau Mwinuka** as the **New Board Director of NMB Bank Plc.**



The Board of Directors of NMB Bank Plc (the Board) is pleased to announce Mr. Clement Esau Mwinuka as a new independent Director of the Board. In line with the competitive selection process for recruitment of independent Directors, Mr. Mwinuka was appointed as an independent Board member by the shareholders of NMB Bank Plc on 3rd June 2022 during its 22nd Annual General Meeting. After that, he obtained the Bank of Tanzania's approval to join the Board.

Mr. Mwinuka is a multidisciplinary and seasoned professional. Currently, he serves as an Independent Consultant in broad-based business management for vibrant private sector development. He has had a distinguished career with over 30 years of working experience in Governance, Risk Management, Business Continuity, Strategy, Financial Management, and Audit in various Government Institutions and International Organizations. He held different management roles within Tanzania and at the SADC Secretariat.

He is highly recognized for his contribution to the development of the Community.

Mr. Mwinuka holds a Masters' of Science in Economic Management Policy (Industrialization, Trade & Economic Policy) and a Masters' of Science in Finance both from the University of Strathclyde, Glasgow, Scotland. He also holds Advanced Diploma in Certified Accountancy (ADCA) from Mzumbe University (MU) and is an Associate member of Certified Public Accountants in Tanzania, CPA (T).

Mr. Mwinuka brings to the Board valuable insights, a wealth of tremendous experience, and professional wisdom in the crucial areas of Governance, Financial Management, Audit, and Risk Management. We warmly welcome Mr. Mwinuka to the Board. Accordingly, we wish him abundant success in the service. At the same time, the Board and Management of NMB Bank Plc take this opportunity to congratulate Mr. Clement Esau Mwinuka on his appointment.

**Dr. Edwin P. Mhede**
**Board Chairman**

www.nmbbank.co.tz

NMB Close to you

## Appointment of **Mr. Aziz Jumanne Dachi** as the **New Board Director of NMB Bank Plc.**



The Board of Directors of NMB Bank Plc (the Board) happily announces Mr. Aziz Jumanne Dachi as a new Board Director representing the Government. Mr. Dachi was appointed as a Board member by the shareholders of NMB Bank Plc on 3rd June 2022 during its 22nd Annual General Meeting. He obtained the Bank of Tanzania's approval to join the Board.

Mr. Dachi has well grounded in IT and system audits. He serves as an Assistant Auditor General Technical Support Services at the honorable National Audit Office of Tanzania (NAOT) with 18 years of hands-on experience in government entities and International Organizations. He is highly recognized for auditing ICT systems and participating in Government negotiations with various stakeholders and development counterparts.

Professionally, Mr. Dachi has a multidisciplinary educational background. He holds a Bachelor of Science Degree in Computer Science from the University of Dar es Salaam and is an Associate Certified Public Accountant (ACPA) and Certified Information Systems Auditor (CISA).

Mr. Dachi brings to the Board invaluable lessons from his work, his deep understanding of IT-cum-Audit functions, and a wealth of experience in the areas of Systems Audit, Technology and Innovation, and Governance. Accordingly, we kindly welcome Mr. Dachi to the Board and wish him abundant accomplishment in the service. Similarly, the Board and Management of NMB Bank Plc take this opportunity to congratulate Mr. Dachi on his appointment.

**Dr. Edwin P. Mhede**
**Board Chairman**

www.nmbbank.co.tz

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga, Azam tunataka historia CAF

**WAWAKILISHI** wa nchi kwenye michuano ya Afrika kwa ngazi ya klabu, Simba, Yanga, Azam FC kwa Tanzania Bara na Kipanga FC kwa Tanzania Visiwani, kwa sasa wapo kwenye maandalizi kuelekea raundi ya kwanza ya michuano hiyo itakayoanza kutimua vumbi kati ya Oktoba 7-9, mwaka huu.


Simba ambayo inaiwakilisha nchi kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, imetinga raundi hiyo ya kwanza baada ya kuitoa Nyasa Big Bullets ya Malawi kwa jumla ya mabao 4-0, ikishinda 2-0 ugenini na kupata ushindi kama huo nyumbani, Uwanja wa Benjamin Mkapa na sasa watakutana na Primeiro de Agosto ya Angola iliyoitoa Red Arrows ya Zambia kwa jumla ya mabao 2-1 wakishinda 1-0 ugenini na nyumbani kutoka sare ya 1-1. Wawakilishi wengine wa nchi kwenye Ligi ya Mabingwa, Yanga wenyewe wametinga hatua hiyo kwa kuitoa Zalan FC ya Sudan Kusini kwa jumla ya mabao 9-0 wakishinda 4-0 mechi ya ugenini na 5-0 ya nyumbani, ila michezo yote ilipigwa hapa nchini Uwanja wa Benjamin Mkapa kutokana na hali ya usalama nchini kwao kutokuwa shwari, hivyo sasa watakutana na Al Hilal ya Sudan iliyoitupa nje St. George kwa faida ya bao la ugenini baada ya mechi ya ugenini kukubali kipigo cha mabao 2-1 nchini Ethiopia na nyumbani kushinda bao 1-0

Azam FC ambayo inaiwakilisha Tanzania Bara kwenye Kombe la Shirikisho Afrika, yenyewe inaanzia moja kwa moja raundi ya kwanza, ambapo itacheza dhidi ya Al Akhdar ya Libya iliyotinga raundi ya kwanza kwa kuitoa Al-Ahli Khartoum kwa jumla ya mabao 3-0 huku Kipanga FC inayoiwakilisha Tanzania Visiwani kwenye Kombe la Shirikisho Afrika, imetinga raundi hiyo kwa kuitoa Al Hilal Wau ya Sudan Kusini kwa mikwaju ya penalti 4-3 kutokana na matokeo ya bao 1-1 nyumbani na ugenini na sasa itakuna na ya Club Africain ya Tunisia Hivyo, ni hatua nzuri kwa wawakilishi wetu hao, jambo ambalo tunatarajia kuona wakiiwezesha nchi kuweka rekodi kwa mara ya kwanza kuingiza timu nne ama hata tatu kwa msimu mmoja katika hatua ya makundi.

Tunaamini kwa usajili uliofanywa na klabu zetu msimu huu, hilo linawezekana endapo zitautumia vizuri muda uliosalia wa takriban wiki mbili kabla mechi hizo kupigwa Yanga ikianzia nyumbani dhidi ya Al Hilal, Simba ugenini nchini Angola, Azam nayo ugenini Libya huku Kipanga FC ikianzia nyumbani dhidi ya Club Africain ya Tunisia. Kinachotupa matumaini hayo makubwa si usajili tu, bali hata mechi za kirafiki za kujipima nguvu ambazo zimekuwa zikicheza tangu wakati wa maandalizi ya msimu mpya na wakati huu wa mapumziko ya Kalenda ya Fifa, pia zinazidi kujenga imani kwetu kwa wao kwenda kufanya vizuri kwenye michuano hiyo na kuiwezesha nchi kuweka rekodi. Azam FC imetoka nchini Zambia kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya TP Mazembe na kutoka sare ya bao 1-1, kipimo ambacho ni kizuri kwao, jana usiku Simba ilitarajiwa kucheza dhidi ya Malindi SC ya Zanzibar katika Uwanja wa Amaan visiwani huko kabla ya keshokutwa kushuka tena dimbani hapo kujipima nguvu na Kipanga FC huku Yanga nayo ikiendelea mazoezi kambini kwao Kigamboni.

Hivyo, kama mabenchi ya ufundi ya timu hizo watazitumia vema mechi hizo kurekebisha kila aina ya makosa wanayoyabaini na kuwajenga ari, kisaikolojia na kujiamini kwa wachezaji wao, hatuoni sababu yoyote kwa wawakilishi wetu hao kushindwa kutinga hatua ya makundi. Endapo pia, Simba na Yanga zitapata matokeo ya jumla nyumbani na ugenini, zitafuzu moja kwa moja hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa, lakini zikitolewa zitaangukia kucheza mechi za mchujo na timu zitakazovuka raundi ya kwanza ya Kombe la Shirikisho ili kuwania nafasi ya kucheza hatua ya makundi ya michuano hiyo, hivyo tunazitakia maandalizi mema.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Waamuzi Bongo watawachosha wawekezaji

**LIGI** Kuu Tanzania Bara imesimama kupisha mechi za timu za taifa zilizo kwenye Kalenda ya FIFA, lakini hapa Bongo mjadala ambao bado unaendelea ni juu ya waamuzi.

Baadhi yao wamepelekwa kwenye Kamati ya Waamuzi kwa ajili ya kuangalia kama wanaweza kupata adhabu gani kutokana na kushindwa kumudu baadhi ya mechi.

Hao ni Ahmed Aragija ambaye Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania Bara inasema alishindwa kumudu mechi kati ya Yanga dhidi ya Azam, lakini Prisons, na Amina Kyando ambaye yeye ameambiwa hakumudu mechi kati ya timu Namungo dhidi ya Coastal Union.

Kuna waamuzi wasaidizi wawili, Frank Komba ambaye ameambiwa hakumudu mechi kati ya Yanga dhidi ya Azam iliyochezeshwa na Aragija, lakini Black Tubuke naye amepelekwa huko baada ya kushindwa kumsaidia mwamuzi Aragija kwenye mechi kati ya Prisons dhidi ya Simba.

Kwa hili lililotokea ni kama msiba mkubwa kwenye soka la Tanzania ambalo wengi wanataka lisonge mbele kwa sababu Aragija na Komba ndiyo waamuzi wa kiwango cha juu kabisa hapa nchini.

Aragija ndiye mwamuzi bora msimu uliopita wakati Komba amekuwa akiiwakilisha na kuitangaza nchi kwenye mechi nyingi za kimataifa. Haijulikani wamepatwa na nini.

Kama waaamuzi wetu tegemeo na ni taswira ya nchi wamekuwa wakipepesa kwenye maamuzi yao, iweje hao wengine ambao hawana uzoefu sana, itakuwaje?

Na kama hawa ndiyo waamuzi bora na wameboronga, je wamefanya hivi kwa bahati mbaya au kwa makusudi? Na kama ni makusudi, kitu gani kimewasukuma?

Haya ndiyo maswali ambayo mashabiki wengi wamekuwa wakijiuliza. Hii ni raundi ya nne tu ya Ligi Kuu, lakini imeonekana mapema tu kuwa matatizo mengi ya waamuzi ambayo yanasababisha baadhi ya timu zilizotakiwa kupata ushindi kwa uwezo wao zishindwe kufanya hivyo kwa maamuzi mabovu ya waamuzi.

Ni kweli waamuzi nao ni binadamu na wanafanya makosa, lakini waamuzi wetu wamekuwa na makosa ambayo ukifutilia utagundua yana aina fulani ya uonevu na wala si makosa ya kibinadamu. Makosa ambayo yanaamua matokeo ya mechi nzima. Hivi sasa baadhi ya makocha wamekuwa wakilalamika 'kunyongwa' kwenye baadhi ya mechi kutokana na maamuzi mabovu.

Hans Van der Pluijm wa Singida Big Stars, Charles Boniface Mkwasa wa Ruvu Shooting na hata makocha wa Mbeya City.

Msimu huu ligi imekuwa ni ngumu mno tofauti na msimu uliopita. Wafadhili na wawekezaji wamewekeza pesa nyingi kwenye klabu, kusajili wachezaji wazuri toka pande zote za dunia, mishahara mizuri, posho, miundombinu kama vile kununuliwa mabasi mazuri ya wachezaji, makocha wenye viwango vya juu, vifaa vya mazoezi, lakini wanakuja kuangushwa na waamuzi ambao hawako makini au wanafanya makusudi. Hii ni aibu kubwa kwa soka la Tanzania.

Itafika wakati wawekezaji watachoka kuwekeza, kwani sababu haina maana mtu anawekeza vitu vyote hivyo na timu yake iko vizuri uwanjani, lakini mwamuzi kwa utashi wake anaamua matokeo yawe anavyotaka yeye.

Mwekezaji anaweza kuachana na soka na kuamua kufanya kitu kingine kwa sababu anaona anapoteza pesa nyingi, bila kuona faida, kwani pamoja na timu yake kustahili kushinda, inalazimishwa kufungwa.

Itafika wakati sasa mashabiki wataanza kudai waamuzi wawe wanatoka nje ya nchi kama ilivyo kwa wachezaji na makocha. Kama mpaka Mwenyekiti wa Kamati ya Waamuzi wanafikia kuomba radhi, basi hali ni mbaya. Na mimi wala sitowapinga, kwani wanaweza kuja kutuonyesha viwango halisi vya timu zetu za Ligi Kuu Tanzania Bara. Inawezekana kuna timu zinashinda lakini hazina viwango hivyo, na kuna timu ambazo tunaona ni vibonde kumbe zinafanywa hivyo kwa makusudi.

Nadhani Bodi ya Ligi sasa ifikirie kuweka kanuni ya kualika au kuchukua waamuzi kutoka nje ya nchi kuchezesha baadhi ya mechi za Ligi Kuu ili kuwafanya hawa wa ndani kuona umuhimu wa kutenda haki pale wanapopewa nafasi.

Hii inaweza kuwafanya kushtuka kidogo na kuimarisha viwango vyao kwa kuona wageni wanaweza kuwapiga bao.

Nasema kama hali hii itaendelea nina wasiwasi wadhamini na wawekezaji wataondoka kwenye soka la Tanzania, kwani inaonyesha badala ya timu kushinda kwa uwezo wake ili soka likue, kumbe kuna timu zinatakiwa kushinda na zingine hazitakiwi licha kuwa zina uwezo huo.

## HABARI KITAIFA



Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana, akipata maelezo jinsi mradi wa SHARPP ulivyofanya kazi katika hafla iliyofanyika wilayani Chunya, mkoani Mbeya, baada ya Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) kufikia ukomo wa ufadhili wa Programu ya Uhifadhi Nyanda za Juu Kusini na Ruaha-Katavi (SHARPP) uliokuwa unatekelezwa na Shirika la Hifadhi ya Wanyamapori Duniani (WCS). **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Mume, mke jela kwa mauaji

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza iliyoketi Geita, imewahukumu mume na mke, wakazi wa Kijiji cha Budoda, Wilaya ya Bukombe, Karume Kakunda (76) na Roza Mayunga (68) kifungo cha mwaka mmoja na miezi minne jela au kulipa faini ya Sh. 600,000 kwa kumuua bila kukusudia Nzengo Nestory.

Hukumu hiyo imetolewa na Jaji Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Jaji John Kahyoza baada ya washtakiwa hao kukiri kosa na kumtaka Wakili wa Serikali, Winfrida Erenest kuwasomea washtakiwa maelezo ya awali.

Akisoma maelezo ya awali, Wakili wa Serikali Erenest alidai mahakamani humo kuwa Nzengo alikuwa na mgogoro wa ardhi na mshtakiwa Kakunda na shauri lao lilikuwa kwenye Baraza la Ardhi la Wilaya na katika shauri hilo Nestory alishinda.

Alidai kuwa wakati Nzengo yuko kwenye mchakato wa kutekeleza hukumu ya shauri lake, Machi 3, mwaka 2017, majira ya jioni, Nestory akiwa na dalali na karani wa baraza hilo, walifika nyumbani kwa mshtakiwa Kakunda kwa ajili ya kumpatia barua ya wito wa baraza na nyaraka za utekelezaji wa hukumu ya kesi.

Alisema mshtakiwa Kakunda alikataa kupokea na kutia saini barua hiyo, hivyo Nzengo na dalali walibandika mbele ya nyumba ya mshtakiwa huyo.

Wakili Winfrida alidai wakati dalali na Nestory wakibandika wito huo wa kwenye nyumba ya mshtakiwa, washtakiwa wote kwa pamoja walipiga kelele huku wakimpiga kichwani kwa marungu, ndipo majirani na wanakijiji wengine wapolifika eneo la tukio na kukuta ameshafariki dunia.

Alidai baada ya kuona amefariki dunia, washtakiwa wote kwa pamoja walikimbia na kwenda kusikojulikana.

Alidai dalali na karani wa baraza nao walikimbia na kutokomea kusikojulikana wakamwacha Nestory akipata kipigo kutoka kwa washtakiwa ambao ni wanandoa.

Alidai mshtakiwa wa kwanza Roza Mayunga (68) alikamatwa Mei, mwaka 2017 na mshtakiwa wa pili Kakunda alikamatwa Agosti mwaka 2018 na wote walipohojiwa, walikiri kumuua.

Baada ya Wakili wa Serikali Ernest kumaliza kuwasomea washtakiwa maelezo ya awali, Jaji Kahyoza aliwahoji washtakiwa na wote walikiri kutekeleza mauaji hayo kutokana na ugomvi uliokuwapo.

Jaji Kahyoza alisema "Washtakiwa wamekiri kosa wenyewe bila ya kulazimishwa, hivyo mahakama hii imewaona mnayo hatia, pia Mahakama hii inawatia hatiani kwa kosa la kuua bila ya kukusudia na mahakamani hii inawataka mjitetee ili iweze kuwapunguzia adhabu."

Washtakiwa wote kwa pamoja walikuwa wakiongozwa na Wakili wa Kujitegemea Laurent Bugoti ambaye alidai hapo mahakamani kuwa wateja wake wamekaa gerezani mwaka mmoja na kwamba wana umri mkubwa na wana wajukuu watano wanaowategemea.

Jaji Kahyoza baada ya kusikiliza utetezi huo, aliwahukumu kifungo cha mwaka mmoja na miezi minne jela au kulipa faini ya Sh. 600,000 na akasisitiza wanayo haki ya kukata rufani kama hamjaridhika na hukumu. Washtakiwa wote walilipa faini ya Sh. 600,000 na kuachiwa huru.

# Mtoto anajisiwa choo cha shule

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MWANAFUNZI wa kike mwenye umri wa miaka sita (jina lake limehifadhiwa) anayesoma darasa la awali amedaiwa kunajisiwa na mtu ambaye hajajulikana, akiwa chooni katika Shule ya Msingi Bugimbagu, Kata ya Mwawaza, Manispaa ya Shinyanga.

Babu wa mtoto huyo (jina tunalo) alisema jana kuwa mjukuu wake alikutwa akiwa amenajisiwa chooni shuleni huko Septemba 15, mwaka huu, na mtu ambaye hajafahamika.

Alisema kuwa baada ya kufanyiwa unyama huo, mtoto huyo alipoteza fahamu na alikutwa amelala chini huku akiwa anatokwa damu nyingi sehemu za faragha.

Alisema taarifa za kunajisiwa mjukuu wake alizipata kutoka kwa wanafunzi wenzake ambao walimwambia kwamba mwenzo alikutwa chooni akiwa amelala na hawezi kutembea na alikuwa anatokwa damu.

Babu huyo alisema baada ya kupata taarifa hiyo aliendа shuleni kufuatilia na kumkuta katika hali mbaya ikabidi ampeleke hospitalini.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Neema Ngongi, alikiri kutokea kwa tukio hilo na kwamba mwanafunzi huyo alikutwa na mwanafunzi mwenzake eneo la choo cha shule huku akiwa hawezi kutembea.

Alisema baada ya kubaini tatizo hilo, alitoa taarifa kwa kamati ya shule na uongozi wa kijiji na walipofika walimpeleka polisi kwenye dawati la jinsia na baadaye hospitalini.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga, Dk. Luzila John, alisema walimpokea mtoto huyo na baada ya uchuguzi, ilibainika kuwa alikuwa na michubuko sehemu za siri na kuchanika kutokana na kuingiliwa.

Alisema walimpatia huduma ya kwanza na kumlaza na kwamba sasa anaendelea vizuri na ameruhusiwa kwenda nyumbani lakini anatakiwa kurejeshwa hospitalini baada ya wiki mbili ili kuona maendeleo ya afya yake na vipimo vingine vya vinasaba kwenda kwa Mkemia Mkuu wa Serikali ili kuendelea na uchunguzi wa tukio hilo.

Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Janeth Magomi, alithibitisha kutokea kwa tukio la kunajisiwa mtoto huyo na wanamska aliyefanya kitendo hicho.

**Babu huyo alisema baada ya kupata taarifa hiyo alienda shuleni kufuatilia na kumkuta katika hali mbaya ikabidi ampeleke hospitalini.**


## FORESTRY DEVELOPMENT TRUST IRINGA

## MNADA WA HADHARA:

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE** Kwa idhini waliyopewa na **Forestry Development Trust** watauza kwa mnada wa hadhara magari matatu (3) aina ya Toyota Hilux Double Cabin tarehe 1 Okitoba, 2022, Jumamosi kuanzia saa 4:00 asubuhi. Mnada utafanyika kwenye viwanja vya Royal Palm, Mtaa wa Ahmadiya Iringa Mjini.

Magari yatakayouzwa:

| Idadi | Aina | Model | Mwaka | Ushuru |
|---|---|---|---|---|
| 3 | Toyota Hilux Double Cabin | 2KD Diesel Engine | 2013 / 2015 | Umelipwa |

Gari zote zinaweza kukaguliwa kwenye viwanja vya Royal Palm Mtaa wa Ahmadiya kuanzia tarehe 29 mpaka 30 September, 2022 Saa 3:00 asubuhi mpaka Saa 11:00 jioni.

**MASHARTI YA MNADA.**

1 Mnunuzi wa atatakiwa kulipa 25% pale pale na salio lilipwe ndani ya siku 7 za kazi mwisho wa kulipa ni tarehe 11 Okitoba, 2022 saa 10:00 jioni, Forestry Development Trust`s account number 01520243222700 CRDB Bank ukishindwa kulipa kwa muda huo Gari litauzwa kwa mshindi mwingine aliyefuata na dhamana haitarudishwa.

2 Gari zote zitauzwa kama zilivyo bila dhamana.

3 Malipo kwa njia ya VISA na Master card za CRDB bank yanakubalika au pesa taslimu (hundi na miamala ya simu haipokelewi)

4 Mnunuzi atawajibika kulipa kodi zote na gharama za kuhamisha umiliki.

5 Magari yote yaliyouzwa yataweza kuondolewa baada ya mnunuzi kulipa malipo yote na kuhamisha umiliki wa gari husika.

6 Kila mtu atatakiwa kuwa na bid namba itakayo patikana getini.

**Kwa maelezo zaidi waone:**
**UNIVERSAL AUCTION CENTRE**
**PLOT NO: 5 "E" LION STREET SINZA** **DAR ES SALAAM**
**CELL NO: 0754 284 926** **E-mail: universalauction@hotmail.com.**

217060602


## KABWELA



## UWT yasaka wataalamu wa kuzalisha, kusambaza chaki

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

JUMUIYA ya Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Kibaha Mjini inatarajia kuanza mchakato wa kutafuta wataalamu watakaosaidia kutengeneza chaki na kuzisambaza kwenye shule ili kuondokana na utegemezi.

Katibu wa UWT wa wilaya hiyo, Mariam Mugasha, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki alipotoa taarifa ya jumuiya hiyo kwenye mkutano mkuu wa uchaguzi uliofanyika Picha ya Ndege, Halmashauri ya Mji Kibaha.

Alisema tayari wana mashine ya kuzalisha chaki na kwamba kinachofuata ni kupata wataalamu wa kutengeneza bidhaa hiyo ili mradi huo uanze kuingiza kipato.

Pia alisema wanatarajia kutembelea shule za halmashauri hiyo kuzungumza na wanafunzi kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia hususani kwa watoto wa kike ambavyo vinaonekana kukithiri kwa sasa.

"Malengo yetu ni kukomesha vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia, hivyo baada ya ziara tutafanya kongamano la watoto wa kike tukiwa na mada za elimu ya kupinga vitendo vya ukatili, watambue namna gani ya kuviepuka, tukomeshe hali hii kwenye jamii zetu," alisema Mugasha.

Akizungumza katika mkutano huo baada ya kushinda kuwa Mwenyekiti wa UWT Kibaha Mjini, Elina Mgonja aliahidi kuwaunganisha wanawake kwenye kupinga utegemezi na badala yake wajikite kwenye uzalishaji.

Awali akitangaza matokeo, Msimamizi wa Uchaguzi huo, Nasri Mkalipa ambaye ni Katibu wa Umoja wa Vijana wa CCM Wilaya ya Kisarawe, alisema wagombea wa nafasi ya mwenyekiti walikuwa watatu na Mgonja ndiye ameibuka mshindi kwa kura 165, dhidi ya Batuli Maero aliyepata kura 72 na Caroline Malekela aliyeambulia kura moja.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (kushoto), akiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Ufadhili la Agence Française de Développement Group, Françoise Lombard, alipotembelea Makao Makuu ya AFD mjini Paris, Ufaransa mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CRDB yatekeleza ahadi ya Samia kufungua uchumi

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA ziara yake ya kwanza ya kikazi Kenya, Rais Samia Suluhu Hassan, pamoja na mambo mengine, aliahidi kuifungua nchi kiuchumi alipozungumza kwenye mkutano maalum na viongozi wa sekta binafsi.

"Tunakwenda kufungua nchi, Kenya kuna Uhuru ikimaanisha uhuru wa kufanya biashara; Tanzania kuna Suluhu, maana yake ni suluhu za vikwazo vya kibiashara, mpira sasa uko kwenye himaya yenu," Rais Samia alisema huku akipigiwa kofi na jumuiya za wafanyabiashara wa Kenya na Tanzania.

Miongoni mwa vikwazo vingi vinavyoikabili sekta binafsi katika nchi kama Tanzania ni mahali pa kupata mikopo nafuu ili kuwekeza kama mtaji.

Tayari sekta ya fedha nchini imeitikia vyema mageuzi ya biashara na kiuchumi ya Rais Samia.

"Sisi kama sekta ya fedha tuna wajibu wa kuunga mkono juhudi za serikali katika kukuza uchumi kwa kutoa fedha kwa sekta ya umma na binafsi," alisema jana Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekele ambaye yuko ziarani Ufaransa kukutana na washirika wake na wawekezaji ikiwamo Shirika la Fedha la Proparco.

Nsekela ambaye anaongoza ujumbe wa benki hiyo, ameahidi kuimarisha utoaji wa mikopo kwa kuongeza kiasi cha fedha za mikopo kupitia uanzishwaji wa ushirikiano na taasisi za fedha za kimataifa kama vile Proparco na nyingine.

Benki ya CRDB ambayo kwa mara ya kwanza ilitia saini ya makubaliano ya ushirikiano na Proparco kupitia Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Ufaransa (AFD) linalojihusisha na ukopeshaji wa kibiashara, inataka kupanua wigo wa ushirikiano na taasisi hiyo yenye makao yake makuu jijini Paris.

Machi mwaka huu, CRDB na Proparco zilitia saini makubaliano ya zaidi ya Sh. bilioni 182 kwa ajili ya kuongeza uwezo wake wa kukopesha wafanyabiashara wadogo na wa kati nchini.

Kiasi hicho kilikuwa katika mfumo wa dhamana ya mikopo ambapo tangu makubaliano hayo fedha hizo zimeelekezwa kufadhili wajasiriamali kulingana na ajenda ya ukuaji wa uchumi wa nchi kwa kuzingatia biashara zinazoongozwa na wanawake ambazo zinaanza kutengemaa kutokana na athari za mlipuko wa janga la UVIKO-19.

Proparco, sehemu ya Agence Française de Development Group (AFD Group), hutoa ufadhili na usaidizi wa biashara kwa taasisi za kifedha barani Afrika, Asia, Amerika Kusini na Mashariki ya Kati. Baada ya kupata mafanikio makubwa kutoka katika ufadhili wa awali, CRDB imeona kuna fursa zaidi ya kushirikiana.

Nsekela alisema majadiliano yao na Mkurugenzi Mtendaji wa Proparco, Françoise Lombard yalijikita katika kukuza uwezo wa CRDB katika kufadhili sekta binafsi, kusaidia uwezeshaji wa wajasiriamali walioathirika na janga la Uviko-19 pamoja na kuziba pengo la ufadhili kwa wajasiriamali wanawake Tanzania na Burundi ambako benki hiyo ina kampuni tanzu.

"Tunafuraha kuimarisha ushirikiano wetu na Proparco yanayolenga kuwezesha maendeleo endelevu na shirikishi. Tuko tayari kuongeza ushirikiano wetu na kutumia utaalamu wetu kufikia ajenda kabambe ya kusaidia ukuaji wa watu wetu na uchumi kwa ujumla," alibainisha.

Nsekela alisema kuwa baada ya miezi michache ya ushirikiano na Proparco, wamebaini kuna fursa nyingi kwa benki hiyo kukuza biashara yake na uchumi wa Tanzania.

Alisema menejimenti yake ina imani kuwa ushirikiano huo utaongeza mtaji wa Benki ya CRDB, hivyo kukuza ukwasi wake wa kutoa mikopo katika nyanja zote za uchumi.

"Sishangai kwamba wawekezaji wanataka kushiriki katika uchumi wa Tanzania kwani Rais wetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan anafanya kazi kubwa katika kufungua uchumi wa nchi na kuhakikisha kuwa nchi inafikia malengo yake ya kiuchumi," alisema.

Kuhusu ushirikiano wa pande hizo mbili, Mkurugenzi Mtendaji wa Proparco, Françoise Lombard, alisema, "Ushirikiano kati ya taasisi za fedha ni muhimu katika kusaidia maendeleo ya sekta binafsi na ukuaji wa uchumi.

"Nimefurahishwa na utayari wa CRDB kuongeza ushirikiano kwani inaonyesha nia yao ya kusaidia biashara na wajasiriamali Tanzania, ambayo inaendana na lengo la Proparco."

Lombard aliongeza kuwa pamoja na msaada wa kifedha, wamejadili kutoa msaada wa kitaalamu kwa CRDB ili kuboresha mbinu za benki hiyo za utoaji mikopo na kusaidia ubunifu wa bidhaa na hivyo kuongeza thamani ya uwekezaji wa Proparco na benki hiyo katika maendeleo ya taifa.

Kwa mujibu wa Lamborda, Tanzania ina uwezo mkubwa wa kukua kiuchumi kwa kuwa eneo lake la kimkakati la kijiografia na wingi wa shughuli za kiuchumi.

"Ukuaji unawezekana tu ikiwa taasisi za fedha zitakuwa tayari kufadhili sekta za uchumi. Benki ya CRDB imeonyesha nia ya dhati ya kuwa sehemu ya safari ya mabadiliko ya Tanzania," alisema.

Huko Ufaransa, ujumbe wa Benki ya CRDB pia umekutana na taasisi za serikali, benki na wafanyabiashara kujadili fursa mbalimbali za uwekezaji zilizoko Tanzania.

Baadhi ya taasisi hizo ni; Business France - Idara ya Biashara ya Ufaransa inayohusika na kusaidia maendeleo ya kimataifa ya uchumi wa Ufaransa, Bpifrance - Benki ya Uwekezaji wa Umma, na SH Biaugeaud - kampuni inayojishughulisha na usindikaji wa matunda na mboga.

Benki ya CRDB mwaka huu pekee imeingia mikataba ya mikopo na dhamana ya zaidi ya Sh. bilioni 500 na mashirika ya Proparco USAID na DFC, IFC, AfDB na AGF kusaidia biashara na SME nchini.

Juni mwaka huu Benki ya CRDB, Shirika la Misaada la Marekani (USAID) na Shirika la Fedha la Maendeleo la Marekani (DFC) walitia saini mkataba wa kuwezesha mikopo ya Sh. bilioni 100.

Benki ya CRDB ndiyo benki kubwa zaidi Tanzania, ikiwa na mizania yenye thamani ya zaidi ya Sh. trilioni 10. Kwa mujibu wa taarifa yake ya fedha ya nusu mwaka, benki hiyo ndiyo inayoongoza kwa kufadhili uchumi wa Tanzania, ikiwa na mikopo ya zaidi ya Sh. trilioni sita.

Benki ya CRDB pia imeorodheshwa miongoni mwa taasisi 10 bora na salama zaidi kuwekeza barani Afrika na Moody`s Investors Services. Moody's imeipa Benki ya CRDB daraja la "B1" ambalo ni la juu zaidi kuwahi kushikiliwa na taasisi za fedha kusini mwa Jangwa la Sahara. Hii imezivutia taasisi nyingi za fedha za kimataifa kushirikiana na Benki ya CRDB.

## Ziara Samia Ubelgiji yaleta neema nchini

**Na Elizabeth Zaya**

ZIARA ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyoifanya Ubelgiji Februari mwaka huu, imezaa matunda baada ya nchi hiyo kutangaza fursa mbalimbali kwa Watanzania.

Akizungumza na waandishi wa habari kwa njia ya mtandao mwishoni mwa wiki, Balozi wa Tanzania Ubelgiji, Jestas Nyamanga, alitaja sekta ambazo fursa zake zinapatikana katika nchi hiyo kuwa ni kilimo, miundombinu, uvuvi, uchumi wa buluu, miundombinu, utalii, elimu na uwekezaji.

Alisema Tanzania imepata fursa ya mikopo mbalimbali kupitia Umoja wa Ulaya na benki zilizopo katika nchi hiyo huku mikoa ya Kigoma, Rukwa na Tabora ikinufaika zaidi na fursa hizo ikiwamo kuboreshewa viwanja vya ndege na kupata fursa ya kuinua katika sekta ya kilimo.

"Kwa sasa tumeanza majadiliano nao kwa ajili ya kuanzisha miradi mingine itakayochukua miaka mitano na Ubelgiji imekubali kutenga Sh. bilioni 67 kwa ajili ya kusaidia katika miradi ya elimu ya sekondari mkoani Kigoma.

"Tuna soko kubwa sana hapa Ubelgiji kwa ajili ya minofu ya samaki hususani sangara wanaotoka Mwanza. Na tunaingiza kati ya tani 50 mpaka 60 kila wiki, zinatumika hapa Ubelgiji na kiasi kingine kinakwenda nchi zingine zikiwamo za Umoja wa Ulaya (EU). Tunaweza kuingiza zaidi, hata tani 200 kila wiki kama tukijipanga. Na fursa hiyo ipo pia kwa dagaa.

"Tunashukuru ziara ya Rais Samia aliyoifanya Ubelgiji imefungua fursa nyingi sana. Rais alikutana na wafanyabiashara wakubwa sana na baada ya pale tumeanza kuona kufunguka kwa fursa nyingi.

Alisema fursa zingine zilizoko huko ni soko la mchele kutoka mkoani Mbeya na kokoa na tayari wameshaanza kuuza mchele kutoka Kyela, Morogoro na maeneo mengine.

Kuhusu zao la parachichi, balozi huyo alisema lina soko kubwa na maparachini yanayopendwa zaidi ni yenye rangi ya kijani, akibainisha kuwa moja kwa sasa nchini humo linauzwa kwa zaidi ya Sh. 10,000.

Alisema pilipili na samaki aina ya migebuka ni fursa nyingine ya kibiashara kati ya Tanzania na Ubelgiji na kwamba kuna fursa za mikopo kwa mashirika na kampuni zinazotaka ziwasiliane na ubalozi.

Balozi huyo alisema wamekubaliana na EU kuwapatia Sh. bilioni 23 ili kusaidia uzalishaji wa asali yenye viwango vinavyotakiwa katika mikoa ya Kigoma, Tabora, Singida, Katavi na Rukwa, pia kisiwani Pemba.

Alisema EU imeahidi kutoa Sh. trilioni mbili kwa ajili ya miradi mbalimbali kuanzia mwaka 2021 hadi 2027, huku msisitizo ukiwa kwenye uchumi wa buluu.

Kwa mujibu wa Balozi Nyamanga, Euro milioni 75 (Sh. bilioni 168.727) zitatumika kubadili mfumo wa mwonekano wa miji ya Mbeya, Mwanza, Tanga na Pemba na Euro milioni 70 (Sh. biloni 157.478) zitasaidia mkakati wa kuwa na usawa wa kijinsia.

# Avunjika kiuno akiangua nazi usiku wa manani

**Na Said Hamdani,** LINDI

HADIJA Magomba (25), mkazi wa Kijiji cha Mchakama, Wilaya ya Kilwa mkoani Lindi, amevunjika kiuno na mkono baada ya kuanguka kwenye mnazi alikodaiwa kupanda ili kuchukua nazi.

Tukio hilo lililowashangaza wengi lilitokea Septemba 14, mwaka huu, majira ya saa saba usiku kijijini huko.

Wakizungumza na Nipashe kuhusu tukio hilo, Ofisa Mtendaji wa Kijiji hicho, Mkwepu Ally, Mwenyekiti wa Kijiji, Mohamedi Mpinga na mmiliki wa shamba, Jonas Timotheo, walithibitisha kutokea kwa tukio hilo.

Mkwepu alisema siku hiyo, akiwa amelala nyumbani kwake, alipigiwa simu na mwenyekiti wa kijiji hicho, Mpinga, akimwagiza kumpatia Hadija barua ya kwenda kupata matibabu kwenye zahanati ya kijiji.

"Nilipigwa na mshangao mkubwa mno usiku huu mwanamke alikuwa anafanya nini!" Mkwepu alisimulia.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Mpinga alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa Hadija, akiwa ameambatana na rafiki yake, walikwenda kwenye shamba hilo kwa ajili ya kuchukua nazi.

"Baada ya kupanda kwenye mnazi huo mrefu, mpenzi wake ambaye wamezaa mtoto mmoja, alibaki chini kuokota nazi zilizodondoshwa.

"Wakati nazi hizo zikidondoka juu ya mti, walinzi wa shamba walitoka huku wakimulika kwa tochi kwenye shamba hilo na walipomulika mnazi aliokuwa amepanda, huyo mwanamke alidondoka kutoka juu na mwanaume aliyekuwa naye alikimbia," alidai.

Mwenyekiti huyo alisema kishindo cha kuanguka na kelele alizokuwa anapiga Hadija kutokana na maumivu ziliwafanya walinzi hao kwenda kumwangalia, wakikuta alishaangua nazi nne.

Mmiliki wa shamba hilo, Timotheo alisema walinzi wake walitoka baada ya kusikia mbwa akibweka na walimulika sehemu mbalimbali lakini hawakuona kitu na walirejea ndani lakini muda mfupi baadaye walisikia kitu kimeanguka na kusikia kelele. "Nimepatwa na mshangao mkubwa kusikia mwanamke anapanda juu ya mnazi tena mrefu zaidi ya mita 50, tena usiku, mara nyingi kazi hii inafanywa na wanaume," alisema Timotheo.

Mtoa huduma wa zahanati ya kijiji ambaye hakutaka kutajwa jina gazetini kwa maelezo kuwa siyo msemaji, alithibitisha kupokewa kwa majeruhi huyo ambaye alihamishiwa Hospitali ya Wilaya ya Kilwa, Kinyonga kutokana na kubainika kupata shida kubwa kiafya.



Wananchi wa Kijiji cha Namalembo, Kata ya Msikisi, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, mkoani Mtwara, wakipanga foleni ya madumu kwa ajili ya kupata huduma ya maji kutokana na kata hiyo kukabiliwa na ukosefu wa majisafi kwa miaka mingi sasa. **PICHA: HAMISI NASRI**

# Wizara, wadau kujifungia kujadili mabadiliko mitaala

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imepanga kujifungia kwa siku tatu na wadau wa elimu wakiwamo wanazuoni, ili kujadili mapitio ya Sera ya Elimu na mabadiliko ya mitaala.

Mkutano huo wa wadau utafanyika jijini Dodoma kuanzia leo hadi Septemba 28 ukijumuisha wahadhiri, waajiri, wadau wa maendeleo, taasisi za umma na binafsi, taasisi za dini, taasisi za uendeshaji wa lugha, wabunge na timu ya Zanzibar inayoshughulikia sera na mitaala.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapo, Waziri wa Elimu, Prof. Adolf Mkenda alisema wadau hao ni kutoka sekta mbalimbali nchini na majadiliano hayo yatatokana na hatua iliyofikiwa ya mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 na mitaala baada ya kukusanya maoni mengi ya wadau ambayo yametolewa.

"Jumuiya za kitaalamu, taasisi za sayansi na utafiti, kesho (leo) tutazindua majadiliano ambayo yatakuwa ya ndani kwa sababu tunataka kupitia rasimu ambazo tunazo sasa hivi, tukimaliza tutakuwa na kongamano la wazi la siku tatu, tarehe itatangazwa," alisema.

Aliwataja wadau wengine ni pamoja na makamu wakuu wa vyuo vya elimu ya juu vya umma na binafsi, maofisa elimu mkoa na wadhibiti ubora wa elimu.

Alisisitiza kuwa wanaendelea kupokea maoni na kwamba pamoja na kuwa suala la elimu siyo la muungano, wanawashirikisha wataalamu kutoka Zanzibar ambao nao wana kamati ya mapitio ya mitaala.

"Tumekusanya maoni mengi na mengine yanakinzana, hivyo tumeamua tuwalete wadau wa elimu kwa pamoja, tunataka tukae nao tuonyeshe kwamba baada ya kukusanya maoni tunacho hiki na tutawagawia rasimu ya mitaala na mapitio ya sera mapema.

"Tutajifungia kuona namna gani tunapata rasimu ambayo ina mwafaka mkubwa zaidi na muda wowote kati ya mwezi Oktoba na Novemba tutakuwa na Kongamano la Elimu la siku tatu ambapo tutaweka hadharani rasimu zote," alisema.

Waziri huyo alisema lengo la wizara ni kuhakikisha ifikapo Desemba rasimu ya mitaala na ile ya mapitio ya sera ziwe tayari kwa ajili ya mchakato wa uamuzi.

# Wasafiri wanaoingia nchini kupimwa ebola

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

MKOA wa Kagera umeanza kuwapima virusi vya ugonjwa wa ebola wasafiri wote wanaoingia nchini kupitia katika mipaka iliyoko mkoani humo.

Imebainishwa kuwa watakaobainika kuwa na ugonjwa huo, hawataruhusiwa kuingia nchini ili kudhibiti ugonjwa huo ambao umegundulika katika Wilaya ya Mubende, Uganda.

Akizungumza na Nipashe ofisini kwake mwishoni mwa wiki, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Dk. Issessander Kaniki, alisema mbali na kuimarisha vipimo na uchunguzi katika mipaka yote, pia wanatoa elimu kwa wananchi, wenyeviti wa vitongoji na vijiji, watendaji wa vijiji na kata na watumishi wa afya walioko mipakani namna ya kudhibiti ugonjwa huo.

Dk. Kaniki alisema wametenga maeneo ya dharura kwenye mipaka yote ambayo yanaweza kutumika endapo litatokea tatizo hilo. "Ugonjwa huu uligundulika Uganda katika Wilaya ya Mubende ambayo inapakana kabisa na Mkoa wa Kagera kupitia Wilaya za Kyerwa, Karagwe, Missenyi na Bukoba, lakini katika visiwa karibia vyote vilivyoko katika Wilaya ya Muleba, tumechukua tahadhari zote katika mipaka yote rasmi na isiyo rasmi," alisema Dk. Kaniki.

Alisema kuwa mbali na kuongeza vituo vya uchunguzi katika mipaka yote, pia wameongeza vifaa mbalimbali vya kusaidia kutambua wagonjwa na watoa huduma za afya ngazi ya jamii waliopo katika vijiji vyote na mitaa katika mkoa mzima nao wameongezewa vifaa ili kama kutakuwa na tatizo wasaidie kulibaini.

"Katika mipaka ya Murongo na Mtukula ambayo ina mwingiliano wa watu wengi, tumeimarisha zaidi suala la uchunguzi na tumeweka sehemu maalum ya idara ya afya kwa ajili ya kuchunguza wasafiri wote na kutoa elimu kwao ya namna ya kujikinga," alisema.

Baadhi ya wananchi waliozungumzia tatizo hilo, waliomba serikali kuendelea kutoa elimu hususani kwa watu wanaishi mipakani ili wasiruhusu wageni kuingia kupitia njia za panya.

"Ebola ni ugonjwa tishio, ni sawa na corona. Kwa hiyo, tusipofanya udhibiti mapema, utaingia na itakuwa shida kubwa kwa wananchi hususani kwa upande wa matibabu, tunaweza kupoteza watu na nguvu kazi ya taifa," alisema mmoja wa wananchi hao.

Baadhi ya dalili za ugonjwa huo ni homa kali, kichefuchefu na kutapika, kuharisha, kuumwa kichwa, maumivu ya misuli, mwili kuchoka, kukosa hamu ya kula na kutokwa na damu sehemu za wazi kama mdomo na pua.




Baadhi ya wasichana walioshiriki mafunzo ya TEHAMA (Code like a Girl) yaliyoandaliwa na Taasisi ya Dlab na kufadhiliwa na Kampuni ya Vodacom Tanzania Plc, wakitoa mada kuhusu vitu walivyojifunza ambapo waliweza kubuni tovuti, kampuni hiyo inadhamani mafunzo hayo yaliyomalizika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## NEST yataka mikakati kuokoa watoto wachanga

**Na Halfani Chusi**

MKURUGENZI wa Mpango wa Kupunguza Vifo vya Watoto Wachanga Hospitalini (NEST360), Catherine Paulo, amesema serikali inapaswa kuweka miundombinu muhimu ikiwamo vifaa tiba, watumishi wenye uwezo na takwimu sahihi ili kukabili vifo vya watoto hao nchini.

Alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki alipotembelea Hospitali ya Rufani Temeke mkoani Dar es Salaam akiwa ameambatana na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dk. Seif Shekhalaghe, kuangalia namna vifaa tiba walivyotoa kwa ajili ya kusaidia kuokoa maisha ya watoto wachanga vilivyoleta matokeo chanya.

Alisema mbali na kutoa vifaa tiba, pia wanatoa elimu kwa wauguzi na wakunga namna ya kutumia vifaa hivyo pamoja na kuwapa elimu ya namna bora ya kuhudumia watoto wachanga.

"NEST ni mpango unaojumuisha mashirika 16, kati yake 12 yapo Afrika Mashariki yanayoshirikiana na Tanzania kutekeleza mpango huu ni iHI, DIT, MUHAS na rice360 iliyoko Marekani.

"Mpango huu ulianza mwaka 2019 na utaisha 2023 kwa lengo la kupunguza vifo vya watoto wachanga kwa asilimia 50 hadi ifikapo 2025.

"Mpango huu unafanya kazi kwa karibu na Wizara ya Afya na wadau wengine ili kuboresha mfumo mzima wa afya. Unafanya kazi katika vituo saba vya KCMC, Hospitali ya Rufani Mbeya. Kwa Dar es Salaam ni Muhimbili, Mloganzila, Amana, Mwananyamala na Temeke," alisema.

Alibainisha vikwazo kadhaa ambavyo vimekuwa vikikwamisha juhudi hizo na kuwaomba wadau kuunga mkono ili kuwawezesha kuvitatua.

"Ufinyu wa bajeti ya kutosha kununua vifaa, vipuli, uhaba wa watumishi hapa Temeke inahitaji wakunga na manesi, bima kwa watoto wachanga ili waweze kupata matibabu ya vipimo (blood culture) ambapo wazazi wengi hushindwa kulipia, hivyo ni muhimu sana kabla ya tiba kufanyiwa vipimo ili kuepusha athari za ziada," alisema.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Joseph Kimaro, alitaja vikwazo vinavyoikabili hospitali hiyo ikiwamo kuongezeka kwa magonjwa yasiyoambukizwa kwenye jamii.

"Tunakabiliwa na ufinyu wa eneo la kutolea huduma kwa wagonjwa kutokana na uchakavu wa baadhi ya miundombinu ya kutolea huduma hususani wodi ya watoto, magonjwa ya ndani na upasuaji, uhaba wa chumba cha upasuaji wa dharula kwa wajawazito.

"Pia uhaba wa mitambo tiba kama CT Scan, MRI, endoscope machine na uhaba wa vifaa tiba vya kibingwa hususani idara ya meno na huduma za macho kutoka," alibainisha.

Aliishukuru serikali kwa kutoa Sh. bilioni nne za ukarabati wa miundombinu hospitalini huko.

Alisema uanzishwaji wa wodi ya watoto wachanga (njiti) chini ya ufadhili wa NEST, umesaidia kupunguza ukosefu wa sehemu za kulaza watoto pamoja na kupunguza rufani za kuwapeleka Muhimbili.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Seif Shekhalage, aliwapongeza watumishi wa afya na NEST360 kwa jitihada walizozifanya katika kupunguza vifo vya watoto wachanga.

"Hivi vifaa tiba kwa watoto wachanga mlivyopewa na NEST360 mvitunze vizuri ili vidumu, wawekeeni mikakati ili waendelee kuwa wadau katika hospitali hii.

"Niwaombe NEST360 kuangalia uwezekano wa kufika katika hospitali zingine au chagueni zile zenye uhitaji mkubwa mfikisha huduma," alishauri.

## Serikali yaahidi mtaala mpya elimu Januari 2024

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imesema inakamilisha kuandaa mtaala mpya wa elimu ambao utaanza kutumika rasmi kuanzia Januari mwaka 2024.

Kamishna wa Elimu, Dk Lyabwene Mtahabwa, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki kwenye mahafali ya kidato cha nne ya Shule ya St Anne Marie Academy Mbezi Kimara.

"Aprili mwaka jana Rais Samia Suluhu Hassan aliagiza tupitie upya mitaala na mfumo wa elimu ili kumwezesha mwanafunzi anayehitimu aweze kujitegemea badala ya kusubiri ajira na tangu agizo hilo litolewe tunaendelea na mwaka 2024 itaanza kutumika," alisema.

Dk. Mtahabwa alisema mfumo wa elimu lazima umwandae mwanafunzi kukabiliana na mazingira yanayomzunguka kwa kufanya kazi za kumwingizia kipato badala ya kukaa na kulalamikia ukosefu wa ajira.

Kamishna aliziponge za shule ambazo hazina kawaida ya kuchuja wanafunzi unapofikia muda wa mitihani ya kitaifa ikiwamo St Anne Marie Academy.

Alikemea tabia ya ubaguzi unaofanywa na baadhi ya shule kwa lengo la kuongeza ufaulu kwenye mitihani ya kitaifa, jambo ambalo alisema ni ubaguzi mkubwa.

"Mheshimiwa Rweikiza Mungu akubariki maana hapa hakuna tabia ya kubagua wanafunzi wakati wa mitihani ya kitaifa. Kumbagua mwanafunzi kwa uwezo wake ni kwenda kinyume na haki za watoto," alisema.

Alisema hatua ya kubagua wanafunzi wakati wa mitihani ya kitaifa ni ukatili mkubwa na fedheha kwa wazazi ambao wamejinyima na kutumia fedha nyingi kuhakikisha mtoto wao anapata elimu bora.

"Badala ya kuwatenga wanafunzi wakati wa mitihani walimu wanapaswa kuwa na mbinu mbalimbali kuhakikisha wanafunzi wote wanakuwa mahiri kwenye masomo.

"Watu wanatofautiana uelewa, wengine wanaelewa haraka na wengine taratibu. Kwa hiyo mbinu zinahitajika kuwawezesha wote kufaulu," alisema.

Aliwapongeza walimu wa shule hiyo kwa ubunifu mkubwa walioonyesha wa kutengeneza bidhaa mbalimbali kama sabuni hali ambayo itawawezesha kuwa wajasiriamali baada ya masomo yao.

"Nimefurahishwa sana na ubunifu wa watoto hapa na wengine wa darasa la tano wamemudu kutengeneza sabuni ambayo kwa kweli nimeifurahia nitaipeleka nyumbani kumwonyesha mke wangu aone kazi za wanafunzi," alipongeza.

Aliwataka wazazi wawafundishe watoto wao ujasiriamali kama njia ya kujitafutia kipato siku zijazo huku akiwataka wenye shule kufundisha lugha mbalimbali ikiwamo Kichina, Kiarabu na Kifaransa kwani yana soko kubwa.

"Dunia inakwenda kwa kasi sana nimeona wanafunzi wanazungumza hata Kifaransa, ninaomba shule zingine ziige kwa kuweka lugha mbalimbali kwa sababu dunia ya sasa ya utandawazi ukiwa na lugha nyingi umejifungulia milango ya mafanikio ukijifungia kwa Kingereza na Kiswahili pekee umejiandalia anguko.

"Mheshimiwa Rweikiza panua wigo wa lugha mbali na Kiswahili, Kiingereza na Kifaransa, weka lugha zingine Kichina na Kiarabu ili uweze kupambana kwenye kanda na kwenye jumuiya ya kimataifa, dunia inakwenda kwa kasi sana," alishauri.



## RC awatupia zigo NEMC urasimu utoaji wa vibali

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Makongoro Nyerere, amelitupia lawama Baraza la Uhifadhi wa Mazingira la Taifa (NEMC) Kanda ya Kaskazini kwa kuendekeza urasimu wa utoaji wa vibali kwa wawekezaji ambao wameonyesha nia ya kuwekeza mkoani humo.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake juu ya maonyesho ya Tanzanite Manyara Trade Fair ambayo yanatarajiwa kufanyika kuanzia Oktoba 19 hadi 23 mwaka huu.

Makongoro alikiri kuwapo kwa urasimu unaofanywa na NEMC kanda ya kaskazini na kuukwamisha mkoa kupata wawekezaji wa viwanda.

"NEMC Kanda ya Kaskazini hawa ni shida, sijui wana kazi nyingi. Kama wangekuwa wanachelewa sana basi ziwe hata wiki mbili. Ila hawa wanachelewa mpaka miaka miwili mtu hajapata kubali," alisema Makongoro.

Alisema majibu yanayotolewa na baraza hilo yanasikitisha na wakisikia kuna wawekezaji ambao wamewafanyia urasimu, wakienda kushtaki makao makuu wanawachukia.

Katibu wa Chama cha Wafanyabiashara wenye Viwanda na Kilimo (TCCIA) Mkoa wa Manyara, Mwanahamisi Hussein alisema kwa sasa kuna kituo cha biashara katika jengo la Halmashauri ya Mji wa Babati, hivyo wawekezaji ambao wanafanyiwa urasimu wanakutana nao na kuwasaidia.

Akizungumza kwa njia ya simu na Nipashe, Meneja wa (NEMC) Kanda ya Kaskazini, Lewis Nzali, alisema hakuna kibali kinachoweza kupatikana ndani ya wiki mbili.

Alisema kwa nchi kama ya Norway kibali kukipata inachukua miaka sita, lakini kwa hapa nchini kitu kinachokwamisha ni hatua tofauti ambazo zinapitiwa ili mwekezaji aweze kupatiwa kibali ikiwamo kuanza kufuatilia eneo analoenda kuwekeza, kuzungumza na wananchi waliomzunguka kujua kama kuna athari za kimazingira.

Alifafanunua kuwa kuna wawekezaji wengine ambao wanapatiwa vibali ndani ya mwezi mmoja au miwili japokuwa wanakwenda sambamba na kasi ya ufuatiliaji wa mwekezaji.

# Wanufaika TASAF watakiwa kuzingatia masharti ruzuku

**Na Allan Isack,** ARUMERU

MRATIBU wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) katika Halmashauri ya Arusha amewataka walengwa wa mpango wa kunusuru kaya maskini awamu ya nne kutimiza masharti ya ruzuku ya fedha walizopokea ili kuwa na sifa za kuendelea kuwa kwenye mpango huo.

Grace Makema alitoa agizo hilo jana wakati wa utoaji ruzuku ya fedha kwa Julai na Agosti mwaka huu.

Alisema fedha hizo zimetolewa kwa walengwa zikiwa na masharti ya kutimiza, ili waendelee kuwa na sifa za kupokea ruzuku hiyo.

Pia aliwataka walengwa hao kuzingatia masharti hayo, yakiwamo ya afya kwa kaya zenye watoto wa kuanzia umri wa mwaka sifuri hadi mitano, kuhakikisha watoto hao wanahudhuria kliniki kwa kipindi chote, pamoja na kupata chanjo zote stahiki.

Alisema kaya hizo, zinatakiwa kuzingatia masharti ya elimu, kwa kaya zenye watoto wa miaka sita hadi 18, wahakikishe wanakwenda shule na kuhudhuria masomo kwa siku zote bila kukosa na kuwapatia mahitaji muhimu ya shule.

"TASAF imeandaa utaratibu wa kufanya warsha za jamii, ili kutoa mafunzo kwa walegwa kila wakati wa kugawa ruzuku, hivyo tunasisitiza kila mlengwa anatakiwa kuhudhuria kwenye hafla hizo za kijamii, ili kupata ufahamu zaidi wa huduma zinazotolewa na mpango, haki, wajibu na umuhimu wa kutimiza masharti ya ruzuku,"alisema Grace.

Walengwa wa Kijiji cha Laroi, waliipongeza kwa kuziwezesha kiuchumi, huku wakiendelea kupewa elimu ya matumizi ya fedha na kutambua haki na wajibu wao kama wanufaika wa mpango huo.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Laroi, Remingi Joseph, alisema uwapo wa programu mbalimbali za mafunzo kwa walengwa unawasaidia wahusika na jamii kupata uelewa wa miradi ya TASAF na ruzuku za fedha wanazopokea walengwa.

"Miradi hii licha ya kuwainua kiuchumi walengwa, pia umefanya wananchi kuchangamsha akili na kubadilika kifikra kwa kuwa wanajumuika na wenzao kwenye vikundi na miradi sambamba na kupata mafunzo yanayowawezesha kubadilika na kukua kifikra," alisema Remigi.



Waziri wa Madini, Dotto Biteko ambaye amemwakilisha Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, kwenye jubilee ya miaka 75 akimpa mkono Askofu Mkuu wa Kanisa la Elim Pentecostal Tanzania, Peter Konki, jana baada ya kuweka jiwe la msingi la kanisa hilo ambalo linatarajiwa kutumia Sh. milioni 800 hadi ujenzi wake kukamilika. **PICHA: JALIWASON JASSON**

# Shirika latoa msaada taulo za kike shuleni

**Na Allan Isack,** ARUMERU

SHIRIKA lisilio la kiserikali la WaterAid Tanzania limetoa msaada wa taulo za kike 660 kwa wasichana wanaosoma kwenye shule za sekondari za pembezoni katika Halmashauri ya Arusha wilayani Arumeru.

Lengo la shirika hilo ni kuwasaidia wasichana kuwa na uhakika wa hedhi salama isiyokuwa na vipingamizi na kuwapa uhakika wa kuhudhuria masomo kipindi chote cha masomo hata wakiwa kwenye hedhi. Mwenyekiti wa Halmashauri ya Arusha, Ojung'u Salekwa, akizungumza wakati wa ugawaji wa taulo hizo, alilishukuru shirika hilo, kwa msaada akisema ni muhimu kwa watoto wa kike.

Alisema kutoa elimu kwa mtoto wa kike ni kuielimisha jamii, hivyo kuwaondolea matatizo watoto wa kike ni kuiondolea jamii matatizo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Arusha, Seleman Msumi, aliwashukuru WaterAid, kwa kutambua thamani ya watoto hao kwa kuwawezesha kujiamini wakati wa hedhi.


"Tunafahamu tatizo ni kubwa kwa watoto wa kike, hasa maeneo ya vijijini, wengi hukosa vifaa vya kujihifadhi na kulazimika kutokuhudhuria masomo, kwa msaada huu, utasaidia kupunguza tatizo hilo, katika halmashauri yetu," Msumi.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkuu katika halmashauri hiyo, Angela Mvaa, alisema ugawaji wa taulo hizo, utakwenda sambamba na utoaji wa elimu ya kujitambua kwa wasichana ili kukabiliana na matatizo ya kijamii, ikiwamo makuzi na mabadiliko ya mwili na athari za mahusiano ya kimapenzi katika umri mdogo.

"Tumeshuhudia vijana wanauana na wengine kujiua kwa ajili ya mahusiano, hivyo tumeamua kuanza kuwapa elimu ya mahusiano na athari zake na namna ya kuishi katika mahusiano kwa kukabiliana na matatizo yake bila kuathiri uhai wa mwingine," alisema Angela.

Ofisa Elimu Kata ya Bwawani, Edward Mbesere, alithibitisha kuwapo tatizo la wasichana kukosa taulo za kujisitiri wakati wa hedhi na kusababisha kushindwa kuhudhuria masomo kila mwezi, kutokana na uwezo mdogo wa kipato kwa familia na kulifanya tukio hilo ni la siri miongoni mwa wanajamii.

Awali shirika hilo lilitoa taulo za kike 660 kwa shule za sekondari za Olokii, Musa, Sambasha, Oljoro, Losinoni, Losikito, Mukulat na Einotj.





# Mjane aiomba serikali kuingilia mgogoro ardhi

**Na Mary Mosha,** HAI

MKAZI wa Kijiji cha Shirimatunda wilayani Hai mkoani Kilimanjaro ambaye ni mjane, Elizaberth Chuwa ameiomba serikali kumsaidia baada ya watoto wa shemeji yake kumfukuza nyumbani kwake alikokaa tangu mwaka 1948

Vijana hao ambao kwa sasa wanaishi Dar es Saalam wamedaiwa kumnyanyasa mjane huyo tangu mumewe na mama mkwe kufariki dunia miaka 20 iliyopita.

Akizungumzana Nipashe, alisema vijana hao wakiongozwa na Erick Chuwa tayari wamechukuwa maeneo mawili aliyoachiwa na muwewe likiwamo eneo lililoko Longuo na Kikavu.

Alisema vijana hao kwa sasa wamemvamia tena eneo analoishi ili aondoke.

"Vijana hawa wamekuja kuvamia eneo hili kwa madai ya kuwa walipewa na bibi yao (Theresia Chuwa) kabla hajafa, jambo ambalo siyo kweli, ninaiomba serikali pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali kunisaidia kuona namna ya kupata haki yangu, nimeteseka kwa zaidi ya miaka 20 sasa.

"Nimefika mahali nikamwomba Mungu anigeuze ndege niweze kuruka na kumwona Rais Samia Suluhu ili aweze kunisaidia, nimeteseka, nateseka na nizidi kuteswa, sijui furaha yangu itatoka wapi na lini, naonewa napigwa vita kali,"alisema.

Mwenyetiki wa Kitongoji hicho, Baltazari Massawe alisema anasikitishwa na kitendo hicho kutokana na kufahamu historia ya eneo hilo tangu mwaka 1968.

"Hili eneo ni la mama mkwe wake na Elizabeth, alijaliwa watoto watatu, Mathey, Zakaria na Fransis, kabla hajafa aligawa kila mtoto na eneo lake lakini cha kushangaza tunaona hawa watoto wa Mathey wanakuja kumfukuza mama yao mdogo nyumbani. Hili halikubaliki, tunaomba serikali iingilie kati ili mama huyu pamoja na watoto wake waweze kupata haki yao," alisema.

Baadhi ya majirani na mjane huyo, akiwamo Rogath Msele aliomba serikali kuchukua hatua za haraka ikiwa pamoja na kufuatilia na kuzungumza na wazee wa kijiji ili kutambua ukweli wa eneo hilo.

Mwenyekiti Mstaafu wa kijiji hicho, Protas Mushi, alisema yeye ni jirani na mjane huyo kwa upande wa kusini wa shamba hilo na anachofahamu eneo hilo ni haki ya Elizabeth na kuiomba serikali kuingilia kati ili kuwasaidia wajane.

Mtoto wa mjane huyo, Edward Chuwa alisema manyanyaso hayo yalianza muda mrefu na kuomba serikali kuwasaidia ili kupata haki.

## UWT Siha yajizatiti kumaliza matukio ya ukatili wa kijinsia

**Na Anjela Mhando,** SIHA

MWENYEKITI wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Wilaya ya Siha, Mkoa wa Kilimanjaro, Bertha Mlay, amesema atahakikisha suala la ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake wilayani humo linakomeshwa kwa kuwafichua watakaofanya vitendo hivyo.

Aliyasema hayo jana baada ya kutangazwa kuwa mshindi katika uchaguzi wa viongozi wa UWT.

Alisema wanawake ndiyo walezi wa familia kuna kila sababu ya kujikita katika kuwalinda, kwamba atahakikisha anakuwa mstari wa mbele kwa kushirikiana na uongozi wa wilaya kutokomeza vitendo hivyo.

"Ni kweli nimeshinda nimeitetea nafasi yangu naombe ushirikiano kama mlivyonipa awali tuweze kusonga mbele katika kuleta maendeleo ya wilaya yetu," alisema Mlay.

Msimamizi wa Uchaguzi huo, ambaye ni Katibu wa CCM Wilaya ya Hai, Ally Ballo, aliwataka wanawake kuendelea kusimamia ilani ya chama hicho pamoja na kuhakikisha wanasimamia malezi ya watoto ili kukuza maadili nchini.

Pia aliwasisitiza wanawake kuendelea kusimamia misingi ya chama tawala pamoja na kuhakikisha chama kinazidi kuwa imara zaidi.

Mwenyekiti wa UVCCM wilayani hapo, Emanuel Abas, aliwaomba vijana kuwapa ushirikiano ili kuhakikisha wanazifikia fursa zinazowazunguka, kuondokana na matatizo ya ukosefu wa ajira ikiwamo ufugaji na kilimo ili waweze kujiajiri wenyewe badala ya kusubiri ajira za serikali.



Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, Stanslous Nyongo, akiomba ufafanuzi wa jambo katika ofisi moja ya kituo cha forodha cha Namanga baada ya kamati hiyo kukitembelea jana, (wa tatu kushoto) ni Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Adam Fimbo, (wa tatu kulia) ni Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel. Kamati hiyo ilikuwa kwenye ziara mkoani Arusha. **PICHA: ASRAJI MVUNGI**

# UVCCM Moshi yapata uongozi mpya

**Na Mary Mosha,** MOSHI

UMOJA wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Manispaa ya Moshi umemchagua Sadath Ndibalema kuwa mwenyekiti wa jumuiya hiyo.

Akitangaza matokeo ya uchaguzi huo, Msimamizi wa Uchaguzi ambaye ni Katibu wa CCM Wilaya ya Moshi Mjini, Ibrahimu Mjanakheri, alisema kuwa nafasi hiyo ilikuwa ikishindaniwa na wanachama watatu ambao ni Anne Makata, Said Kifalali na Sadath Ndibalema.

Alisema kura zilizopigwa zilikuwa ni 222, zilizoharibika ni mbili, kwamba Anne alipata kura 10 na Said alipata kura 64 huku Sadath akipata kura 146 na kuibuka mshindi.

Akizungumza baada ya kutangazwa kwa matokeo hayo, Sadath aliahidi kushirikiana na wanachama wa umoja huo kuhakikisha chama kinasonga mbele.

Sadath alisema kwa kushirikiana na wanachama wa CCM atahakikisha kazi zote nzuri zilizofanywa na watangulizi wake anaziendeleza ili kuhakikisha kuwa jumuiya hiyo inasonga mbele.

Aidha, aliwaahidi vijana wa Manispaa ya Moshi kuhakikisha anawasemea matatizo yao pamoja na kuhakikisha wanaunda vikundi vya ujasiriamali na kunufaika na mikopo ya halmashauri ambayo ni asilimia nne ya mapato ya ndani.

Akifungua mkutano hauo kabla ya kujiuzulu aliyekuwa Mwenyekiti wa jumuiya hiyo, Issa Bulilo aliwataka viongozi waliochaguliwa kuongoza chama kuanzia ngazi ya matawi, shina na kata kutambua kuwa jukumu lao kubwa ni kwenda kutafuta ushindi katika uchaguzi wa serikali za mitaa na ule uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Bulilo alisema wanachama wa CCM wanawaangalia viongozi waliowachagua kuwaongoza na kuwataka kutochukulia uongozi walioupata kama jambo la kawaida kwani hati ya chama ipo katika mabega yao.

Aidha, alitumia pia nafasi hiyo kuwaasa vijana kutumia elimu waliyoipata katika kuisaidia serikali ikiwamo kutafsiri kazi kubwa zinazofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan na kuacha tabia ya kulalamika.

Katibu wa UVCCM Wilaya ya Moshi Mjini, Arafat Mbiruka, alisema jumuiya hiyo itaendelea kuwatetea vijana katika kuhakikisha wanapata haki zao ikiwamo mikopo ya halmashauri.

Mbiruka alisema kuwa, UVCCM katika Manispaa ya Moshi imeendelea kujipanga kuhakikisha CCM inaendelea kutawala Moshi Mjini pamoja na kata zake.

Alisema: "Vijana ndiyo nguvu kazi ya chama na sisi kama vijana tutaendelea kumsemea vizuri Mwenyekiti wetu wa CCM Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan hasa kazi nzuri na kubwa ambazo amekuwa akizifanya na hatutamvumilia yeyote atakayekuwa na nia ya kumkwamisha katika utendaji wa kazi zake."

Nipashe
# Spotika



SAJILI 5 ZA FEDHA NYINGI ZILIZOFELI UK. 16



# 'MANDONGA MTU KAZI'...

Bondia Karim Said 'Mandonga' (kulia) akizipiga na Salim Abeid wa Tanga katika pambano lililofanyika Uwanja wa Nangwanda Sijaona mkoani Mtwara juzi. **HABARI UK. 15.** **PICHA: SAADA AKIDA**

## ISIKUPITE

KATIKA Ligi tano-bora Ulaya, England, Hispania, Italia, Ujerumani na Ufaransa, hadi sasa msimu huu, nyota wa PSG, Neymar ndiye mchezaji aliyetengeneza nafasi nyingi za mabao akifanya hivyo mara 25, akifuatiwa na Kevin de Bruyne wa Man City (22), Mohamed Salah wa Liverpool (24), Lionel Messi wa PSG (24) na Benjamin Bourigeaud (22)wa Stade Rennais.

MAKALA ULAYA

# MAKOCHA WA5 BORA DUNIANI KWA SASA

Carlo Ancelotti alionekana kukosa ubora wake kule Everton. Uamuzi wa kumrejesha katika Klabu ya Real Madrid msimu wa majira ya joto wa 2021, ulionekana kuwa mzuri sana. Lakini kocha huyo wa Italia amefanya kazi kubwa sana pale Santiago Bernabeu...

Klopp atahitaji kupata wachezaji wapya wenye ubora katika dirisha la Januari, ingawa kikosi alichonacho kwa sasa hakijapungua sana.



**Jurgen Klopp (Liverpool)**

**MADRID, Hispania**

MAKOCHA wa soka katika ngazi ya juu wanaishi maisha ya hofu. Nywele zao hugeuka kijivu haraka na mikunjo na mistari ya wasiwasi huanza kuonekana kwenye nyuso zao. Matokeo uwanjani mara moja tu yanaweza kubadilisha mustakabali mzima wa kocha.

Ndiyo maana makocha wa ngazi ya juu wanastahili sifa nyingi kwa kutofuatilia sana maoni hasi. Sio makocha wote wanapewa rasilimali sawa. Wengine huingia kwenye klabu zenye kikosi chenye wachezaji nyota, huku wengine wakilazimika kupambana na vile ambavyo havina wachezaji wa kiwango cha juu.

Lakini tofauti wanayoifanya kwa timu yoyote ipo kwa wote. Bila kuchelewa, hebu tuwaangalie makocha watano bora zaidi katika soka la sasa dunia...

**#5. Diego Simeone (Atletico Madrid)**

Atletico Madrid ilishinda taji la Ligi Kuu Hispania, LaLiga, msimu wa 2020-21. Hawajawa katika kiwango bora kabisa tangu wakati huo, lakini Diego Simeone amefanya maajabu hapo awali na inaonekana kama bado anaweza. Simeone ameweza kuwafanya 'Rojiblancos' hao kucheza dhidi ya wachezaji bora nchini Hispania na Ulaya kwa takriban muongo mmoja sasa.

Ukweli ni kwamba anafanya bila kuwa na rasilimali zinazopatikana kwa washindani wake wengi na anastahili sifa kwa hilo. Ingawa wana wachezaji wachache wenye ubora wa juu, baadhi yao wapo katika siku zao za mwisho za uchezaji.

Simeone anahitaji kuthibitisha msimu huu kwamba mawazo na mbinu zake bado zinaweza kuwapeleka kwenye utukufu. Atletico Madrid mara kwa mara imedumisha hadhi yao kama wapinzani wa taji la nchini Hispania kwa miaka mingi, Simeone anastahili nafasi kwenye orodha hii.

**#4. Antonio Conte (Tottenham Hotspur)**

Ukweli kwamba Tottenham Hotspur wana changamoto katika nyanja zote msimu huu baada ya kuwa katika hali mbaya chini ya mwaka mmoja uliopita, unazungumza mengi kuhusu uwezo wa usimamizi wa Antonio Conte. Kocha huyo wa Kiitaliano amefanya kazi nzuri na Spurs na usajili wao wa majira ya joto na rasilimali chache zinazopatikana ni wa kupongezwa.

Wana kikosi kizuri ambacho kinaweza kuwasaidia kuendana na ukali wa kuwa timu ya daraja la juu Ulaya. Wiki saba baada ya msimu wa 2022-23 wa Ligi Kuu England, Spurs wako nafasi ya tatu kwenye jedwali na wako pointi moja nyuma ya vinara Arsenal.

Conte amethibitisha uwezo wake siku za nyuma akiwa Juventus, Chelsea na Inter Milan. Anaweza kufanya hivyo hivyo akiwa Spurs.



Pep Guardiola (Manchester City)

**#3. Jurgen Klopp (Liverpool)**

Liverpool wamevumilia mwanzo mbaya wa msimu wa 2022-23. Lakini kwa kiasi kikubwa inatokana na mlolongo wa majeruhi katika klabu. Huenda wasiweze kushinda taji la Ligi Kuu England msimu huu baada ya kuanza polepole. Lakini hiyo haimaanishi kuwa hawatasimama tena hivi karibuni.

Klopp ameshinda matatizo mengi katika maisha yake ya ukocha. Inatosha kusema, Liverpool wako mbali sana kuanza kuwafikiria vibaya kwa sasa.

Klopp atahitaji kupata wachezaji wapya wenye ubora katika dirisha la Januari, ingawa kikosi alichonacho kwa sasa hakijapungua sana.

**#2. Pep Guardiola (Manchester City)**

Akiwa amebarikiwa na rasilimali zisizo na kikomo na maarifa ya kimbinu ya kuwazidi akili watu wa enzi zake, inasikitisha sana kwamba, Pep Guardiola hajashinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Manchester City.

Ana wachezaji wa kiwango cha kimataifa katika takriban kila nafasi na City hawajawahi kushindwa kufikia malengo yao ya juu ya uhamisho katika siku za hivi karibuni.

Kuongezwa kwa Erling Haaland kumeifanya City kuonekana zaidi ya timu kamili. Wanapigiwa upatu kushinda taji la Ligi Kuu kwa mara ya tatu mfululizo msimu huu. Lakini zaidi ya hayo, Guardiola atakuwa na matumaini ya kubeba taji la Ulaya.

Atakuwa na hamu ya kushinda tena taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

**#1. Carlo Ancelotti (Real Madrid)**

Carlo Ancelotti alionekana kukosa ubora wake kule Everton. Uamuzi wa kumrejesha katika Klabu ya Real Madrid msimu wa majira ya joto wa 2021, ulionekana kuwa mzuri sana. Lakini kocha huyo wa Italia amefanya kazi kubwa sana pale Santiago Bernabeu.

Aliwapa umaarufu wa nyumbani na Ulaya katika msimu wa 2021-22 licha ya kuwa na msingi wa wachezaji wazee. Ancelotti sasa ameimarisha hadhi yake kama mmoja wa makocha bora wa soka wa wakati wote. Atatafuta kuiga mafanikio yake kutoka msimu wa 2021-22 kwa msimu huu.

MAKALA BONGO

NGUMI MPAPASO



# MANDONGA MTU KAZI NA 'NDONGA' YA JICHO MTWARA

Bondia Karim Said 'Mandonga' akiwa na manundu usoni baada ya kupelekewa 'ndonga' nzito na Salim Abeid wakati wa pambano lao lililofanyika Uwanja wa Nangwanda Sijaona mkoani Mtwara juzi. **MPIGAPICHA WETU**

**Na Saada Akida, MTWARA**

"MIMI si mtu wa kuogopa, siangalii hela wala nini hata bure ukiniita tu napanda uliongoni hata kesho niite 'Mandonga Mtu' Kazi'," hivyo ni baadhi ya vionjo vya bondia, Karim Said 'Mandonga', ambaye amejizoelea umaarufu mkubwa hapa nchini kwa siku za hivi karibuni.

Mandonga mwenye rekodi ya kucheza mapambano matano kabla ya pambano lake la juzi, Jumamosi dhidi ya Salim Abeid kutoka Tanga lililofanyika mkoani Mtwara katika Uwanja wa Nangwanda Sijaona, ameshinda moja kwa TKO kati ya hayo matatu amepigwa kwa KO huku akitoka sare moja.

Katika pambano ambalo Mandonga alishinda kwa TKO lilikuwa dhidi ya Musa Omary kwa TKO akitumia dakika moja na sekunde 56 katika pambano lililofanyika viwanja vya Leaders, Dar es Salaam kwenye kilele cha tamasha la kihistoria la Sensabika.

Bondia huyo ambaye amekuwa na misemo kila pambano alianza na 'Mandonga Mtu Kazi', 'Mtumbwi wa Vibwengo' baada ya kuchapika kwa Shaban Kaoneka akaibuka na kaulimbiu yake nyingi 'Mwanaume alii na bahari haikauki'.

Mbali na hizo katika pambano la Mtwara juzi dhidi ya Salim Abeid aliingia na kaulimbiu mpya ya 'Ngumi Mchomoko' akidai atampa kipigo mpinzani wake huyo kama vile amemwibia mke.

Kauli na kelele hizo nyingi za Mandongo kabla ya kupanda uliongoni ndizo ambazo zimekuwa kivutio kikubwa hata kwa wadau wa ngumi na hata wale ambao hawashabikii mchezo huo wamejikuta wakimfuatilia kila akipanda uliongoni.

Kwa Mandongo, ushindi si suala la muhimu sana kwa mashabiki wake, kwani hata yeye anatambua akishindwa ndiyo mashabiki huvutiwa na yeye zaidi hasa kutokana na tambo anazozitoa kabla ya kupanda ulingoni.

Katika pambano la juzi Mandonga aliendelea kupata mashabiki wapya ndani ya mkoa wa Mtwara katika pambano alilomsindikiza Twaha Kiduku alipochapana na bondia kutoka Misri, Abdo Khaled.

Hata hivyo, katika pambano hilo la juzi kati ya Mandonga na Salim Abeid hakupatikana mshindi kutokana na Rais wa Kamisheni ya Ngumi za Kulipwa, Chaurembo Palasa, kulifuta kutokana na Mwamuzi Habibu Mkarafuu, ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Waamuzi wa Ngumi za Kulipwa, kutochezesha kwa haki.

Lakini wakati raundi ya pili ikielekea ukiongoni Mandonga alionyesha burudani kwa mashabiki kwa kuonyesha staili ya kucheza ulingoni wakati anatakiwa kwenda kupumzika kwa dakika ili kurudi raundi ya tatu kuendelea kupigana.

Katika makala haya tumezungumza na Mandogo mambo mbalimbali ikiwamo maisha yake ndani na nje ya ngumi kabla ya kuanza kupata umaarufu.

"Niko tayari kurudia hii pambano hata bure, leo (jana) nimecheza staili mpya ambayo nimeitoa nchini Japan," anasema Mandonga.

> "Niko tayari kurudia hii pambano hata bure, leo (jana) nimecheza staili mpya ambayo nimeitoa nchini Japan," anasema Mandonga.

### Malengo yake

"Katika ngumi niko kwa ajili ya kuwapa furaha mashabiki wangu na kutafuta pesa ili kuishi vizuri, kutembelea gari zuri pamoja na watoto wangu wapate elimu bora ya bila manyanyaso," anasema Mandonga.

Anasema hafikirii kabisa kucheza na mabondia kutoka nje kwa sababu anacheza mchezo huo kwa ajili ya kujitangaza ili kupata matangazo na ubalozi wa makampuni mbalimbali na kufika malengo yake.

"Kwa sasa Mungu amefungua wakati wangu, kwa wale nilikuwa nikiwasapoti sasa ni zamu yangu kunisapoti katika harakati zangu za kuhamasisha mchezo wa ngumi na kuzidi kukua."

### Kuhusu mashabiki

"Kweli mashabiki wangu wote wanatumia ukurasa wangu wa mtandao wa kijamii kutuma ujumbe kwamba wanafurahi ninapopigwa, niwahakikishie sitawaangusha, nitafanya wanavyotaka wao," anasema Mandonga ambaye kwa sasa amepewa jukumu la kutangaza mkoa wa Mtwara.

Anasema hatarudi nyuma kwa kuwakwaza mashabiki wake kwani anaamini katika mapambano yake akipigwa yeye ni kama amempiga mpinzani wake, jambo ambalo huwafurahisha mashabiki ambao wako nyuma yake.

"Mashabiki wameniambia hawapendi kuniona nampiga mtu, furaha yao nikipigwa katika hilo nimezingatia," anasema bondia huyo ambaye ameacha kazi yake ya kupiga debe katika Stendi ya Msavu mjini Morogoro.

Anasema kabla ya kujulikana kupitia ngumi alikuwa mpigadebe, licha ya kwamba awali alikuwa akipigana kabla ya Francis Cheka na Twaha Kiduku.

"Nilikuwa nacheza ngumi kabla ya hao mabondia huko Morogoro, lakini sikupata nafasi ya kujulikana kwa sababu ya kuwekewa ukuta," anasema Mandonga Mtu Kazi, ambaye katika pambano la juzi alipelekewa 'ndoga' (ngumi) ya jicho la kulia na kumsababishia uvimbe.

### Pambano hatokuja kusahau

"Baada ya kupigwa kwa KO dhidi ya Shaban Kaoneka,

"Kwenye pambano letu la awali wakati tukisindikikiza pambano la ubingwa kati ya Selema Kidunda na Alex Kantopa mjini Songea, nilipigwa kwa KO na Shaban Kaoneka katika raundi ya nne, nilijisikia burudani sana kwa kupigwa kwa sababu nilianza kutambulisha ngumi katika pambano la kimataifa na kidunia kwa kupigwa."

### Mafanikio

Mandonga anasema pamoja na mafanikio mengine yote kimaisha aliyoyapata ikiwamo kuwa balozi katika mashirika mbalimbali na kumwingizia fedha, lakini kubwa zaidi anautangaza mchezo wa ngumi na amekuwa mtu maarufu.

"Kila unapotaja jina la Mandonga watu hushangilia, hivyo napata mashabiki wengi pamoja na ubalozi katika mikoa mbalimbali ikiwamo Songea na Mtwara kwa sasa."

# SAJILI 5 ZA FEDHA NYINGI ZILIZOFELI



Nunez

**LONDON, England**

DIRISHA la uhamisho wa majira ya joto la msimu wa 2022-23, lilishuhudia ikitumika fedha nyingi kusajili wachezaji. Wakati wachezaji kama Erling Haaland wa Manchester City (euro milioni 60) na Aurelien Tchouameni wa Real Madrid (euro milioni 80) wakiwa wameanza vema katika nyumba zao mpya, baadhi yao bado hawajaweza kufikia matarajio.

Hapa, tutawaangalia wachezaji wachache bora ambao bado hawajafikia matarajio katika klabu zao mpya. Hawa ni wachezaji watano waliosajiliwa kwa fedha nyingi msimu huu wa majira ya joto ambao hawajapata matokeo ambayo mashabiki waliyatarajia kutoka kwao...

**#5. Yves Bissouma - Tottenham Hotspur**

Tottenham Hotspur ilitumia fedha nyingi kwa wachezaji wawili msimu huu wa majira ya joto. Walimsajili Richarlison kutoka Everton kwa ada ya euro milioni 58 na wakampata Yves Bissouma kutoka Brighton & Hove Albion kwa euro milioni 29.2. Wakati fowadi huyo wa Brazil ameanza vizuri moto wake hapo Spurs, Bissouma bado hajaonyesha dalili nzuri.

Bissouma alikuwa na kiwango cha kuvutia macho wakati akiwa Brighton katika msimu wa 2021-22. Alifunga mara mbili na kutoa pasi mbili za mabao katika mechi 28 alizoichezea klabu hiyo kwenye mashindano yote.

Huku wachezaji wawili wa kiungo chaguo la kwanza, Pierre-Emile Hojbjerg na Rodrigo Bentancur wakifanya kazi kwa kiwango cha kufurahisha pale Spurs, imekuwa vigumu kwa usajili wa majira ya joto kupata dakika za kucheza mara kwa mara. Bissouma ameanza katika mechi moja pekee ya Ligi Kuu England msimu huu, akitokea benchi katika mechi nne na kubaki bila kutumika mara moja. Bado hajafunga au kutoa pasi, lakini tayari ameshapata kadi mbili za njano.

**#4. Casemiro - Manchester United**

Kwa kushtua wengi, Manchester United ilimsajili kiungo aliyeshinda mara tano Ligi ya Mabingwa Ulaya, Casemiro kutoka Real Madrid mapema msimu huu wa majira ya joto. Kiungo huyo wa kati mkabaji wa Brazil aliigharimu klabu hiyo kitita cha euro milioni 70.65, na kumfanya kuwa mmoja wa wachezaji ghali zaidi waliosajiliwa katika historia ya klabu hiyo.

Casemiro aliunda ushirikiano wa kutisha wa safu ya kiungo na Luka Modric na Toni Kroos wakiwa Real Madrid, huku watatu hao wakishinda mataji manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya pamoja. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil, alikaa chini ya safu ya kiungo, akinasa pasi za kutisha na mara nyingi kuanzisha mashambulizi.

Mchezaji huyo mpya wa Man United, Casemiro ameripotiwa kuwa atapunguziwa mshahara wake ikiwa klabu hiyo itashindwa kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao. Mashabiki walitarajia angetikisa uwanjani Old Trafford, lakini haijawa hivyo. Hadi sasa ameshiriki katika mechi nne (katika mashindano yote) kwa United, na kushindwa kuwavutia watazamaji kwa uchezaji wake.

Katika mechi tatu za Ligi Kuu England alizoshiriki, Casemiro amezuia mpira mara nne pekee na kupoteza mpira mara saba. Mechi yake ya kwanza ya Ligi ya Europa dhidi ya Real Sociedad (kipigo 1-0) pia haikuwa ya kuridhisha kwake.

**#3. Matthijs de Ligt – Bayern Munich**

Vigogo wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, Bayern Munich walitumia euro milioni 67 kumnunua Matthijs de Ligt kutoka Juventus mapema msimu huu wa majira ya joto. Nyota huyo wa zamani wa Ajax, ambaye anajulikana kwa uongozi wake dimbani, ustadi wa kujilinda, na utimamu wa mwili, bado hajajitambulisha kama mmoja wapo wa majina ya kwanza kwenye karatasi ya timu ya kocha Julian Nagelsmann.

Nagelsmann alimpa mechi yake ya kwanza kamili ya Bundesliga dhidi ya VfL Bochum, De Ligt alifunga bao, akiisaidia timu yake kushinda mabao 7-0. Alianza pia dhidi ya Union Berlin na VfB Stuttgart, lakini kiwango chake hakijawa cha kuvutia moyo. Bayern walipata sare mfululizo dhidi ya Berlin (1-1) na Stuttgart (2-2), huku mlinzi huyo akiibuka kinara wa faulo.

Ilikuwa ni faulo yake ya dakika za majeruhi kwa Sehrou Guirassy, ambayo iliwazawadia Stuttgart penalti. Guirassy kwa kujiamini alifunga mkwaju wa penalti na kusaidia sare ya 2-2 kwenye Uwanja wa Allianz Arena.

De Ligt aliachwa kwenye mechi ya Kundi C ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ya Bayern dhidi ya Barcelona (Septemba 13).

**#2. Kalidou Koulibaly - Chelsea**

Mwanzoni mwa majira ya joto, Chelsea iliwapoteza mabeki wao wawili wa kati, Antonio Rudiger na Andreas Christensen, huku wote wakiondoka klabuni hapo kama wachezaji huru.

Chelsea ilijibu kwa kumsajili Kalidou Koulibaly kutoka klabu ya Italia ya Napoli kwa ada ya euro milioni 38. Beki huyo wa kati wa Senegal, ambaye mara kwa mara alisifiwa kwa uchezaji wake huko Napoli, bado hajacheza soka lake bora pale Stamford Bridge.

Koulibaly anaonekana kuwa na wakati mgumu kuzoea kasi ya Ligi Kuu England. Nyakati zake hazijafikia kiwango na alionekana wa kawaida katika mfumo wa mabeki watatu wa Tuchel, akiruhusu mabao nane katika mechi tano za Ligi Kuu.

Kocha mpya Graham Potter anatazamiwa kuweka mfumo mpya hapo Stamford Bridge, na Koulibaly lazima ahakikishe ni mmoja wa wachezaji anayeweza kutegemewa.

**#1. Darwin Nunez - Liverpool**

Siku chache baada ya Manchester City kuthibitisha usajili wa Erling Haaland, Liverpool walijibu kwa uhamisho wa kipekee, na kumnyakua Darwin Nunez kutoka Benfica. Mshambuliaji huyo wa Uruguay alijiunga na 'Wekundu' hao mapema msimu huu wa majira ya joto kwa ada ya euro milioni 75, akisaini mkataba wa miaka sita.

Mchezaji huyo aliyesajiliwa majira ya joto alifurahia mwanzo wa ndoto ndani ya Liverpool, akifunga bao katika ushindi wa 3-1 wa Ngao ya Jamii dhidi ya Manchester City. Alipata bao katika mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu England pia, akifunga mara moja na kutoa asisti na kuwasaidia 'Wekundu' hao kutoka sare ya 2-2 dhidi ya Fulham.

Alionyeshwa kadi nyekundu ya moja kwa moja kwa kumpiga kichwa Joachim Andersen, na kusimamishwa mechi tatu kwenye ligi. Nunez alirejea uwanjani kwenye mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Everton, Septemba 3, mwaka huu lakini bado hajawa na kiwango cha kuvutia.

Mshambuliaji huyo ametatizika kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya pia, akishindwa kuibuka na mchango wa mabao katika mechi mbili (zote akitokea benchi).

## Nukuu

"Primeiro de Agosto ni timu inayotumia nguvu na wachezaji wake wapo timamu, hatutakuwa na ulazima wa kucheza kama wanavyocheza wao, kazi kubwa iliyopo yetu ni kuhakikisha tunaandaa kikosi ambacho kitacheza kiakili zaidi ili kukwepa kutolewa mchezoni," **Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda kuelekea mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya timu hiyo ya Angola.**



"Cristiano Ronaldo alitikisa utoto wangu. Nilikuwa na mabango yake chumbani kwangu. Ni mchezaji niliyempenda. Alikuwa na kipaji, lakini kwa bidii aliyoiweka, alijigeuza kuwa gwiji," **Nyota wa PSG na Ufaransa, Kylian Mbappe akielezea anavyomkubali Ronaldo.**




"Ni hatua katika msimu ambapo siwezi kuwataka wachezaji wacheze mpira wa kuvutia. Ninawataka wacheze mpira wa akili ili kushinda michezo kwa njia iliyonyooka zaidi," **Kocha wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, mwanzoni mwa msimu huu wakiwa tayari wameshinda mechi saba na hawajapoteza wala kupata sare.**





Djuma Shaaban akiifungia Yanga kwa faulo wakati wakiichapa Mtibwa mabao 3-0 kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara Septemba 13, mwaka huu, iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: MAKTABA**

# MABAO 11 YA FAULO RAUNDI YA 4 LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Ligi Kuu Tanzania Bara imefikia raundi ya nne, jumla ya mabao 69 yamefungwa, na kati ya hayo 11 yamefungwa kwa mipira ya adhabu.

Kwa muda mrefu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara kumekuwa na malalamiko ya wadau wa soka kutokuwa na mabao mengi ya 'mipira' iliyokufa au yanayotokana na mipira hiyo, na hii inasemekana ni kukosekana kwa wachezaji ambao ni mahiri kwa kupiga faulo hizo.

Msimu huu imeonekana huenda kunaweza kuwa na idadi kubwa ya mabao ya mipira ya faulo, au yanayofungwa kutokana na adhabu hizo.

Inawezekana ni kwa sababu kumekuwa na wapigaji wazuri wa mipira hiyo, au waunganishaji, lakini pia inawezekana ikawa kuna uzembe kwa baadhi ya walinzi kwenye timu mbalimbali.

Kwenye makala haya, tumekukusanyia mabao yote 10 yaliyotokana na mipira ya faulo kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa na wafungaji wake, twende sasa...

**#1. Vedastus Mwihambi (Mtibwa vs Namungo)**

Beki Mwihambi alikuwa mchezaji wa kwanza kufunga bao lililotokana na mpira wa faulo kwenye mechi kati ya timu yake ya Mtibwa Sugar dhidi ya Namungo katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam Agosti 15, mwaka huu na kutoka sare ya mabao 2-2.

Faulo ilipigwa na Ismail Mhesa pembeni nje ya eneo la hatari, mfungaji aliruka juu kuliko wote na kuuweka wavuni kwa kichwa dakika ya 54.

**#2. Nickson Kibabage (Mtibwa vs Namungo)**

Kwenye mechi hiyo hiyo ya Namungo dhidi ya Mtibwa Sugar, beki wa kushoto, Nickson Kibabage alifunga bao dakika ya 79, baada ya Mhesa kwa mara nyingine kupiga faulo lililozaa bao la pili kwa Mtibwa.

Safari hii alipiga moja kwa moja, mpira ukatemwa na kipa Jonathan Nahimana, mfungaji akauwahi na kuukwamisha wavuni, mechi iliyoisha kwa sare ya mabao 2-2.

**#3. Augustine Okrah (Simba va Geita Gold)**

Mghana Augustine Okrah alikuwa ni mchezaji wa tatu msimu huu kupachika bao la mkwaju wa faulo. Yeye alifunga moja kwa moja.

Clatous Chama alichezewa madhambi nje kidogo ya eneo la hatari kwenye mechi ya Simba dhidi ya Geita Gold, Uwanja wa Benjamin Mkapa Agosti 17, mwaka huu.

Faulo ilipigwa na Okrah kwa shuti kali la mguu wa kushoto dakika ya 37 lililokwenda moja kwa moja wavuni, likimwacha kipa Sebusebu Samson akijaribu kuudaka bila mafanikio. Simba ilishinda mabao 3-0.

**#4. Adeiyum Selemani (Geita Gold vs Azam)**

Mechi ilichezwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi kati ya wenyeji dhidi ya Geita Gold na timu hizo kwenda sare ya bao 1-1, Agosti 21, mwaka huu.

Bao la Geita Gold lilifungwa kwa mkwaju wa moja kwa moja wa faulo iliyopigwa na Adeiyum Selemani dakika ya 55 na kumuacha kipa Ali Ahamada asijue la kufanya.

**#5. Daniel Amoah (Azam vs Yanga)**

Daniel Amoah aliunganishwa kwa kichwa faulo na mpira kujaa wavuni, akimuacha kipa Djigui Diarra akidaka hewa.

Ilikuwa ni faulo iliyopigwa na Ayoub Lyanga, iliyozaa bao kwa Azam FC dakika ya 24 ya mchezo kati ya timu hiyo dhidi ya Yanga, Septemba 6, mwaka huu timu hizo zikitoka sare ya mabao 2-2 Uwanja wa Benjamin Mkapa.

**#6. Andrew Sinchimba (Mtibwa vs Ihefu)**

Straika wa Ihefu FC alifunga naye dakika ya saba kwenye Uwanja wa Manungu Complex, Turiani, Morogoro bao lililotokana na faulo iliyopigwa na Never Tegere. Shuti lilikuwa kali na kumfanya kipa Farouk Shikalo kulitema, kabla ya mfungaji hajaukwamisha wavuni Septemba 7, mwaka huu Mtibwa Sugar ikishinda mabao 3-1.

**#7. Ismail Mhesa (Mtibwa vs Ihefu)**

Mpaka hapa utaona kuwa Mtibwa Sugar ndiyo wanaongoza kwa kupachika mabao mengi yaliyotokana na 'mipira iliyokufa', kwani hili ni bao la tatu kwao, baada ya yale mawili kwenye mechi dhidi ya Namungo, huku Ismail Mhesa akihusika.

Wakati yale mawili alipiga faulo wenzake wakifunga, hili alifunga mwenyewe moja kwa moja dakika ya 44 kwenye mechi hiyo hiyo iliyochezwa Manungu dhidi ya Ihefu na kushinda mabao 3-1.

**#8. Habib Kyombo (Simba vs KMC)**

Habib Kyombo aliisawazisha Simba ikitoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya KMC, Uwanja wa Benjamin Mkapa, dakika mbili kabla mechi kumalizika, Septemba 7, mwaka huu.

Ilikuwa ni faulo iliyopigwa na Chama, Moses Phiri akapiga kichwa ambacho kilimkuta mfungaji.

**#9. Reliants Lusajo (Namungo vs Ruvu)**

Ni faulo iliyoanzishwa haraka haraka, mpira akapelekewa mfungaji akaujaza wavuni, likiwa ni bao pekee kwenye mechi hiyo, Namungo ikiichapa Ruvu Shooting bao 1-0, Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi.

Wachezaji wa Ruvu walalama kuwa faulo ilipigwa mbele zaidi ya pale madhambi yalipotendeka, lakini haikusaidia.

**#10. Djuma Shaaban (Yanga vs Mtibwa)**

Mwihambi alimfanyia madhambi Farid Mussa, kabla ya Djuma kupiga faulo kwa shuti kali umbali kiasi cha mita 30 hivi, Shikali hakuuona mpira huo uliokwenda wavuni.

Ilikuwa ni Septemba 13, mwaka huu Uwanja wa Benjamin Mkapa, Yanga ikiifunga Mtibwa Sugar mabao 3-0.

**#11. Styve Nzigamasabo (KMC vs Ihefu)**


Nzigamasabo alifanyiwa madhambi yeye mwenyewe, na akapiga faulo iliyokwenda moja kwa moja wavuni, bao lililoipatia ushindi timu yake ya KMC wa mabao 2-1 dhidi ya Ihefu, Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, Septemba 20, mwaka huu.

## NDANI YA 18



KIPA wa Barcelona, Marc-Andre Ter Stegen kwa sasa ndiye mlinda mlango mwenye uwiano wa juu zaidi wa kuokoa katika ligi tano-bora za Ulaya (England, Hispania, Italia, Ujerumani na Ufaransa) akiwa na asilimia 92.9 ya kuokoa anafutiwa na Yann Sommer wa Borussia Mönchengladbach (90.9%), Neto wa Bournemouth (90.9%), Gero Rulli wa Villarreal (89.5%) na Gianluigi Donnarumma wa PSG mwenye asilimia 85.7.

# FUNDI WA WIKI...



## AUGUSTINE OKRAH

| | |
|---|---|
| KUZALIWA | Septemba 14, 1993 (miaka 29) |
| URAIA | Ghana |
| KIMO | 1.72 m (5 ft 8 in) |
| NAFASI | Kiungo mshambuliaji/ Winga |
| KLABU | Simba |
| JEZI | Na. 27 |



Haaland

# MASHOTO WA TANO BORA ZAIDI DUNIANI KWA SASA

**LONDON, England**

WACHEZAJI wanaotumia mguu wa kushoto ni wachache katika ulimwengu wa soka. Lakini licha ya hilo, baadhi ya wanasoka wakubwa wa wakati wote wana mguu wa kushoto dimbani. Ukweli ni kwamba wao wanawapa nafasi ngumu sana mabeki wanaokabiliana nao.

Wachezaji wanaotumia mguu wa kushoto huongeza ari zaidi kwa timu na wanaweza kuthibitisha kuwa wapinzani wagumu sana. Wachezaji kama Diego Maradona na Lionel Messi, wanaochukuliwa kuwa (bora wa wakati wote) katika soka, wote ni mashoto.

Hata leo, kuna wachezaji wengi wa kiwango cha kimataifa wanaotumia mguu wa kushoto ambao hutufurahisha kwa ustadi wao kwa mchezo bora. Hapa tuwaangalie wachezaji watano bora zaidi kwa sasa duniani wanaotumia mguu wa kushoto.

**#5. Mohamed Salah (Liverpool)**

Mohamed Salah alikuwa mmoja wa wachezaji walio katika kiwango bora zaidi ulimwenguni katika nusu ya kwanza ya msimu wa 2021-22. Alionekana kutozuilika huku akiwatia hofu mabeki kwa kasi yake, udhibiti wa karibu, kufanya maamuzi na uwezo wa kupiga mashuti ndani ya tatu ya mwisho.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Misri, alifunga mabao ya kujifurahisha na alionekana kuiinua Liverpool. Hata hivyo, kiwango cha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, kimeshuka tangu mwanzo wa mwaka huu.

Salah hakuwa katika kiwango bora mwaka huu na kutokuwa na uwezo wa kuathiri michezo kama ilivyokuwa awali kumechangia kwa Liverpool kuanza polepole msimu wa 2022-23. Bado ni mwanasoka mzuri sana na mmoja wa wachezaji bora wanaotumia mguu wa kushoto ambao tumewaona hivi karibuni.

Katika mechi tisa kwenye michuano yote hadi sasa msimu huu, Salah amefunga mabao manne na kutoa asisti tatu.

**#4. David Alaba (Real Madrid)**

Baada ya kukaa kwa misimu 11 na Bayern Munich, David Alaba alihama klabu hiyo na kwenda Real Madrid msimu wa majira ya joto wa 2021. Alifurahia msimu mzuri wa kwanza katika mji huo mkuu wa Hispania, akishinda mataji ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga, na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Alaba yuko imara pale kwenye dimba la Santiago Bernabeu na anaendelea kuwa mmoja wa mabeki wao wa kati chaguo la kwanza. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Austria ni mwanasoka hodari ambaye anaweza kucheza katika nafasi nyingi kama beki wa kati, beki wa kushoto, winga ya kushoto na kiungo wa kati pia.



**Lionel Messi (Paris Saint-Germain)** Baada ya kuondoka katika klabu yake ya utotoni ya Barcelona majira ya joto ya 2021, Lionel Messi alivumilia mwanzo mbaya wa maisha katika klabu yake mpya ya Paris Saint-Germain...

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, amefanya kazi nzuri kama beki kwa timu hiyo ya kocha, Carlo Ancelotti hadi sasa msimu huu.

**#3. Bernardo Silva (Manchester City)**

Kiungo wa kati wa Manchester City, Bernardo Silva alionekana kama ameanza kuchoka katika msimu wa 2021-22. Ingawa amekuwa akizingatiwa kuwa mchezaji bora, hakuainishwa kama mwanasoka wa kiwango cha kimataifa hadi msimu uliopita.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno, amekuwa katika kiwango kizuri kwa miaka michache. Silva ni mzuri wa kugawa mipira na anaweza kukimbia na safu ya ulinzi licha ya ukosefu wa kasi. Ni mpiga pasi nadhifu na anapenda kuchelewa kufika kwenye eneo la hatari na kufunga mabao muhimu kwa upande wake.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, alihusishwa kwa kiasi kikubwa kuhamia Barcelona msimu huu wa majira ya joto. Lakini aliishia kukaa City na ameanza vema msimu mpya. Silva amefunga mabao mawili na kutoa pasi tatu za mabao katika mechi 10 alizocheza kwenye mashindano yote kwa City hadi sasa.

**#2. Lionel Messi (Paris Saint-Germain)**

Baada ya kuondoka katika klabu yake ya utotoni ya Barcelona majira ya joto ya 2021, Lionel Messi alivumilia mwanzo mbaya wa maisha katika klabu yake mpya ya Paris Saint-Germain. Mshindi huyo mara saba wa Ballon d'Or hakuwa karibu na ubora wake, lakini bado aliweza kuchangia kwa kiasi kikubwa kuelekea kunyakua taji la Ligue 1 la PSG msimu uliopita.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35, anaonekana sasa ametulia katika mji mkuu wa Ufaransa huku akirejea kucheza kama mshindi wa dunia kwa mara nyingine tena. Messi amekuwa katika kiwango cha hali ya juu akiwa na PSG chini ya kocha mpya, Christophe Galtier.

Messi amefunga mabao sita na kutoa pasi nane za mabao katika mechi 11 alizocheza kwenye michuano yote akiwa na PSG hadi sasa msimu huu.

**#1. Erling Haaland (Manchester City)**

Erling Haaland alijiimarisha kama mmoja wa washambuliaji bora zaidi duniani katika kipindi cha miaka miwili na nusu akiwa Borussia Dortmund. Aliondoka kwenye kikosi hicho cha Bundesliga msimu uliopita wa majira ya joto na kupata uhamisho wa euro milioni 60 kutua Manchester City.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway, ameanza kwenye Ligi ya England kwa dhoruba kali msimu huu na amekuwa na mwanzo mzuri wa maisha katika klabu yake mpya.

Katika mechi 10 kwenye michuano yote, aliyoichezea Manchester City kufikia sasa msimu huu, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, amefunga mabao 14 na kutoa asisti moja. Kwa kiwango cha sasa, ndiye mchezaji bora zaidi wa mguu wa kushoto duniani hivi sasa.

## JE, WAJUA?

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti na aliyekuwa akiinoa Manchester United, Sir Alex Ferguson, ni makocha wawili pekee ambao wameweza kushinda jumla ya mechi 100 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hadi sasa.





# Wamiliki hoteli watakiwa kuboresha huduma zao

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya amewataka wawekezaji wa hoteli katika Jiji la Mbeya kuboresha huduma kwenye maeneo yao ili kuwavutia wageni katika biashara zao.

Juma Homera alitoa agizo hilo juzi jijini Mbeya alipozindua Hoteli ya ECHA Luxury Villa, akibainisha kuwa wageni wengi huwa wanakimbia kwenye hoteli kutokana na huduma mbovu ambazo wamekuwa wakipata.

Alisema wamiliki wa hoteli wanatakiwa kuyaweka mazingira ya hoteli zao kuwa safi na kuwaweka watoa huduma wenye weledi wa kazi wakiwamo wasimamizi, wahasibu na wafanyakazi wengine.

Homera alisema serikali inajiandaa kuanza kujenga miundombinu ya kisasa kwa ajili ya maonyesho ya hudumu ya wakulima baada ya serikali kuridhia maonyesho hayo kuanza kufanyika kimataifa katika mkoa huo.

Alisema mkoa huo utakuwa unapokea wageni wengi ambao watahitaji maeneo ya kulala na kupata huduma zingine na hivyo akasisitiza huduma za hoteli kuendelea kuboreshwa.

Homera aliwataka wawekezaji kutoka katika maeneo mbalimbali nchini kujitokeza kuwekeza kwenye biashara ya hoteli mkoani humo ili kuongeza ushindani na kuboresha huduma.

"Ukikuta hoteli imekufa basi tatizo la kwanza huwa ni meneja, wahasibu na wahudumu kwahiyo ni lazima wawekezaji muwe makini mnapoajiri watu hawa, boresheni huduma zenu ili msikimbiwe na wateja," alisema Homera.

Alimpongeza Mkurugenzi wa Hoteli hiyo, Edda Mosha kwa uwekezaji alioufanya ndani ya mkoa huo, akisisitiza ni wanawake wachache huwa wana uthubutu kufanya uwekezaji wa aina hiyo.

Mkurugenzi wa Hoteli hiyo, Edda aliishukuru serikali kwa kuwawekea wawekezaji wazawa mazingira mazuri ya kufanya biashara, akieleza kuwa amekuwa akiwekeza kwenye biashara mbalimbali.

Alisema serikali isingekuwa inaruhusu wawekezaji binafsi hata yeye asingepata fursa hiyo ambayo alieleza kuwa ina manufaa kwake na kwa wawekezaji wengine.

Edda alisema mbali na serikali kuweka mazingira mazuri lakini bado kuna baadhi ya matatizo ambayo yanawakabili ikiwamo wingi wa kodi zinazokusanywa na serikali.

Alisema zipo taasisi nyingi za serikali ambazo zinakusanya kodi na tozo kwenye hoteli na kwamba huwa maofisa wa taasisi hizo wanakwenda kwa nyakati tofauti hali ambayo alisema wakati mwingine huwa inasababisha usumbufu.

Hivyo, aliomba tozo hizo pamoja na kodi ziunganishwe kwenye eneo moja ili ukusanyaji wake usilete shida kwa wawekezaji na kwamba wamekuwa wakilipa kwa sababu ni utaratibu uliowekwa na serikali.

"Mimi ukiacha hii hoteli ninamiliki pia viwanda vidogo vya kuchakata mpunga na mafuta ya alizeti, vilevile nipo kwenye sekta ya usafirishaji nina mabasi yangu yanafanya safari kati ya Jiji letu la Mbeya na wilayani huko, kwahiyo nawasihi wanawake wenzangu wasiogope kuingia kwenye biashara," alisema Edda.

Diwani wa Mwakibete ilipojengwa hotel hiyo, Lucas Mwampiki aliiomba serikali kujenga barabara inayopita katika eneo hilo kwa kiwango cha lami ili kumwekea mwekezaji huyo mazingira rafiki zaidi ya biashara.

Alisema barabara hiyo ina urefu wa mita 500 pekee na kwamba ikikamilika hata wananchi wa kata hiyo watakuwa wanapata huduma nzuri.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, akimkabidhi cheti Mkurugenzi wa Hoteli ya ECHA Luxury Villa, Edda Mosha, katika uzinduzi wa hoteli hiyo juzi, cheti hicho kilitolewa na Chama cha Wakulima, Wafanyabiashara na Wenye Viwanda (TCCIA). **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Madaktari kutoka China kutoa matibabu Mbeya

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

MADAKTARI bingwa kutoka China wamewasili katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya kwa ajili ya kutoa huduma za kibingwa kwa wananchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Dk. Godlove Mbwanji, aliwatambulisha madaktari hao mwishoni mwa wiki na kusema kuwa watashirikiana na madaktari wa hospitali hiyo kutoa huduma za kibingwa kwa wagonjwa.

Alisema hospitali hiyo ilipokea madaktari hao wanne ambao walipelekwa katika hospitali hiyo na Wizara ya Afya baada ya kuwasili nchini, kwamba mbali na kushirikiana na madaktari wazawa lakini pia watabadilishana uzoefu.

Dk. Mbwanji alisema madaktari hao wamebobea katika magonjwa mbalimbali na hivyo watasaidia kuokoa maisha ya wananchi wa mikoa ya nyanda za juu kusini ambao watapata huduma hizo jirani badala ya kuzifuata katika maeneo mengine ikiwamo nje ya nchi.

"Huduma zitakazotolewa na madaktari hawa zitasaidia kuwapunguzia wananchi gharama, baadhi ya huduma hizi huenda wangelazimika kuzifuata Hospitali ya Taifa Muhimbili lakini watazipata hapahapa," alisema Dk. Mbwanji.

Dk. Mbwanji alisema hospitali hiyo inapokea wagonjwa kutoka katika mikoa yote ya nyanda za juu kusini pamoja na wengine kutoka nchi jirani na kwamba wengi wanakuwa wameshindikana kutibiwa kwenye hospitali za rufani za mikoa.

Aidha, aliishukuru Wizara ya Afya kwa kuwapeleka madaktari hao kwa maelezo kuwa huduma za kibingwa ni muhimu kwenye hospitali hiyo ya kanda kutokana na kuwa na uhaba wa madaktari wa kundi hilo.

# Serikali yapewa kongole uwekaji ruzuku mbolea

**Na Nebart Msokwa,** MBOZI

VIONGOZI wa Kanisa la Kilutheri la Afrika Mashariki (KKAM) Dayosisi ya Nyanda za Juu Kusini wameipongeza serikali kwa kuamua kuweka ruzuku kwenye mbolea.

Wamesema hatua hiyo imewapunguzia wakulima gharama za uzalishaji.

Askofu wa KKAM Dayosisi ya Nyanda za Juu Kusini, Dk. Edward Mwaikali, aliyasema hayo juzi wakati wa ibada maalumu ya kuadhimisha siku 70 tangu kanisa hilo lilipoanza kutoa huduma katika ukanda huo pamoja na uzinduzi wa Parishi ya Mlowo.

Ibada hiyo ilifanyika kwenye Usharika wa Mlowo uliopo katika Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe, mgeni rasmi alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Ileje, Anna Gidalya ambaye alimwakilisha Mkuu wa Mkoa huo, Waziri Kindamba.

Alisema ruzuku hiyo itasaidia wakulima kuongeza uzalishaji wa mazao na hivyo kuwa na uhakika wa chakula pamoja na kukuza pato lao wenyewe na taifa kwa kuuza ziada ya mazao hayo ndani na nje ya nchi.

Dk. Mwaikali alisema msimu wa kilimo uliopita wakulima walishindwa kuzalisha kwa tija kutokana na bei ya mbolea kuwa juu kuliko miaka iliyopita na hivyo wengi walishindwa kumudu kununua.

Alisema hali hiyo ni moja ya vitu vilivyosababisha bei ya vyakula mwaka huu kupaa na hivyo kuwa na tishio la njaa katika baadhi ya maeneo nchini.

"Tunaishukuru serikali kwa kuamua kuleta mbolea ya ruzuku, tunaamini hii itasaidia wakulima kuongeza uzalishaji kwa nchi nzima, hali ilikuwa mbaya sana msimu uliopita maana bei ilikuwa juu sana ya mbolea," alisema Dk. Mwaikali.

Mkuu wa Wilaya ya Ileje, Gidalya alisema baada ya serikali kuweka ruzuku kwenye mbolea bei imeshuka na kwamba hakuna aina ya mbolea ambayo inauzwa kwa zaidi ya Sh. 70,000 tofauti na msimu uliopita ambapo ilikuwa inauzwa kwa zaidi ya mara mbili.

Alisema kwa sasa serikali inaendelea kuwaandikisha wakulima kwenye maeneo mbalimbali ili waingizwe kwenye mfumo wa kunufaika na mbolea hizo ambazo alisema kwa sasa zipo katika maeneo yote nchini.

Hivyo, aliwataka wakulima kujitokeza kujiandikisha ili wanufaike na ruzuku ya mbolea hiyo kwa maelezo kuwa utaratibu uliopo kwa sasa hakuna mtu atakayenufaika na mbolea ya ruzuku hiyo kama hatakuwapo kwenye mfumo ulioandaliwa.

"Hata sisi viongozi wa serikali tulikuwa tunapata shida sana, kila sehemu tulikokuwa tunakwenda kufanya mikutano na wananchi swali la mbolea lilikuwa lazima liulizwe, sasa serikali yetu imeamua kutuwekea ruzuku ili kutupunguzia mzigo, ni wajibu wa wakulima kuchangamkia sasa," alisema Gidalya.

Hivyo, aliwaomba viongozi wa dini nchini kusaidia kuliombea taifa ili liendelee kuwa na amani ili maendeleo yaendelee kupatikana.





## Viongozi UVCCM wapewa angalizo

**Na Peter Mkwavila,** BAHI

MWENYEKITI mstaafu wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) wilayani Bahi, amewataka viongozi wa umoja huo kutobweteka na kulewa na madaraka badala yake wafanye kazi ya kukisaidia chama hiko kimaendeleo.

Hassan Kidoke alitoa rai hiyo juzi alipozungumza na vijana wa wilaya hiyo kwenye mkutano mkuu wa uchaguzi wa viongozi watakaongoza kwa miaka mitano.

Kidoke aliwataka viongozi waliochaguliwa kushika nafasi ngazi mbalimbali, wasibwete na madaraka waliyopata bali wakisaidie chama na jamii kujikwamua kiuchumi.

"UVCCM inatarajia kuona vijana wanafanya kazi za kujiingizia kipato cha kiuchumi pamoja na kuhakikisha Chama Cha Mapinduzi (CCM) kinafufuka kupitia kwao katika kutekeleza ilani zake," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Munkunda alisema nafasi walizochaguliwa zitumike kukemea maovu vikiwamo vitendo vya rushwa.

Alisema nafasi hizo walizochaguliwa watambue wamepewa dhamana na vijana wenzao ili kuwatumikia na kuleta mabadiliko ndani ya chama na jumuiya hiyo.

Pia aliwataka vijana hao kutotumiwa na wagombea wa jumuiya zingine kuwafanyia kampeni zenye rushwa kwa kuwa CCM inahitaji viongozi wenye uadilifu na sifa ya kuongoza.

Katika uchaguzi huo Mwenyekiti wa UVCCM Wilaya ya Bahi aliyechaguliwa ni Jastin Sangula.

# Ajali 1,700 zaripotiwa barabarani miezi minane

## • Magari ya serikali yaongoza

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KIKOSI cha Usalama Barabarani nchini kimetaja takwimu mbalimbali za ajali mwaka huu, kikibainisha kuwa ndani ya miezi minane ya mwanzo ajali 1,177 zilitokea huku 135 zikiwa za magari ya serikali, sawa na asilimia 11.5.

Kutokana na hali hiyo, kikosi hicho kimetoa elimu kwa madereva wa magari ya serikali na kuwataka kuacha mihemko kwa kuwa hawako juu ya sheria.

Akizungumza mwishoni mwa wiki katika mafunzo maalum ya elimu ya usalama barabarani kwa madereva wa magari ya viongozi wa serikali na wabunge jijini hapo, Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Wilbroad Mutafungwa, alisema ajali hizo za magari ya serikali zimetokea kwa kipindi cha Januari hadi Agosti 2022.

Kamanda Mutafungwa alisema ili kudhibiti ajali, elimu ya usalama barabarani kwa madereva wa serikali ni muhimu kwao kwa kuwa wanapaswa kulinda uhai wao na wateja wao kwa kuheshimu na kutii sheria.

Alisema madereva hao wanapaswa kujitambua kuwa hawako juu ya sheria na wanapaswa kutii sheria kama madereva wengine.

"Waache kutumia vyeo na ukuu wa viongozi wao ambao siyo madereva wa magari ya serikali kwa kuwa wameajiriwa kwa majukumu mengine na siyo udereva tu, dereva hapaswi kuwa na mihemko na anatakiwa kujiepusha na 'makandokando' yanayoweza kupelekea apoteze weledi katika kazi zake, mfano ulevi na kuheshimu sheria ya mwendokasi," alisema.

Alisisitiza wataendelea kusimamia sheria bila kumwonea dereva yeyote na atakayebainika hatua za kisheria zitachukuliwa ikiwamo kuwafungia au kufuta leseni.

Akizungumzia takwimu hizo za ajali, alisema ndani ya kipindi hicho, vifo vyote vilikuwa 1,038 ambapo kati yake, vifo 90 vilitokana na ajali za magari ya serikali, sawa na 8.7 huku majeruhi wa magari hayo wakiwa 211.

Katika kipindi cha mwaka 2020, Kamanda Mutafungwa alisema ajali zote zilizotokea zilikuwa 1,714 na kati ya hizo ajali 260 zilikuwa za magari ya serikali na kusababisha vifo 82, sawa na asilimia 6.5.

"Kwa mwaka 2021 ajali zote zilizotokea zilikuwa 1,698 kati ya hizo ajali 158 zilitokana na magari ya serikali sawa na asilimia 9.3. Vifo vilikuwa ni 1,245. Kati yake, ajali za magari ya serikali ni vifo 94 sawa asilimia 7.6," alifafanua.

Naibu Waziri Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sagini alisema elimu hiyo iliyotolewa kwa madereva hao ni muhimu kutolewa kwa viongozi wao huku akisisitiza sheria kuchukuliwa kwa yeyote atakayekiuka.



Aliyekuwa Mwenyekiti wa UVCCM Wilaya ya Bahi, Hassan Kidoke, akizungumza wakati akiwaaga vijana (hawapo pichani), baada ya kumaliza kipindi chake cha miaka mitano kwenye mkutano mkuu wa uchaguzi uliofanyika kwa ajili ya kuwapata viongozi watakaongoza kwa kipindi kingine jijini Dodoma jana. Kulia ni Halima Zuberi msaidizi wa usimamizi wa uchaguzi huo na Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Mwankunda (wa pili kulia). **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Waziri: Utaratibu uzingatiwe kufuta kaya 158,000 TASAF

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, ameagiza kufanyika utaratibu mzuri wa kuziondoa nyumba 158,000 ambazo zipo kwenye Mpango wa Kusaidia Kaya Maskini (TASAF) kutokana na kufanikiwa kujikwamua na umaskini.

Pia amewataka viongozi wapya wa Kamati ya Taifa ya TASAF kufuatilia majina hewa ya baadhi ya walengwa ambao hawakustahili kuingizwa kwenye mpango huo.

Waziri Mhagama alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki jijini Dodoma alipozindua kamati ya uongozi wa TASAF iliyoteuliwa hivi karibuni baada ya iliyokuwapo kumaliza muda wake.

Alisema walengwa hao ambao wamehitimu kwenye mpango huo wanatakiwa kuondolewa ili wengine waingie kwa ajili ya kupata msaada wa kujikwamua kiuchumi na kuondokana na umaskini. "Ninaomba muwaondoe polepole walengwa hao na siyo kuwafukuza bila kuwapa maelekezo yoyote ya namna ya kuendeleza mitaji waliyoanzisha kupitia TASAF, tukiwapa elimu itasaidia," alisema Mhagama.

Pamoja na hayo, alielekeza kamati hiyo kuwatembelea walengwa ili kubaini kero zao zinazowakabili na kuzitafutia ufumbuzi.

Aliwapongeza TASAF kutokana na kufanikiwa kupeleka wanafunzi 1,200 katika vyuo vya elimu ya juu pamoja na kupata mikopo huku akiahidi kwa mwaka huu wanafunzi wengi zaidi watapelekwa.

Katibu wa Ikulu, Moses Kusiluka aliahidi kuendelea kushirikiana na viongozi walioteuliwa wa kamati hiyo ili mipango waliyonayo isikwame.

Mkurugenzi wa TASAF, Ladislaus Mwamanga, alisema katika mpango wa pili awamu ya tatu watasaidia kuwapeleka vyuo vikuu zaidi ya wanafunzi 1,000, akibainisha kuwa kwa sasa kuna maombi zaidi ya 3,000 ya walengwa wa mpango huo.

"Tunashukuru tunakwenda vizuri katika mpango huo tunashukuru pia kwa fedha kuongezwa kwa ajili ya kusaidia walengwa," alisema Mwamanga.

Mwenyekiti mpya wa kamati hiyo, Peter Ilomo alisema wako tayari kutekeleza maagizo yote yaliyotolewa na serikali.



# Mafunzo maalum yatolewa Zanzibar ukaguzi wa meli

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Khadija Khamis Rajabu, amewataka wahitimu wa mafunzo ya ukaguzi wa masuala ya meli kuyatumia vyema mafunzo waliyopatiwa ili kufikia lengo lililokusudiwa.

Katibu Mkuu huyo alitoa rai hiyo jana wakati akifunga mafunzo hayo katika ukumbi wa mikutano wa Mamlaka ya Usafiri Baharini (ZMA) Malindi, Zanzibar.

Alisema serikali kupitia Wizara ya Ujenzi inathamini usalama wa wananchi wake kupitia usafiri wa baharini, hivyo itaendelea kuhakikisha inawawezesha watendaji wake kwa kuwajengea uwezo kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao.

Alisema uongozi wa wizara kupitia ZMA itahakikisha Zanzibar inakidhi vigezo vya kimataifa katika usimamizi wa usalama wa baharini.

Mkurugenzi Mkuu wa ZMA, Sheikha Ahmed Mohamed, alisema mamlaka hiyo imeamua kumleta mkufunzi kutoka Afrika Kusini kwa lengo la kuwapatia mafunzo hayo watu wengi kwa wakati mmoja.

Alisema kukamilika kwa mafunzo hayo ambayo yalianza Septemba Mosi mwaka huu, kunakwenda kuongeza nguvu kwa wakaguzi kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi.

Mkufunzi wa Mafunzo hayo kutoka Afrika Kusini, Kapteni Andre Goncharko, aliipongeza Serikali ya Zanzibar kwa kumwamini na kumpa kazi hiyo ya kuendesha mafunzo kwa watendaji mbalimbali wa taasisi za serikali, akisisitiza uamuzi huo utawajengea uwezo watendaji hao.

Katibu Mkuu alitunuku vyeti kwa wanafunzi 28 waliohitimu mafunzo hayo ya ukaguzi wa meli kutoka taasisi mbalimbali za serikali na watendaji kutoka taasisi wanazoshirikiana nazo.

# Waziri apata mbinu kuzuia uvuvi haramu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar, Suleiman Masoud Makame amewataka wavuvi wa Kisiwa cha Kojani, Pemba kuwa walimu kwa wengine ambao wanaendelea na shughuli za uvuvi haramu katika maeneo ya hifadhi za bahari na kusababisha kupungua kwa samaki baharini.

Suleiman alitoa rai hiyo ofisini kwake mjini Zanzibar juzi alipozungumza na wavuvi wa Kojani kwa lengo la kuwa na ushirikiano wa karibu kati ya wavuvi na wizara hiyo.

Alisema uvuvi haramu unarudisha nyuma juhudi za serikali kutokana na matumizi mabaya ya rasilimali za bahari kwa kutumia dhana zisizokubalika kisheria.

Mwakilishi wa Kojani, Hassan Hamad Omar aliiomba wizara hiyo kuendelea kutoa elimu zaidi kwa wavuvi kuhusu matumizi sahihi ya bahari kwa kufuata sheria ili kuvua kwa tija na kuzingatia maslahi kwa taifa.

Wavuvi hao walisema wako tayari kubadilika na kutoa ushirikiano kwa taasisi husika pamoja na kuwa walimu kwa wavuvi wengine ambao wanaendelea kuharibu mazingira ya bahari kwa kufuata sheria ya uvuvi ambayo imeeleza matumizi sahihi ya rasilimali za bahari.



Makamu Mwenyekiti wa Chama cha ACT- Wazalendo, Othman Masoud Othman (wa tatu kushoto), akimsalimia mtoto Saluwa Said wa Bububu Jazira Zanzibar aliyebebwa na baba yake, wakati akiwa katika ziara ya kichama Wilaya ya Magharib A Unguja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makamu wa Rais ahimiza kuzitumia fursa za uwekezaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman, ameitaka Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini A Unguja kuitumia fursa ya uwekezaji wa miradi ya maendeleo.

Amesema kuna tatizo kubwa kwa halmashauri kuona uwekezaji unawezekana tu pale wanapokuwa na eneo lao wakati sheria zinaruhusu kuingia ubia na wananchi ili faida kupatikana kwa pande mbili hizo.

Aliyasema hayo jana katika Soko la Kinyasini wilayani humo baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara kuwa soko halikidhi mahitaji yao.

Othman alisema kama halmashauri hawana eneo la kujenga soko kubwa zaidi ya hilo ambalo litachukua wafanyabiashara wengi, ni vyema kufanya ubia na wananchi ili kupata eneo litakalokidhi mahitaji.

Makamu wa Rais alisema serikali inadhamira kuwa na sayansi na teknolojia ya kilimo ili Zanzibar ijitosheleze kwa chakula.

Alisema Zanzibar ikizalisha chakula kwa wingi itaondokana na utegemezi wa chakula kutoka nje.

Alisema pia itakapozalisha vyakula kwa wingi ikiwamo mifugo, itakidhi soko la utalii kwa sababu nyama ya ng'ome, kuku na mayai inategemea soko kubwa kutoka Tanzania Bara.

"Tukizalisha chakula kwa wingi hakuna atakayelia njaa maana hivi sasa hata nyama na mayai tunaagiza kutoka Tanzania Bara wakati upo uwezekano wa kuzalisha hapa hapa," alisema.

Baadhi ya wafanyabiashara wa soko hilo la Kinyasini walisema wanakabiliwa na kero nyingi ikiwamo miundombinu ya soko hilo kutokuwa rafiki kwa biashara zao.

Mariyam Yussuf, mmoja wa wafanyabiashara hao, alisema nyakati za mvua maji hutuama sokoni huko hali ambayo huleta usumbufu kwa wananchi wanaofika kununua bidhaa.

"Umebahatika leo umekuja na mvua imenyesha, ninadhani umejionea mwenyewe jinsi maji yalivyotuama hapa," aliwasilisha kilio chao.

Alisema soko hilo ni dogo, hivyo halikidhi mahitaji ya wafanyabiashara, akiomba serikali kutatua kero hizo.





# Moto ulivyoua watoto wanne, kujeruhi watatu

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

WATOTO wanne wamefariki dunia huku wengine watatu wakiokolewa baada ya nyumba waliokuwa wamelala, kuungua katika mgodi wa almasi wa Mwadui wilayani Kishapu mkoani Shinyanga.

Watoto waliopoteza maisha kutokana na tukio hilo la moto, ni Cecilia Richard (14), Clarence Richard (6), Thadeo Richard (3) na Aisha Ashraf mwenye umri wa miaka sita.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Jackson Mwakagonda, akizungumza jana na Nipashe kwa njia ya simu, alisema tukio hilo la ajali ya moto lilitokea juzi majira ya saa sita usiku ndani ya mgodi huo wa almasi.

Alisema ndani ya nyumba hiyo walikuwa wamelala watoto saba na wazazi hulala kwenye nyumba nyingine kutokana na nyumba za mgodi huo kuwa ndogo.

Aliongeza kuwa ajali hiyo ilitokana na mmoja wa watoto hao kuwasha jiko la umeme na kuliacha likiwaka na kusababisha tukio hilo.

"Kwenye nyumba hiyo walikuwa wamelala watoto saba na baada ya moto kutokea waliobahatika kuokolewa ni watoto watatu, lakini wanne waliteketea kwa moto," alisema Mwakagonda.

Alitoa wito kwa wazazi kuacha tabia ya kuwaacha watoto walale peke yao bila ya uangalizi ili kutosababisha majanga kama hayo ya moto.

# Wazee walaani mauaji

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

BARAZA la Wazee Mkoa wa Shinyanga limelaani vitendo vya mauaji ya wazee vinavyotokana na imani za kishirikina ambavyo vimeanza kujitokeza upya.

Katibu wa Baraza la Wazee mkoani Shinyanga, Anderson Lyimo, alibainisha hayo jana alipozungumza na Nipashe, akisema vitendo hivyo vinasikitisha kwa kuwa vilikuwa vimeisha.

Alisema wanalaani na kupinga vikali mauaji ya kinyama dhidi ya mzee mwenzao Sophia Dotto (66), mkazi wa Kijiji cha Kazuni, Kata ya Bukeni wilayani Shinyanga ambaye aliuawa na watu wasiojulikana, akituhumiwa kuwa mshirikina.

"Baraza la Wazee mkoani Shinyanga tunalaani na kupinga vikali mauaji ya kinyama dhidi ya wazee kuanza kuibuka upya sababu ya imani potofu za kishirikina," alisema Lyimo. "Tunaliomba Jeshi la Polisi liwasake na kuwakamata watu wote waliohusika na mauaji haya ya mzee mwenzetu Sophia Shija pamoja na kuwachukulia hatua kali za kisheria, ili kudhibiti mauaji haya ya watu wasio na hatia kuendelea," aliongeza.

Septemba 20, mwaka huu, katika Kijiji cha Kazuni, Kata ya Bukene wilayani Shinyanga, kulitokea tukio la mauaji ya Sophia Dotto (66) ambaye aliuawa kwa kushambuliwa kichwani na watu wasiojulikana nyumbani kwake majira ya saa mbili usiku, unyama huo ukihusishwa na imani za kishirikina.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Janeth Magomi, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kubainisha kuwa upelelezi wa awali unaonyesha bibi huyo aliuawa kwa imani potofu za kishirikina.

Alisema wanamshikilia mtoto wa kiume wa marehemu kwa mahojiano kuhusu tukio hilo huku wakiendelea kuwatafuta wahusika wa mauaji hayo na kutoa wito kwa wananchi kuacha tabia ya kuendekeza imani potofu za kishirikina.



Sehemu ya nchi kavu pembezoni mwa mwalo wa Mswahili katika Ziwa Viktoria, wilayani Nyamagana mkoani Mwanza ikitumika kama eneo la kutupia taka, ingawa si rasmi kwa shughuli hiyo. **PICHA: VITUS AUDAX**

# RC awataka watendaji kuepuka unyang'anyi

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

MKUU wa Mkoa wa Kagera, Albert Chalamila, amewataka watendaji wa kata na maofisa tarafa mkoani humo kufanya kazi kwa uadilifu na kuepuka k uwa wanyang'anyi wa mali za umma.

Pia amewataka kutokuwa chanzo cha migogoro ya wananchi na kutojihusisha na vitendo vya rushwa ili kuimarisha amani na usalama katika mkoa huo.

Akizungumza katika kikao cha pamoja na watendaji wa kata na maofisa tarafa kutoka wilaya zote za mkoani humo mwishoni mwa wiki, Chalamila alisema Rais Samia Suluhu Hassan hakuwatuma wawe chanzo cha migogoro kwa wananchi badala yake wasimamie sheria na kuisaidia jamii kuondokana na umaskini.

Chalamila alisema kuna baadhi ya watendaji waliopo visiwani badala ya kuwasaidia wananchi kufanya uvuvi bora, wanashiriki katika vitendo vya uvuvi haramu.

"Hii ni kwa sababu nanyi 'mmejipiga pini', badala ya kuepuka uvuvi haramu mnakwenda kuugeuza chanzo cha mapato yenu, mnaruhusu watu kutumia makokoro na mitumbwi isiyoruhusiwa na kila mwezi mnapewa pesa.

"Mnayafanya haya na mwisho wa siku mnasema samaki wameisha ziwani kwa sasa samaki ambaye angenunuliwa kwa Sh. 2,000 ananunuliwa kwa Sh. 10,000, mnasababisha ugumu wa maisha kwa wananchi, " alionya Chalamila.

Ofisa Tarafa ya Rwamishenye, Jovin Rutainulwa, alisema wamepokea maelekezo ya mkuu wa mkoa na wanakwenda kuyafanyia kazi kwa kutenda mema katika jamii kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi.

"Mheshimiwa mkuu wa mkoa, tunakushukuru kwa kutuita na kwa maelekezo yako, tunakuahidi kwenda kuyafanyia kazi ili kuhakikisha mfumo wa kisiasa unakaa vizuri na tunatekeleza ilani ya chama kilichoko madarakani kwa manufaa ya wananchi," aliahidi Rutainulwa.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Kyebitembe wilayani Muleba, Majura Samueli, alisema migogoro ya mirathi imekithiri katika wilaya hiyo na kutokana na maelekezo waliyopewa, wanakwenda kuishughulikia na kuhakikisha inapatiwa ufumbuzi katika ngazi ya kata badala ya kuwaacha wahusika kwenda ngazi ya wilaya kulalamika.

HABARI KIMATAIFA

# 1,600 wafariki dunia mafuriko Pakistan

**ISLAMABAD,** PAKISTAN

MAFURIKO yanayoendelea nchini Pakistan yamesababisha vifo vya watu takribani 1,600 tangu Juni mwaka huu pamoja na kuikumba theluthi moja ya nchi hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na RFI, Waziri Mkuu wa Pakistan Shehbaz Sharif, katika mkutano wa umoja wa mataifa unaoendelea New York, alielezea kwa uchungu nchi yake ilivyo haribiwa, huku akinyoosha kidole cha lawama kwa nchi zinazochafua mazingira.

Alisema mafuriko mabaya yaliyoikumba Pakistan msimu huu wa kiangazi ni utangulizi kwa sayari nzima kuwa inaathiriwa na mabadiliko ya tabia nchi.

"Ninaposimama hapa moyo wangu na akili yangu vinaelekezwa katika nchi yangu, huwa nahisi kama ninatembelea mojawapo ya maeneo yaliyoathiriwa na mafuriko, kwa siku 40 mchana na usiku tumeangukiwa na gharika," alisema.

"Katika 'Ground Zero' ya mabadiliko ya tabia nchi, mamilioni ya wahamiaji wa hali ya hewa bado wanatafuta sehemu ndogo ya ardhi, ambako wanaweza kukimbilia, sehemu kavu ili kuweka hema zao, wakiomboleza ndugu zao waliowapoteza, huku wakifikiria maisha yao ya baadaye na riziki zao," alisema.

Aliongeza kuwa ni wakati wa kujiuliza sio nini kinachoweza kufanyika bali ni nini kifanyike, akieleza kuwa kinachotokea Pakistan hakipaswi tu kuhusisha nchi yake, na kwamba nchi yake iko kwenye orodha ya nchi 10 zilizoko hatarini zaidi na mabadiliko ya tabia nchi, akisisitiza kuwa ni busara kutarajia angalau mwonekano wa haki kwa hasara na uharibifu huo.

"Tunapotoka kwenye mkutano huu wa mwezi Agosti, na tunazungumza juu ya migogoro kama huko Ukraine, swali ninalojiuliza ni je, tutakuwa peke yetu? Itabidi tusimamie mzozo huu peke yetu, tukiachwa kwa hatima yetu, kwa shida ambayo hatukusababisha," aliuliza katika mkutano huo wa UN.

Inaelezwa kuwa mafuriko nchini Pakistan yamesababishwa na mvua kubwa yenye upepo mkali, ambao nguvu yake inaongezeka kutokana na ongezeko la joto duniani.

Maofisa nchini humo wanasema mafuriko hayo yamefunika theluthi moja ya nchi eneo lenye ukubwa wa Uingereza, yakiharibu nyumba, biashara, barabara, madaraja na mazao ya kilimo.

Akiwa ziarani nchini humo mwezi Septemba, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, alieleza kuwa hajawahi kuona uharibifu wa tabia nchi wa kiwango hicho, huku akitoa wito kwa wachafuzi wa mazingira kukomesha hali hiyo kwa kuwekeza zaidi katika nishati ya mafuta. **RFI**



Wananchi wakiyakabili maji ya mafuriko ambayo yanatajwa kuikumba theluthi moja ya eneo zima la Pakistan. **PICHA: MTANDAO**

# China, India zaigeuzia mgongo Russia

**BEIJING,** CHINA

HATIMAYE China na India zimetoa wito wa kufikiwa kwa makubaliano ya kumaliza vita nchini Ukraine hatua inayoashiria kwamba washirika hao wa Russia sasa wanaonyesha kuigeuzia mgongo sera ya uvamizi.

China na India wametoa wito huo kwenye mkutano wa kilele wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UN), unaoendelea mjini New York Marekani.

Baada ya wiki ya kuongezeka kwa ukandamizaji dhidi ya uvamizi wa Russia kwenye hadhara hiyo kuu ya UN, Waziri wa Mambo ya Nje wa Russia, Sergei Lavrov, alipanda jukwaani na kuyashambulia mataifa ya magharibi kwa kile alichokitaja kama kampeni ya chuki dhidi ya Russia.

Inaelezwa kuwa, hakukuwa na taifa lolote kubwa lililoiunga mkono Russia, hata China ambayo siku chache kabla ya Russia kuivamia Ukraine mwishoni mwa mwezi Februari mwaka huu iliapa kuimarisha mahusiano yake na Rais wa Russia, Vladimir Putin.

Waziri wa Mambo ya Nje wa China, Wang Yi, alitoa wito kwa Russia na Ukraine kujizuia ili kuepusha mzozo huo kusambaa zaidi, lakini pia kutoathiri zaidi mataifa yanayoendelea.

"China inaunga mkono juhudi zozote za azimio la amani katika mzozo wa Ukraine, kipaumbele cha msingi ni kuandaa mazungumzo ya amani," alisema Wang.

Wakati wa ziara ya UN, Wang alikutana na Waziri wa Mambo ya Nje wa Ukraine, Dmytro Kuleba, katika mazungumzo yao ya kwanza tangu vita hivyo vilipoanza, ikielezwa kuwa mwanzoni mwa mwezi huu Putin alikiri kwamba China ina wasiwasi, kuhusiana na mzozo huo, kwenye mazungumzo kati yake na Rais Xi Jinping.

Maofisa wa Marekani walielezea ahueni kutokana na hatua hiyo ya China ya kupunguza ushirika na Russia kutokana na vita hivyo na kusema Beijing imekataa ombi la kupeleka vifaa vya kijeshi, na kuilazimisha Russia kugeukia Korea Kaskazini na Iran kama wasambazaji wake.

Kwa upande wa India inaelezwa kuwa ina mahusiano mazuri na Marekani lakini ina mahusiano ya kihistoria na Russia, ambayo imekuwa msambazaji wake wa silaha kwa muda mrefu.

Waziri wa Mambo ya Nje wa India Subrahmanyam Jaishankar, alisema "wakati mzozo wa Ukraine ukiendelea kufukuta, mara nyingi huwa tunaulizwa msimamo wetu na jibu letu kila wakati ni la moja kwa moja na la kweli," alisema na kuongeza;

"India iko upande wa amani na itaendelea kusimamia hilo kwa uthabiti, tuko upande unaotaka mazungumzo na diplomasia kama njia mwafaka ya kumaliza mzozo huo," alisema.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Russia, Sergei Lavrov, kwenye mkutano na waandishi wa habari alikataa kujibu swali la iwapo kumekuwapo na shinikizo kutoka kwa China, huku kwenye hotuba yake, akitaka kuyamwagia lawama mataifa ya magharibi.

"Marekani tangu kumalizika kwa vita baridi imekuwa ikijiweka kama mjumbe wa Mungu ulimwenguni na mwenye haki ya kufanya lolote, wakati wowote," alisema.

Pia aliulaumu Umoja wa Ulaya (EU) akiufananisha na chombo cha kibabe na kusema uongozi wa umoja huo ulilazimisha kiongozi wa taifa moja wanachama Rais wa Cyprus Nicos Anastasiades, kusitisha mkutano aliopangwa baina yao.

Aidha, ilielezwa kuwa Lavrov aliyakosoa mataifa ya magharibi kwa kutojihusisha na Russia, akieleza kuwa hawajawahi kukataa kufanya nao mawasiliano.

Taarifa zinaeleza kuwa mataifa hayo yanaangazia vikwazo zaidi dhidi ya Russia baada ya Putin kutangaza nia ya kuongeza wanajeshi na kutoa kitisho cha kutumia silaha za nyuklia, na kuapa kutotambua kura ya maoni iliyopigwa na Russia kwa lengo la kuyanyakua maeneo manne inayoyakalia nchini Ukraine.

Katika hatua nyingine, Rais wa Ukraine Volodymyr Zelenskyy alilaani nia hiyo ya Russia ya kukusanya wanajeshi zaidi kupigana vita nchini mwake kwa kuifananisha kama uhalifu, na kutoa wito kwa vikosi vya Russia kuweka chini silaha zao.

Amesema kwenye ujumbe wake wa video kwamba ni bora kukataa kujiunga na jeshi, kuliko kufa kwenye ardhi ya kigeni kama mhalifu wa kivita, ikiwa ni mara ya pili kwa Zelensky kuwatolea wito kama huo watu wa Russia. **DW**

**endelea kusimamia hilo kwa uthabiti, tuko upande unaotaka mazungumzo na diplomasia kama njia mwafaka ya kumaliza mzozo huo," alisema.**

## Utafiti: Somo Uraia linapuuzwa shuleni

**Na Elizabeth Zaya**

UTAFITI uliofanywa na Taasisi ya HakiElimu umeonyesha kupuuzwa somo la Uraia shuleni na kuonekana halina umuhimu.

Vilevile, utafiti huo umebainisha upuuzwaji huo ni kwenye mitaala ya elimu, upatikanaji wa walimu wake na namna linavyofundishwa kwenye shule za sekondari.

Utafiti huo ambao uliangazia mchango wa elimu ya uraia shule za sekondari katika kumwandaa kijana kujifunza na kushiriki vyema katika michakato ya kidemokrasia nchini, umebaini kikwazo kikubwa ni mtaala kwa somo hilo na idadi ndogo ya walimu wake.

"Kwa mfano utafiti ulibaini kwamba hakuna walimu waliobobea katika somo hilo la uraia. Kinachofanyika inapoonekana hakuna mwalimu mahususi wa kufundisha, anaambiwa mwalimu yeyote afundishe hata kama hajasomea kufundisha somo hilo," anasema Mtafiti wa kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe, Perpetua Kalimasi.

"Tumebaini kwamba mitaala yetu ya elimu katika eneo la somo hilo nayo ina changamoto, haijatiliwa mkazo maudhui na mbinu za ufundishaji za kuwaandaa wanafunzi juu ya mawanda mapana ya ufahamu juu somo hilo," anasema.

Kwa mujibu wa mtafiti huyo, wamebaini elimu ya uraia itolewayo shuleni ina mchango mdogo katika kumsaidia kijana wa kitanzania kujifunza na kushiriki shughuli za kisiasa na kidemokrasia.

"Mfano katika eneo la mtaala kwenye somo hilo, kwa kiwango kikubwa haumpi mafunzo stahiki mwanafunzi yatakayomsaidia aelewe vyema na kushiriki shughuli za kidemokrasia katika ngazi mbalimbali katika nafasi yake na hata walimu wengi wanaofundisha somo hilo, hawana maarifa stahiki yanayowawezesha kufundisha na kuwaanda vijana," anabainisha Kalimasi.

Kaimu Mkurugenzi wa HakiElimu, Godfrey Boniventura, alisema mwishoni mwa wiki kuwa taasisi hiyo inapendekeza kufanyike mapitio ya mtaala wa elimu ya uraia ili kutilia mkazo maudhui na mbinu za ufundishaji kwa ajili ya kuwaandaa wanafunzi na vijana kuhusu mambo ya uraia na umuhimu wa ushiriki wao katika demokrasia na kupata maarifa ya uongozi mapema.

Alisema wanapendekeza serikali kupunguza umri wa vijana kupiga kura kutoka miaka 18 hadi 14, ili kutoa fursa kwa vijana hao kuanza kushiriki shughuli za kijamii na maendeleo mapema kwa kuwa huo ni umri ambao wanatambua na kupambanua mambo vizuri.

Mapendekezo mengine ni kuboresha ufundishaji wa somo hilo darasani, ikiwamo kusisitiza mawasiliano ya karibu zaidi kati ya walimu na wanafunzi.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, akimkabidhi tuzo Mwenyekiti aliyemaliza muda wake kuiongoza Kamati ya Taifa ya Uongozi ya TASAF, Dk. Moses Kusiluka, ya kutambua mchango wake wakati wa uongozi. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Ladislaus Mwamanga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bil. 4/- kutumika kunoa vijana kufuga kibiashara

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

ZAIDI ya Sh. bilioni nne zimetengwa kwa ajili ya mafunzo ya ufugaji wa kisasa kwenye vituo atamizi vinane katika mikoa mitatu kwa lengo la kuwawezesha kufuga kibiashara.

Vituo hivyo vitakuwa kwenye mikoa ya Tanga, Mwanza na Kagera, vitasimamiwa na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI), pamoja na Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo Tanzania (LITA).

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Tixon Nzunda, aliyasema hayo wakati akifunga mafunzo ya siku mbili ya wasimamizi wa vituo atamizi vya ufugaji mifugo kibiashara kwa vijana yaliyofanyika kwenye Chuo cha Mafunzo ya Mifugo Kampasi ya Morogoro.

Alisema dhamira ya serikali ni kuwajengea uwezo vijana kupitia mikopo ili kukuza uchumi kupitia biashara ya mifugo.

Nzunda alisema katika kutekeleza dhamira hiyo wizara hiyo imeamua kufungua milango kwa vijana kupitia sekta ya mifugo na kwamba vituo hivyo vitasaidia kuwabadilisha vijana kifikra kuhusu ufugaji.

Alisema vijana waliopatiwa mafunzo kwenye vituo hivyo ni waliohitimu masomo ya taaluma ya mifugo ngazi ya astashahada, stashahada na shahada ambao wapo mitaani hawana kazi.

Alisema vituo hivyo vitasaidia kupunguza tatizo la ajira, kuongeza uzalishaji wa mifugo na mazao yake kwa kuzingatia viwango, kuongeza kipato cha vijana na taifa kwa ujumla.

Nzunda alisema mafunzo yataanza kwa mwaka wa fedha 2022/23 na katika awamu ya kwanza vijana 240 wamesailiwa kupewa mafunzo hayo na jumla ya ng'ombe 2,400 watanunuliwa na kila kituo kitapewa ng'ombe 300.

Katibu Mkuu alisema kila kituo kinakuwa na washiriki au wawekezaji 30 wa kiume na wa kike na kila mmoja atapewa mifugo 10 ya kuilea.

Katibu Mkuu huyo alizitaka LITA na TALIRI kuhakikisha kazi hiyo inaanza kutekelezwa kwa wakati na kwamba fedha zilizotolewa kwa kazi hiyo zisitumike kwa ajili ya kuendeshea ofisi wala kazi nyingine yoyote nje ya kazi iliyokusudiwa na serikali. Nzunda alisema vituo hivyo vitasaidia kuwabadilisha vijana kifikra kuhusu ufugaji, kupunguza tatizo la ajira, na kuongeza uzalishaji wa mifugo na mazao yake kwa kuzingatia viwango na kuongeza kipato cha vijana na taifa kwa ujumla.

Aliwataka vijana waliochaguliwa kujiunga na vituo atamizi kuwa na moyo wa kujituma na kujitambua kwamba wao ni wawekezaji ambao wameingia kuwekeza kwenye sekta ya mifugo.

Alishauri taasisi za kifedha kuwasaidia vijana kuingia kwenye ujasiriamali hasa sekta ya mifugo kwa kufuga kisasa kwa kuwapatia mikopo ili wainuke kiuchumi.

Pamoja na hayo, alisema jukumu la serikali ni kutoa fedha na kuwaandalia mazingira ya kuwaweka pamoja kwa kuunda vyama vidogo vya ushirika vya wafugaji, ili waanze kufuga kisasa na kuweza kukopesheka.

Aliwataka wasimamizi wa vituo hivyo kuwa wabunifu na kuhakikisha wanasimamia utekelezaji wa mwongozo uliotolewa kuhusu vituo hivyo.

Katibu Mkuu huyo aliwataka kuwajenga vijana hao kuwa na uwezo wa kufuga kisasa kwa vitendo, kuwa na mahusiano na mawasiliano mazuri ambayo yatawasaidia katika masoko ya mifugo na mazao ya mifugo watakayokuwa wanazalisha.

Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Vyuo vya LITA, Dk. Pius Mwambene, alisema wakala unakwenda kuanzisha vituo sita katika kampasi za Kikulula (Kagera), Mabuki (Mwanza) na Buhuri (Tanga) na kwamba kila kituo kitachukua vijana 30 ambao watafundishwa namna ya kufuga kibiashara kwa muda wa miezi 12.

Mkurugenzi wa TALIRI Kanda ya Mashariki, Dk. Zabron Nziku alisema taasisi yake itasimamia kwa weledi mpango huo ili vijana waliochanguliwa awamu ya kwanza kujiunga kwenye vituo atamizi wakipate kilichokusudiwa.

Mtumishi wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Dk. Moses Olenesele, aliwataka vijana waliopata nafasi ya kujiunga na mafunzo hayo kuhakikisha wanaitumia fursa hiyo vizuri kwa kuwa serikali imeweka matumaini kwa vijana hao kuja kuwa wafanyabiashara wakubwa wa mifugo iliyo bora.

Mkurugenzi Msaidizi wa Utafiti wa Mifugo na Mafunzo wa wizara hiyo, Dk. Hassan Mrutu alisema kuwa jitihada kubwa zimewekwa ili kuhakikisha vijana wanabadilisha mtazamo wao kwa kutumia ufugaji wa kibiashara kwenye ng'ombe, mbuzi na hata kondoo kwa kuwainua kiuchumi.

# DC awataka wanawake kuchangamkia mikopo

**Na Mary Geofrey**

MKUU wa Wilaya ya Namtumbo, Dk. Julius Mingu, amewataka wanawake wilayani humo kuchangamkia fursa za mikopo inayotolewa na taasisi za fedha ili kujikwamua kiuchumi.

Amesisitiza wanawake kuchukua mikopo kwa ajili ya kuboresha biashara zao kwa kiwango wanachoweza kurejesha.

Dk. Mingu alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki wakati akizindua tawi jipya la Kampuni ya BRAC Tanzania Finance Ltd (BTFL) ikiwa ni sehemu ya matawi yake mawili yaliyozinduliwa mkoani Ruvuma.

"Ninaamini kuwa familia yeyote yenye mafanikio na ustawi bora, inakuwa na mama ambaye ni imara na anayejitambua. Hivyo, mikopo hii siyo tu msaada kwa kinamama, bali kwa familia nzima.

"Ninawaomba BRAC kuwasaidia kinamama kwa kuwafundisha pia maarifa ya fedha ili watumie mikopo yao ipasavyo na kuendelea kukuza biashara zao na familia kwa ujumla," alisema.

Alipongeza juhudi za BTFL za kusogeza huduma za mikopo karibu na wananchi na kuiomba ishirikiane kwa karibu na wanawake hao ili kujenga uhusiano mzuri na kuwasaidia kwa kuwapa elimu ya biashara na utunzaji wa fedha.

Matawi hayo mawili yaliyozinduliwa katika wilaya za Namtumbo na Nyasa, ni sehemu ya matawi tisa mapya yaliyoanzishwa mwaka huu na kuifanya BTFL kuwa na jumla ya matawi 164 nchini.

Tawi la BRAC la Nyasa lilizinduliwa na Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya ya Nyasa, Paulo Lugongo ambaye aliwasisitiza wanawake wanaochukua mikopo, kuitumia katika biashara husika na siyo shughuli zingine ambazo hazitawaingizia kipato kama vile sherehe na ngoma za wanawake.

Meneja wa Mkoa wa Ruvuma wa BRAC, Shali Albert, alisema wanajivunia kwa kumpa kipaumbele mwanamke, ili ajiinue kiuchumi na kijamii.

Alisema kupitia mikopo ya masharti nafuu, wanawake wajasiriamali wanapata fursa za kukuza biashara zao, kuanzisha biashara mpya, kutoa ajira na pia kuchangia katika maendeleo ya familia zao.

"BRAC tunaelewa matatizo ya wanawake katika kupata huduma za kifedha na kwa kulitambua hilo, tumejikita kuwa na bidhaa ambayo inamruhusu mwanamke yeyote kupata mkopo kwa ajili ya kuwekeza katika biashara yake," alisema.

**BURUDANI**

# SHAMSA FORD ATAKA NDOA NYINGINE

**Na Mwandishi Wetu**

NYOTA wa kike wa bongo muvi, Shamsa Ford, ameweka wazi kuwa anataka kuolewa tena baada ya kupata elimu ya kutosha kuhusu mahusiano ikiwa imepita miaka mitatu tangu atoke kwenye ndoa.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Shamsa aliweka picha yake na kuisindikiza kwa ujumbe huo ya kwamba yupo tayari kuolewa tena.

"Tangu nimetoka kwenye ndoa ni miaka 3 sasa. Nimejipa muda wa kutosha na kupata elimu kubwa juu ya mahusiano.

"Sasa hivi akili yangu imetulia nipo tayari kuolewa tena inshaaallah. Sitaki kuendelea kufanya zinaa mimi ni binadamu sijui mwisho wangu ni upi.

"Sitaki kuendelea kufanya zinaa. Inshaaallah Mwenyezi Mungu unipe mume mwenye kheri na mimi atayenipenda, kunithamini na kunitunza.

"Mume atayempenda mwanangu na atayesimama kuwa baba bora kwa mwanangu maana kila ninapokwenda nipo naye."

Shamsa alifunga ndoa na mfanyabiashara Rashidi Said 'Chidi Mapenzi' mwaka 2016 na kisha ndoa yao kuvunjika baadaye.

Kabla ya kuolewa na Chidi, Shamsa alikuwa kwenye mahusiano na Dickson Matoke 'Dick' ambaye alizaa naye mtoto mmoja.





## KANYE WEST AMWANGUKIA KIM KARDASHIAN

**LOS ANGELES, Marekani**

RAPA wa Marekani, Kanye West amemwomba msamaha kwa "mfadhaiko wowote" aliomsababishia hivi karibuni mke wake wa zamani, Kim Kardashian.

Kanye ameomba msamaha huo kwa mke wake huyo waliyezaa naye watoto wanne kupitia mahojiano ya Kipindi cha Good Morning America kilichorushwa jana usiku.

Rapa huyo ambaye ni mfanyabiashara bilionea, amesema anamwomba radhi mkewe huyo kwa maudhi yoyote yaliyotokea katika kuwalea watoto wao hao.

"Huyu ni mama wa watoto wangu, na ninaomba msamaha kwa changamoto zozote ambazo nimemsababishia," alisema Kanye.

"Ninamhitaji sana mtu huyu asiwe na msongo wa mawazo na awe na akili timamu na mtulivu iwezekanavyo ili kuweza kuwalea watoto wetu."

Kanye amesema matatizo yote aliyomsababishia mzazi mwenzake, yanatokana na yeye kuhisi ananyimwa haki ya kuwalea watoto wao, North mwenye miaka tisa, Saint miaka sita, Chicago miaka minne na Psalm miaka mitatu.

Kanye pia amezungumzia suala la matamanio yake ya kuwania urais wa Marakeni.

Kanye mwenye umri wa miaka 45, na Kim miaka 41, walitalikiana mapema mwaka huu, kabla ya wawili hao kuanza kushambuliana kupitia mahojiano na mitandao ya kijamii.



## MAUA SAMA AJA NA ATM YA MUZIKI

**Na Mwandishi Wetu**

MSANII wa muziki wa Bongo Fleva, Maua Sama, ameibuka kivingine na kwa staili ya aina yake kwa kuzindua ATM maalumu kwa ajili ya kusikiliza na kutazama video za muziki wake.

Sama amesema uzinduzi huo wa ATM ya muziki itawawezesha mashabiki wake wengi kupata kile wanachokitaka kwa wakati.

Akizungumza na waandishi wa habari, Sama alisema hiyo ni sehemu ya ubunifu wa kuufikisha muziki wake mbali zaidi hasa kwa mashabiki wake.

Alisema amekuja na wazo hilo ambapo amewapa nafasi mashabiki wake kusikiliza na kuangalia video mpya za ngoma zake kwa wakati mmoja.

"Hii ni fursa nzuri kwa mashabiki wangu kusikiliza na kuangalia muziki wangu kwa wakati mmoja na kuwapa nafasi ya kufanya hivyo sehemu yoyote walipo," alisema.

# HAIKUWA RAHISI KUIFUNGA UGANDA - KOCHA STARS

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA wa Timu ya Taifa ya Tanzania 'Taifa Stars', Honour Janza, amesema haikuwa rahisi kuifunga Uganda kama watu wengi wanavyodhani, badala yake kumetokana na jitihada na wachezaji, pamoja na benchi la ufundi, ikiwamo kubadilisha mifumo na kikosi pia.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mechi hiyo ya kirafiki ya kimataifa iliyo kwenye Kaenda ya FIFA, Stars ikishinda bao 1-0 juzi usiku kwenye Uwanja wa Modern Benghazi nchini Libya, kocha huyo aliwasifu wachezaji wake kuwa walijituma, kukimbia, kukaba nafasi na kufanya kila kitu kwa usahihi, ingawa walikutana na timu bora ya Uganda Cranes.

"Uganda ni wazuri, wana nguvu, wana utimamu wa mwili, hata kwa wachezaji wao mmoja mmoja ni wazuri, wanaweza kukulazimisha kufanya makosa, pia wanaweza kubadilika kutokana na mazingira. Unaona kipindi cha pili walibadilika kabisa, ilibidi na sisi tufanye kazi ya ziada," alisema kocha huyo raia wa Zambia.

Akizungumza wachezaji wake, Janza alisema kumekuwa na mabadiliko makubwa ya kiuchezaji, na amewasifia kwa kujituma, kukimbia sana, kukaba na kuziba mianya yote ya wapinzani wao kiasi cha kuibuka na ushindi huo.

"Kila mchezaji alitumia nguvu zake, kukimbia, kubaka na kuziba mianya, na hivyo ndiyo vitu ambavyo nilikuwa nataka kuviona kwenye kikosi hiki," alisema.

Bao pekee kwenye mechi hiyo lilifungwa dakika ya 28 na Simon Msuva ikiifanya Stars kulipa kisasi cha kuondolewa hivi karibuni kwenye michuano ya kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

Kwenye mechi hiyo Stars ilifanya mabadiliko kwenye kikosi chake, ikiwachezesha baadhi ya wachezaji ambao hakuwamo kwenye mechi ya kusaka tiketi ya CHAN kama Beno Kakolanya, David Luhende, Abdallaah Mfuko, na Himd Mao ambao walianza.

TUPO TAYARI...



Wachezaji wa Simba kutoka kushoto; Denis Kibu, Nelson Okwa na Kennedy Juma, wakiwa mazoezini Zanzibar juzi kabla ya jana usiku kushuka Uwanja wa Amaan visiwani hapo kuivaa Malindi SC kwenye mechi ya kirafiki: **PICHA: SIMBA**

## Mkwawa Queens yapokelewa kishujaa Iringa

**Na Friday Simbaya, Iringa**

TIMU ya Mkwawa Queens ya mkoani Iringa, imepokelewa kishujaa na wakazi wa mjini Iringa ikitokea jijini Dodoma baada ya kufanya vizuri na kupanda daraja kucheza Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara (SWPL), huku Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Halima Dendego akijitolea kuwa mlezi mkuu wa timu hiyo.

Akizungumza jana kwa furaha na shangwe, Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Dendego kwenye hafla fupi ya kupokea timu hiyo iliyofanyika katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Iringa (Iringa Girls), alisema atahakikisha timu hiyo inapata malezi mazuri kwa kushirikiana na wadau huku akiahidi kuwatafutia wafadhili. "Hii ni heshima kubwa ambayo mmetupa mkoani Iringa, ukizingatia mkoa wetu hauna timu inayocheza ligi, kwa kweli mmetuheshimisha sana mabinti zetu baada ya kushuka daraja timu ya Lipuli FC msimu wa 2019/2020," alisema Dendego.

Aliwataka vijana hao kufanya kazi kwa bidii pamoja na mazoezi zaidi ili kuweza kufanya vizuri kwenye Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara na kuongeza kuwa huo ndio uchawi pekee wa mafanikio na hakuna mwingine zaidi ya huo na kujituma.

Katika hafla hiyo, kuliandaliwa chakula na vinywaji mbalimbali kama soda, juice, maji na shampeni, huku vijana wa Mkwawa Queens pamoja na benchi lao la ufundi wakijazwa noti kwa kila mmoja kupewa shilingi laki moja zilizotoka kwa wadau wa michezo mkoani hapo.

Timu za Amani ya Lindi na Mkwawa Queens zimepanda Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara na zitaanza kuwania taji hilo msimu huu wa 2022/23.

Ligi Daraja la Kwanza kwa Wanawake ambayo imeshirikisha timu sita; Mkwawa (Iringa), Amani (Lindi), Lengo (Arusha), Mapinduzi (Njombe), Ukerewe (Mwanza) na Allan Queens (Dar es Salaam), ilianza Septemba 12, mwaka huu na kumalizika jana katika Uwanja wa Fountain Gate jijini Dodoma.

Kwa upande wa timu za Allan Queens (Dar es Salaam) na Mapinduzi Queens ya Njombe zitasalia kwenye ligi hiyo (Daraja la Kwanza) baada ya kumaliza katika nafasi ya tatu na ya nne ambapo zitaungana na Mlandizi, Ilala, Oysterbay na TSC Queens zilizoshuka daraja kutoka Ligi Kuu huku zikiungana pia na Bunda Queens na Mwanza Queens ambazo zimepanda Daraja la Kwanza msimu huu kutoka Ligi ya Mabingwa wa Mikoa (WRCL).

Katika michezo ya mwisho ambayo imepigwa jana asubuhi na jioni, Lengo imepigwa mabao 2-0 na Allan Queens hivyo kupoteza michezo yake minne na kuambulia ushindi katika mchezo mmoja tu, huku Mkwawa ikiwachapa vibonde Ukerewe Queens mabao 4-1 na Mapinduzi ikachapwa 2-1 na Amani.

Hivyo, Amani imemaliza ya kwanza na pointi 15, Mkwawa ya pili (12), Mapinduzi ya tatu (9), Allan pointi sita, Lengo (3) na Ukerewe Queens ikiambulia patupu.

## Biashara kibonde Championship

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Biashara United ambao ilishuka Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliomalizika, imeendelea kuwa kibonde kwenye Ligi ya Championship, baada ya kupokea kipigo cha bao 1-0 dhidi ya JKT Tanzania, mechi iliyochezwa juzi Jumamosi kwenye Uwanja wa Meja General Isamuhyo, Dar es Salaam.

Hiki ni kipigo cha pili kwa Biashara United, kwani kwenye mechi ya kwanza ilifungwa pia bao 1-0 kwenye mechi ya ufunguzi wa ligi hiyo dhidi ya Fountain Gate na kuifanya kutokuwa na pointi yoyote wala bao na kuweka mashakani ndoto yao ya kutaka kurejea kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Wakati Biashara United ikisuasua, wenzao walioshuka nao, Mbeya Kwanza wameendeleza ubabe kwa mara nyingine na dhamira ya kutaka kurejea Ligi Kuu Tanzania Bara kwa kuinyuka Pamba FC mabao 3-1, mechi ikichezwa Uwanja wa Nyamagana Mwanza, ukiwa ni ushindi wa pili mfululizo, kwani mechi ya raundi ya kwanza iliichapa Gwambina mabao 2-1.

Timu ya Mbuni FC, imeonekana kuwa tishio kwenye ligi hiyo kwani imepata ushindi mwingine wa mabao 3-0 dhidi ya Green Warriors kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha na kuendelea kujikita kwenye kilele cha msimamo wa ligi hiyo.

Kwenye mechi ya raundi ya kwanza, timu hiyo pia ilipata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Ndanda.

## Chipukizi kuendeleza moto Ligi Kuu ugenini

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BAADA ya kufanikiwa kuutumia vema uwanja wake wa nyumbani, timu ya Chipukizi FC imesema itaendeleza moto huo kwenye Ligi Kuu Zanzibar hata itakapocheza ugenini kwa mechi zijazo.

Chipukizi FC imecheza michezo minne nyumbani Kisiwani Pemba, katika Uwanja wa Finya na kushinda miwili, sare moja na kufungwa mchezo mmoja, hivyo kujikusanyia alama saba katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar yenye timu 16.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na Bodi ya Ligi, timu ya Chipukizi kuanzia mzunguko wa sita hadi wa 10 itacheza ugenini Kisiwani Unguja baada ya kucheza michezo mitano ikiwa nyumbani.

Chipukizi FC mchezo wake wa mwisho ikiwa nyumbani itapepetana na Wanajeshi wa Kipanga Septemba 30, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili Kocha Mkuu wa Chipukizi, Ali Bakar Khalfan, alisema kasi waliyoianza katika uwanja wa nyumbani ndio watakayoendelea nayo wakiwa ugenini Kisiwani Unguja.

Alisema kikosi chake amekiandaa vizuri kuhakikisha kinafanya vizuri ugenini kama ilivyokuwa katika uwanja wake wa nyumbani, Kisiwani Pemba.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**RASHFORD MWAKA MMOJA**
KLABU ya Manchester United itamwongezea mwaka mmoja mshambuliaji wake raia wa England, Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 24. (***Daily Star on Sunday***).

**DE GEA NAE KUONGEZWA**
MANCHESTER United pia inatafakari uwezekano wa kumwongezea mkataba mlinda mlango wao raia wa Hispania, David de Gea utakaomweka hadi mwaka 2024. Mkataba wa sasa wa kipa huyo mwenye miaka 31, utafikia kikomo mwishoni mwa msimu huu. (***Sunday Telegraph***)

**POCHETTINO ATAJWA VILLA**
KOCHA wa zamani wa Tottenham Hotspur na Paris St-Germain, Mauricio Pochettino yupo tayari kwa uwezekano wa kuinoa klabu ya Aston Villa ambayo kwa sasa ipo chini ya Steven Gerrard. (***Football Insider***).

**MADISON AWANIWA**
KLABU ya Newcastle inatarajia kuwasilisha dau jipya la kumsajili kiungo mshambuliaji wa Leicester City, James Madison mwenye umri wa miaka 25 katika dirisha la usajili la Januari baada ya kushindwa kumnasa mchezajji huyo kwenye dirisha la majira ya kiangazi lililofungwa hivi karibuni. (***Football Insider***).

**ARSENAL YAMFUATILIA MAJER**
ARSENAL imeendelea kumfuatilia kiungo wa klabu ya Rennes, Lavro Majer wakati mchezaji huyo alipokuwa akiichezea timu yake ya taifa ya Croatia siku ya Alhamisi na kuibuka na ushindi wa 2-1 dhidi ya Denmark. (Sunday Mirror).

**HARRIS AWINDWA CHELSEA**
CHELSEA inajipanga kulipa dau la pauni milioni 30 kumnasa kinda wa Fulham, Luke Harris mwenye umri wa miaka 17. Mshambuliaji huyo kinda amejumuishwa kwenye kikosi cha timu ya Taifa ya Wales kwa michezo ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Ubelgiji na Poland. (***Sunday Mirror***).

**ALLAN KUTIMKIA ARABUNI**
KIUNGO wa Everton raia wa Brazil, Allan mwenye umri wa miaka 31, amekubali kujiunga na klabu ya Al-Wahda iliyopo katika nchi ya Umoja wa Falme za Kiarabu. (***Football Inside***r).

**BUSQUETS AHUSISHWA MAREKANI**
KIUNGO wa Hispania, Sergio Busquets mwenye umri wa miaka 34, ambaye mkataba wake na Barcelona unamalizika mwishoni mwa msimu huu anahusishwa na kuhamia nchini Marekani ingawa kiungo huyo amesema bado hajafikia maamuzi kuhusu mustakabali wake. (***90 Min***).

**DE JONG NA BARCA**
KLABU ya Barcelona itafanya mazungumzo na kiungo wake, Frankie de Jong mwenye umri wa miaka 25, mwishoni mwa msimu kuhusu madeni anayoidai klabu hiyo na kima cha mshahara kwa siku zijazo. (Que T'hi Jugues, via Sunday Mirror).

**BELLERIN KUONGEZEWA**
BARCELONA wanatarajiwa kujaribu kuongeza mkataba wa mlinzi, Hector Bellerin mwenye umri wa miaka 27, kwenda zaidi ya msimu ujao, ingawa mchezaji huyo anaweza kutaka kurejea katika klabu ya Real Betis ambayo alichezea kwa mkopo msimu uliopita. (***Fichajjes.net***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# KOUNDE HATIHATI KUKOSA EL CLASICO

**Pia Depay, Dembele na De Jong watafuatiliwa hali zao baada ya kupata matatizo wakiwa...**

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA imethibitisha kuwa Jules Kounde amepata jeraha la msuli wa paja akiwa na kikosi cha Ufaransa na sasa kuna shaka kama ataweza kucheza dhidi ya Real Madrid kwenye mchezo wa El Clasico mwezi ujao.

Kounde alicheza dakika 23 pekee za ushindi wa mabao 2-0 wa Ufaransa dhidi ya Austria kwenye Ligi ya Mataifa ya Uefa Alhamisi kabla ya kutolewa na nafasi yake kuchukuliwa na William Saliba wa Arsenal.

Katika taarifa iliyotolewa Jumamosi asubuhi, Barcelona ilithibitisha kuwa Kounde amefanyiwa vipimo na sasa yuko mbioni kukaa nje ya uwanja.

"Majaribio ya Jumamosi asubuhi yamethibitisha kuwa Jules Kounde ana jeraha la kwenye msuli wa paja la kushoto. Kwa sababu hiyo ana uwezekano wa kukaa nje ya dimba kwa muda," ilisema taarifa hiyo.

Wakati Barcelona haijaweka muda kwa umma kuhusu kupona kwa Kounde, gazeti la AS limeripoti kwamba, huenda akakosa safari yao ya kwenda Real Madrid Oktoba 16, mwaka huu kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga.

Barca pia watacheza na Inter Milan kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya mara mbili kabla ya safari hiyo ya Santiago Bernabeu, huku wakiwakaribisha Bayern Munich mwishoni mwa Oktoba. Kounde sasa pia anakabiliwa na wakati mgumu wa kuhakikisha anakuwa fiti kabla ya kuanza kwa Kombe la Dunia Novemba mwaka huu nchini Qatar.

Pia ameungana na mchezaji mwenzake wa Barca, Ronald Araujo kwenye orodha ya walio majeruhi baada ya kupata jeraha la paja akiwa na timu ya Taifa ya Uruguay.

Pia Memphis Depay, Ousmane Dembele na Frenkie de Jong watafuatiliwa hali zao baada ya kupata matatizo wakiwa kwenye majukumu ya timu zao za taifa.

Barcelona wapo nyuma kwa pointi mbili dhidi ya Real Madrid kwenye msimamo wa LaLiga, wakishinda mechi tano na kutoka sare moja kati ya sita za ufunguzi msimu huu.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 355

MECHI KALI
ENGLAND
VERSUS
GERMANY
1 | 2.48
X | 3.16
2 | 2.86

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KOULIBALY: NITAPAMBANA KURUDISHA NAMBA



**DAKAR, Senegal**

MLINZI mpya wa Chelsea, Kalidou Koulibaly amekiri kwamba, amepata wakati mgumu kuzoea maisha katika Ligi Kuu England, lakini ameapa kushinda tena nafasi yake ya kuanza kwenye kikosi cha kocha mpya, Graham Potter.

Alipowasili kwa pauni milioni 40 msimu huu wa majira ya joto, Koulibaly alikuwa chaguo la kwanza chini ya kocha wa zamani wa 'Blues' hao, Thomas Tuchel, lakini alikutana na utofauti baada ya kuwekwa benchi katika mechi ya kwanza ya kocha Potter, huku akiwaanzisha mabeki watatu Marc Cucurella, Thiago Silva na Cesar Azpilicueta.

Akizungumza kwa Le Quotidien, Koulibaly alisisitiza kuwa hana matatizo na Potter na alikiri kwamba bado hajafikia kiwango bora zaidi kule Stamford Bridge.

"Kocha mpya alikuja na mawazo mazuri," alisema Koulibaly.

"Yeye ni kocha wa kweli. Alifanya mambo mazuri na Brighton.

"Ana miongozo na matarajio. Ni juu yangu kuwa mvumilivu, ni juu yangu kuonyesha kwamba ninastahili kucheza, kuonyesha katika mazoezi kwamba kocha anaweza kuniamini. Hakutakuwa na tatizo.

"Sisi pia tuko katika wiki za kwanza, ni kawaida kwa kocha kuwategemea wachezaji ambao wamezoea nembo ya Chelsea na ambao wamekaa hapo kwa muda mrefu sana.

"Nikiwa fiti asilimia 100 hakutakuwa na shida, nitacheza tena."

Koulibaly pia alitafakari uamuzi wake wa kujiunga na Chelsea baada ya miaka nane na Napoli.

"Unajua, ni chaguo la maisha," alisema. "Nilitaka kubadilisha klabu. Nilihisi kama nimetoa kila kitu kwa Napoli. Ilifika wakati nilitaka kubadilisha maisha, kujipa changamoto na kujitupa kwenye changamoto mpya.

"Chelsea ilifika na haikuchukua muda mrefu kwangu kuchagua. Ni moja ya klabu tano bora duniani, zenye historia kubwa; timu ambayo imezoea kushinda. Sitaacha kuwashukuru (Napoli) kwa walichonipa, nilihisi ni wakati wa kugundua kitu kingine."

# Southgate ajipigia debe England

**LONDON, England**

KOCHA wa England, Gareth Southgate amesisitiza kuwa yeye ndiye mtu sahihi wa kuiongoza timu hiyo kwenye Kombe la Dunia nchini Qatar licha ya kuwa na matokeo mabaya.

Kufungwa na Italia Ijumaa na kushuka daraja katika Ligi ya Mataifa ya Uefa, na kuendeleza mfululizo wa kutoshinda hadi mechi tano katika mchakato huo, kumefanya wadau wengi kuwa na maoni tofauti juu yake.

Southgate alidhihakiwa na mashabiki wa England waliosafiri hadi kule jijini Milan kwenye Uwanja wa San Siro, lakini, licha ya kuwa chini ya shinikizo kubwa, amekuwa katika muda wake wa miaka sita wa kuinoa, hivyo anaamini anasalia kuwa chaguo bora zaidi kuipeleka timu hiyo Qatar.



"Bila shaka. Tunacheza na tumekuwa tukicheza na timu za kiwango cha juu na tutakuwa bora zaidi kwa hilo," alisema.

"Nina wachezaji wachanga haswa, ambao wamekuwa kwenye michezo hii watakuwa wamejifunza mengi kutoka kwao.

"Hapo zamani tulikuwa na mechi za kirafiki au mechi zozote na kisha tukaingia kwenye mashindano na ndiyo mara ya kwanza tunapata upinzani wa hali ya juu.

"Sasa tunajua kiwango, sasa tunajua tunachopaswa kuboresha na tutakuwa katika nafasi nzuri zaidi kwa kuwa na ubora wa mechi ambazo tumekuwa nazo."

Maoni ya Southgate yaliungwa mkono na nahodha wa England, Harry Kane, ambaye ana imani Simba Watatu hao watarejea katika ubora wao kwa ajili ya kuanza kwa michuano hiyo Novemba.

"Ninaamini tutahukumiwa jinsi tunavyocheza Qatar. Tuko katika moja ya wakati ambapo hauendi sawa. Tuna imani tunaweza kubadilisha hilo," alisema.

,121,030

# MULTIBETI BONUS SPORTPESA YANOGA, WENGI WASHINDA



Meneja Mawasiliano na Uhusiano wa SportPesa, Sabrina Msuya.

**Na Mwandishi Wetu**

IKIWA ni zaidi ya miezi mitatu tangu kuanzishwa kwa huduma ya Multibet Bonus ya SportPesa, washindi kibao wameanza kujishindia vitita zaidi ya shilingi milioni 10.

Akizungumza katika Ofisi za SportPesa Oysterbay, Dar es Salaam jana, Meneja Mawasiliano wa kampuni hiyo, Sabrina Msuya, alisema huduma ya Multibet Bonus imeanza kutoa washindi wa vitita vinono kwa wateja wao tangu msimu huu mpya wa ligi wa 2022/23 ulipoanza.

"Katika kitu ambacho kimetushangaza siku za hivi karibuni, imekuwa kawaida kwa wachezaji wa Multibet Bonus kushinda kuanzia Sh. milioni 10 na kuendelea. Hii inatokana na asilimia kubwa ambayo tumeiweka kwa wateja wetu ambapo ukicheza unaweza kupata bonasi mpaka asilimia 750 ya ushindi wako.

"Kwa mfano ndani ya mwezi huu tu, washindi wawili wameshinda mamilioni ya shilingi, tukianzia na Vincent Mwantellah aliyeshinda milioni 36 ambapo baada ya kodi alipata milioni 32 na Denis Mwakunza aliyeshinda milioni 17 na baada ya kodi alipata milioni 15 kama ambavyo tumeweza kuonyesha mikeka yao kupitia kurasa za mitandao yetu ya kijamii wa Instagram @tzsportpesa, mtandao wa Twitter @tzsportpesa na mtandao wa Facebook Sportpesa Tanzania.

"Kwa namna ambavyo washindi hawa wameshinda, Denis alipata zaidi ya milioni nne na Vincent alipata Sh. milioni 11 na ushehe kama nyongeza kwenye ushindi wao wa multibet," alisema Sabrina.

Sabrina anaendelea kueleza kuwa kwa sasa SportPesa wamejikita zaidi katika kuboresha na kuwapa nafuu wachezaji wake ili waweze kufurahia namna ambavyo wanabashiri mikeka yao.

"Kama mnavyojua tumejitahidi kuweka mazingira rafiki ambayo yatamfanya kila mteja wetu kutumia huduma ama bidhaa zetu kulingana na uwezo wake.

Mfano mzuri ni pamoja na mteja wetu mwenye simu aina ya kitochi, sasa anacheza kwa USSD na SMS bila kukatwa makato ya aina yoyote na pia kwa wateja wetu wenye simu za Android ama smartphone wana 'download App' yetu na kucheza bila ya kuwa na bando.

Aidha, Sabrina aliwaasa Watanzania kutumia fursa ya kucheza mara nyingi kadri wanavyoweza ili waweze kushinda kama wengine ambao tayari wanafurahia matunda ya kucheza na SportPesa.

"Napenda kuwasisitiza kujitahidi kucheza mara kwa mara ili muwe na nafasi ya kushinda kama wachezaji wetu wengine".

# JACKPOT MECHI WIKI HII

## BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 27/09/22 | 21:45 | Portugal vs Spain | 2.28 | 3.22 | 3.12 |
| 02. 27/09/22 | 21:45 | Ukraine vs Scotland | 2.47 | 3.28 | 2.77 |
| 03. 28/09/22 | 01:00 | CA Atlanta vs Chaco For Ever | 2.80 | 2.85 | 2.55 |
| 04. 28/09/22 | 01:05 | Raya2 Expansion vs M. Zacatecas | 2.43 | 3.14 | 2.70 |
| 05. 28/09/22 | 05:00 | Mexico vs Colombia | 2.70 | 3.21 | 2.65 |
| 06. 28/09/22 | 18:00 | Inter Turku vs Haka | 2.22 | 3.41 | 3.11 |
| 07. 29/09/22 | 01:00 | Coritiba vs Ceara CE | 2.40 | 3.00 | 2.85 |
| 08. 29/09/22 | 01:00 | Club Celaya vs CF Atlante | 2.26 | 3.04 | 3.04 |
| 09. 29/09/22 | 03:00 | Cuiaba MT vs America Mineiro MG | 2.24 | 2.90 | 3.24 |
| 10. 29/09/22 | 03:45 | Goias vs Botafogo RJ | 2.46 | 3.10 | 2.70 |
| 11. 29/09/22 | 03:45 | Atletico Mineiro vs Palmeiras | 2.27 | 3.18 | 3.23 |
| 12. 29/09/22 | 18:00 | Honka vs HJK Helsinki | 2.72 | 3.05 | 2.47 |
| 13. 29/09/22 | 21:30 | Barracas Central vs Gimnasia y Esgrima | 2.85 | 3.15 | 2.42 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMATATU - 26/09/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2372 | Jeonnam Dragons vs Busan I Park | 1.98 | 3.29 | 3.43 |
| 13:30 | 1228 | Gwangju vs Ansan Greeners | 1.39 | 4.43 | 6.50 |
| 14:00 | 3890 | Sheffield Wednesday U23 vs Wigan U23 | 3.14 | 4.51 | 1.79 |
| 16:00 | 1576 | Baalama vs Al-Arabi | 2.43 | 3.14 | 2.70 |
| 16:00 | 4259 | Reading U23 vs Millwall U23 | 1.96 | 3.57 | 3.23 |
| 16:00 | 5890 | Finland U19 vs Portugal U19 | 5.89 | 4.81 | 1.38 |
| 18:00 | 1238 | Serbia U19 vs France U19 | 3.50 | 3.69 | 1.84 |
| 19:30 | 5304 | Chateauroux vs Dunkerque | 2.21 | 3.19 | 3.14 |
| 20:00 | 2125 | Gais vs Lindome Gif | 1.14 | 7.06 | 12.74 |
| 20:00 | 4996 | Hammarby W vs Linkopings W | 2.85 | 3.44 | 2.18 |
| 21:00 | 1190 | Birmingham U23 vs Coventry U23 | 2.21 | 3.69 | 2.65 |
| 21:00 | 5242 | Sacachispas FC vs Deportivo Moron | 3.34 | 2.90 | 2.20 |
| 21:30 | 1308 | San Martin Burzaco vs Csyd Liniers | 2.45 | 2.69 | 3.13 |
| 21:30 | 1744 | El Porvenir vs Ferrocarril Midland | 4.22 | 2.94 | 1.91 |
| 21:30 | 1932 | Bracknell Town vs Hanwell Town | 2.05 | 3.70 | 3.10 |
| 21:30 | 3175 | Berazategui vs Claypole | 2.41 | 2.76 | 3.10 |
| 21:35 | 1429 | Los Andes vs CA San Miguel | 2.05 | 3.00 | 3.58 |
| 21:45 | 1110 | Hungary vs Italy | 3.85 | 3.22 | 2.00 |
| 21:45 | 1601 | England vs Germany | 2.48 | 3.16 | 2.86 |
| 21:45 | 2357 | Redditch United vs Rushall Olympic | 1.80 | 3.67 | 3.67 |
| 21:45 | 2600 | Beaconsfield Sycob vs Harrow Borough | 1.63 | 3.95 | 4.70 |
| 21:45 | 2803 | San Marino vs Estonia | 10.11 | 4.75 | 1.31 |
| 21:45 | 3408 | Montenegro vs Finland | 2.61 | 3.07 | 2.77 |
| 21:45 | 4272 | Romania vs Bosnia and Herzegovina | 2.15 | 3.18 | 3.44 |
| 21:45 | 4649 | Kings Langley vs Needham Market | 2.14 | 3.50 | 3.05 |
| 21:45 | 4677 | North Macedonia vs Bulgaria | 2.06 | 3.33 | 3.53 |
| 21:45 | 4844 | Hitchin Town vs St Ives Town | 2.00 | 3.24 | 3.43 |
| 21:45 | 5051 | Gibraltar vs Georgia | 12.06 | 5.83 | 1.23 |
| 22:00 | 1082 | Albion FC vs CA Fenix | 2.90 | 3.09 | 2.32 |
| 22:00 | 1147 | Shamrock Rovers vs UCD Dublin | 1.11 | 7.07 | 17.66 |
| 22:00 | 3431 | FC Cartagena vs Alaves | 2.60 | 3.15 | 2.65 |
| 22:00 | 4385 | Las Palmas UD vs Granada | 2.29 | 3.11 | 3.11 |
| 23:00 | 1893 | Aldosivi vs Central Cordoba | 2.70 | 3.10 | 2.46 |
| 23:00 | 2319 | Colon Santa Fe vs Argentinos Juniors | 2.55 | 3.04 | 2.65 |
| 23:30 | 2529 | Cobreloa vs Union San Felipe | 2.03 | 3.09 | 3.53 |
| 23:45 | 4871 | Atlas W vs Puebla FC W | 1.38 | 4.94 | 5.73 |

## JUMANNE - 27/09/2022

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 00:00 | 1522 | Deportivo Cali vs La Equidad | 2.61 | 3.15 | 2.51 |
| 01:00 | 2668 | Toluca W vs Uanl W | 4.93 | 4.44 | 1.49 |
| 01:05 | 3244 | Leon W vs Guadalajara W | 7.07 | 5.89 | 1.27 |
| 02:00 | 3501 | Jaguares de Cordoba vs Rionegro Aguilas | 2.94 | 2.89 | 2.42 |
| 02:00 | 4403 | CSA AL vs Tombense MG | 1.77 | 3.14 | 4.62 |
| 02:00 | 5943 | Deportes Temuco vs San Luis Quillota | 2.02 | 3.33 | 3.28 |
| 02:30 | 5392 | Santamarina vs Gimnasia Mendoza | 4.60 | 3.23 | 1.74 |
| 03:10 | 2800 | Ferro CO vs Estudiantes Rio Cuarto | 2.36 | 2.84 | 3.08 |
| 04:00 | 1155 | Alianza Lima vs Univ San Martin | 1.19 | 5.71 | 11.81 |
| 04:05 | 5646 | Atletico Nacional vs Patriotas FC | 1.42 | 4.22 | 6.27 |
| 14:30 | 2376 | CSC Dumbravita vs FC Politehnica Iasi | 3.80 | 3.30 | 1.95 |
| 16:00 | 5434 | Ripensia Timisoara vs U Craiova SA | 4.80 | 3.87 | 1.58 |
| 16:00 | 5489 | BFC Daugavpils vs Rigas Futbola Skola | 11.00 | 6.00 | 1.21 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Kiduku bingwa UBO, Mandonga duh...

INATOKA UK. 32

mchezo wa ngumi huku akiamini huo utakuwa mwanzo mzuri kwa mkoa huo kujiwekeza katika michezo.

"Kiduku kupigana na bondia kutoka Misri ni moja ya mwendelezo wa 'Royal Tour', ameshawafungulia, hivyo wizara tunajukumu kubwa la kuhakikisha tunafanya uwekezaji katika sekta ya uchumi ili uweze kukua zaidi na michezo kama hii iweze kuendelea ndani ya mkoa wetu," alisema Kihange.

Mbali ya pambano la Kiduku, bondia Karim Mandonga pambano lake halikuweza kupatikana mshindi kutokana na Kamisheni ya Ngumi za Kulipwa nchini (TPBRC) chini ya rais wake, Chaurembo Palasa, kulifuta kutokana na kuwapo makosa ya kisheria kwa mwamuzi, Habib Mkarafuu kufanya makosa ya kimsingi.

Wengine, Adam Lazaro alifanikiwa kumchapa kwa pointi Francis Miyeyusho 'Chichi Mawe' katika pambano la raundi kumi wakati Ibrahim Tamba akimpiga Alto Kyenga, Joseph Mchapeni ameendeleza utemi wake kwa Pascal Manyota kufanikiwa kumpiga kwa pointi wakati Bosco Bakari wakitoka sare na Malik Deo wa Mwanza sawa na Mrisho Mzelele dhidi ya Karim Omari.

Emilian Polino alifanikiwa kumchapa Osama Arabi wa Mtwara wakati Nasra Msami akimpiga Halima Bandora huku Shaban Ndaro akimpoteza kwa kipigo kizito mkongwe Seleman Galile.

# MGUNDA APATA MBINU

INATOKA UK. 32

Phiri hadi sasa ana mabao matatu mkononi kwenye michuano hiyo baada ya kufunga moja ugenini dhidi ya Nyasa Big Bullets na kisha kutupia yote mawili wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 2-0 Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Simba ambayo ipo Zanzibar bila kikosi chake kamili, kutokana na baadhi kuwa katika timu zao za taifa kipindi hiki cha Kalenda ya Fifa, baada ya kuivaa Kipanga FC keshokutwa, itarejea Dar es Salaam na kisha Oktoba 2, mwaka huu itashuka Uwanja wa Benjamin Mkapa kucheza mechi moja ya Ligi Kuu dhidi ya Dodoma Jiji FC kabla ya kuifuata Primeiro de Agosto.

# Michezo

Jumatatu Septemba 26, 2022
Nipashe

UKURASA 30



## Koulibaly: Nitapambana kurudisha namba

UTAUMIA WEWEEE...




Bondia Mtanzania, Twaha Kiduku (kushoto), akikichafua ulingoni dhidi ya Mmisri Abdo Khaled kwenye pambano la raundi 10 uzani wa Super Middle kuwania mkanda wa UBO Intercontinental, lililofanyika Uwanja wa Nangwanda Sijaona mkoani Mtwara juzi usiku. Kiduku alishinda kwa pointi. **PICHA: SAADA AKIDA**

# Mgunda apata mbinu za kuishika De Agosto

●●●Video zambeba, sasa awajaza ufundi mastaa wake Zanzibar kabla ya...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI jana akikiongoza kikosi chake kushuka dimbani kwenye mechi ya kirafiki dhidi ya Malindi SC ya Zanzibar, Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, tayari amewasoma wapinzani wao, Primeiro de Agosto ya Angola kuelekea mchezo wa raundi ya Kwanza wa Ligi ya Mabingwa Afrika.

Simba ipo visiwani Zanzibar ikijiandaa na mchezo huo utakaopigwa Oktoba 9 nchini Angola kabla ya kurudiana Uwanja wa Benjamin Mkapa Oktoba 16, mwaka huu na mshindi wa jumla atakata tiketi ya kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo inayoongoza kwa utajiri kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

Timu itakayotupwa nje itaangukia kucheza mechi za mchujo na timu zitakazovuka raundi ya kwanza ya Kombe la Shirikisho ili kuwania nafasi ya kucheza hatua ya makundi ya michuano hiyo ya pili kwa utajiri kwa ngazi ya klabu Afrika.

Jana usiku Simba ilijipima nguvu dhidi ya Malindi katika Uwanja wa Amaan kabla ya keshokutwa, Jumatano kushuka tena uwanjani hapo kucheza mechi nyingine ya kirafiki dhidi ya Kipanga FC ambayo nayo ina kibarua kigumu dhidi ya Club Africain ya Tunisia kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Lakini Mgunda, alimwambia mwandishi wetu kuwa, tayari ameziona baadhi ya video za Primeiro de Agosto na kubaini uchezaji wao, jambo ambalo anaendelea kulifanyia kazi katika michezo hiyo ya kirafiki Zanzibar.

"Primeiro de Agosto ni timu inayotumia nguvu na wachezaji wake wapo timamu, hivyo hatutakuwa na ulazima wa kucheza kama wanavyocheza wao, kazi kubwa iliyopo mbele yetu ni kuhakikisha tunaandaa kikosi ambacho kitacheza kiakili zaidi ili kukwepa kutolewa mchezoni," alisema Mgunda maarufu kama Pep Guardiola Mnene.

Alisema kikubwa watakachokifanya katika mchezo huo wa awali ugenini ni kucheza mchezo wao na si kuiga wa wapinzani wao ambao watakuwa uwanja wa nyumbani mbele ya mashabiki wao.

Primeiro de Agosto msimu huu inaelezwa kufanya usajili mkubwa, kikosi chake kikiundwa na wachezaji kutoka mataifa mbalimbali ikiwamo Ureno na Brazil na imefanya vizuri katika mchezo wake wa awali kwa kuitoa Red Arrows ya Zambia kwa jumla ya mabao 2-1 ikishinda bao 1-0 ugenini na nyumbani kutoka sare ya 1-1.

Lakini hilo si tatizo kubwa kwa Simba, kwani yenyewe ilipata ushindi mkubwa ugenini wa mabao 2-0 na kama huo nyumbani hivyo kuitoa Nyasa Big Bullets ya Malawi kwa jumla ya mabao 2-0.

Tayari mshambuliaji hatari wa Simba, Moses Phiri, ametoa ahadi ya kuendelea kushirikiana vema na wachezaji wenzake kuipambania timu yao kuweza kufika mbali kwenye michuano hiyo msimu huu.

INAENDELEA UK. 31

## Kiduku bingwa UBO, Mandonga duh...

**Na Saada Akida, Mtwara**

BONDIA wa ngumi za kulipwa nchini, Twaha Kiduku amefanikiwa kushinda mkanda wa UBO Intercontinental na kutetea mkanda wake wa ubingwa wa UBO Afrika uzani wa Super Middle dhidi ya Abdo Khaled wa Misri.

Katika pambano hilo ambalo lilipigwa juzi usiku kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona mkoani Mtwara, lilikuwa la raundi kumi.

Kiduku alikutana na upinzani mkali huku mpinzani wake akiwa mwepesi kukimbia kwenye maeneo yasiyo na madhara kwake na kuonyesha ubora wa hali ya juu kabla ya bondi huyo Mtanzania kutoka mkoani Morogoro kushinda kwa pointi.

Baada ya pambano hilo, Kiduku aliwashukuru Watanzania kwa sapoti kubwa waliyompa hususan serikali ya mkoa wa Mtwara hadi kufanikiwa kushinda ubingwa huo huku akitoa zawadi ya ushindi huo kwa mtoto wa mfanyabiashara, Said Salim Bakharesa.

"Nimecheza mapambano mengi magumu, nikiri mchezo huu dhidi ya Abdo Khaled nimepata ushindani mkubwa, kwa sababu ukiangalia bondia kama huyu huwezi kumpiga KO," alisema Kiduku.

Alisema bondia anayekimbiakimbia ulingoni ni vigumu sana kumpiga KO na kwenda naye hadi raundi ya 10 na kuibuka bingwa wa UBO Intercontinental na kutetea mkataba wangu wa UBO Afrika, amefanya kazi ngumu.

Naye Bondia, Abdo Khaled alisema alijiandaa vizuri na anafurahi kucheza pambano na Kiduku ambaye ni bondia mzuri na kuonyesha ushindani mkubwa licha ya kupoteza.

"Nafurahi kucheza hili pambano Tanzania, nimemwona Kiduku ni mzuri namuheshimu ni bondia mzuri, nakubali nimepoteza pambano kwa sababu mpinzani wangu alikuwa bora," alisema Khaled.

Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, ambaye alikuwa mgeni rasmi wa pambano hilo, alisema serikali itahakikisha wanakuza uchumi wa mkoani wa Mtwara ili kuvutia wawekezaji wengi katika sekta ya michezo.

Alisema amefurahi kuona wanaifungua upya Mtwara kupitia

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >